Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 19 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Usafiri Dar es Salaam kwa Mwaka 2002 *(The Annual Report and Accounts of Shirika la Usafiri Dar es Salaam Limited for the year 2002).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. FESTUS B. LIMBU):** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - (K.n.y. MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni yake kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 284

### Ujenzi wa Zahanati Vijijini

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. MWANNE I. MCHEMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikihamasisha wananchi kuchangia shughuli za maendeleo pale inapohitajika kufanya hivyo na kutoa kipaumbele katika huduma muhimu kama vile afya na kwa kuwa wananchi wengi wameitikia wito huo kwa kujenga zahanati vijijini na kwa kuwa, Serikali hupokea taarifa ya zahanati zilizokwishakamilika pamoja na kupokea maombi ya zahanati hizo ya kupatiwa wauguzi, waganga, vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika shughuli za matibabu:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka mahitaji yanayotakiwa kwenye zahanati hizo zilizokamilika ili kuondoa kabisa tatizo hilo?

(b) Je, ni vituo vya afya na zahanati ngapi zimekamilika hapa nchini na havitoi huduma?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inapeleka Wauguzi, Waganga, madawa na vifaa mbalimbali kwa kadri vinavyopatikana kupitia Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Afya.

Kwa mfano, mwaka 2003/2004 jumla ya zahanati mpya 235 na vituo vya afya 16 vilipelekewa makasha ya dawa. Aidha, watumishi waliajiriwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia vibali vilivyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa wauguzi, waganga, madawa na vifaa vinavyopelekwa havitoshelezi mahitaji, hii inatokana na ufinyu wa Bajeti uliopo.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa kuna jumla ya Vituo vya Afya 445 na Zahanati 4,051 nchini. Idadi hii inajumuisha vituo vya Afya na Zahanati za Serikali, Mashirika ya Umma, binafsi madhehebu ya dini na taasisi mbalimbali.

Kati ya vituo hivyo, vituo vya afya ambavyo havitoi huduma ni 6 na zahanati 115.

**MHE. AZIZA S. ALI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba Zahanati ambazo wananchi waliojitolea nguvu zao na kuzijenga na kutokupata huduma hawawatendei haki?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inawatendea haki wananchi wake. Kwa mfano, katika

mwaka huu wa fedha Serikali imetenga dawa katika zahanati 175 zitapata dawa na vituo vya afya 27 vitapata dawa. Kwa maana nyingine ni kwamba hivyo vituo ambavyo nimevielezea kwamba havijaanza huduma ni kwa sababu havijakamilisha utaratibu wa kupatiwa dawa pamoja na waganga. Lakini kwa kweli tuipongeze Serikali yetu imefanya kazi kubwa katika kuboresha afya ya wananchi. *(Makofi)*

Na. 285

**Ukosefu wa Barabara Morogoro Vijijini**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Morogoro Vijijini inasifika sana kwa uzalishaji wa matunda kwenye maeneo ya Lung'ala, Hewe, Bagilo, Tandai, Amini, Tegetero, Bulugi, Kivuma, Kibuko, Kibwaya, Changa, Mwarazi, Kalundwa na Mfumbwe:-

Je, kwa nini Serikali haijatenga fedha za kukarabati barabara zinazoenda kwenye maeneo hayo zikiwemo zile za Tomondo hadi Vuleni, Kungwe Vuleni na Bamba – Tegetero Kiroka hadi Kizinga?

**SPIKA:** Katika swali lililokwenda kwa Waziri Kijiji kimeandikwa kwa usahihi, Tegetero. Kwa hiyo, lijibiwe Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo la Mashariki mwa Wilaya ya Morogoro Vijijini linasifika sana kwa uzalishaji wa matunda kwenye maeneo ya Lung'ala, Hewe, Bagilo, Tandai, Amini, Tegetero, Buhigi, Kivuma, Kibuko, Kiwaya, Changa, Mwarazi, Kalundwa na Mgumbwe. Pia barabara za Tomondo – Kungwe – Mvule (km.6), Tegetero-Kifuru-Bamba (km.4) na Kiroka-Kizinga (km.4.5) zipo katika Wilaya ya Morogoro na zinaunganisha maeneo yaliyotajwa hapo juu ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa matunda.

Mheshimiwa Spika, hali ya matengenezo ya barabara zinazopita katika maeneo haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara za Madamu-Kinole (Tanda) (km.11.80) na Tandai-Tawa (km.14) zimekarabatiwa na MVIWATA kwa ufadhili wa Serikali ya Ufaransa,

barabara hizi zinahudumia vijiji vya Kiwaya, Mgumbwe, Kalundwa, Tandai, Kisambwa, Mkalazi na Amini.

(ii) Barabara ya Kinole (Tanda)-Tegetero (km.7) imekarabatiwa na *TASAF,* barabara hii inahudumia vijiji vya Bagilo, Tegetero, Hewe na Mifuru.

(iii) Barabara za Tegetero-Karunga (km.3.5) na Mafumba-Mkumbuluni-Bulugi (km.5.5) zimekarabatiwa na mradi wa *VTTP* chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswizi *(SDC),* barabara hizi zinahudumia vijiji vya Tegetero, Lubwe, Mkumbuluni, Bulugi, Mkalazi na Kirunga.

(iv) Barabara ya Tandai-Amani (km.4.5) imekarabatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Halmashauri, barabara hii inahudumia vijiji vya Tandai, Amini, Mfumbwe na Kiroka.

(v) Barabara za Kibwaya-Mfumbwe (km.5) na Tegetero-Hewe (km.4) zitakarabatiwa wakati wa utekelezaji wa mpango wa pili wa Mradi wa *TASAF.*

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara zilizotajwa hapo juu ni mbali ya matengenezo yanayofanywa kwenye barabara za mkoa zinazopita kwenye maeneo hayo na kuhudumiwa na *TANROADS,* Mkoa wa Morogoro. Pia ni mbali na matengenezo ya barabara za vijiji ambazo huhudumia na huendelezwa na vijiji vyenyewe kwa kupata huduma ya utaalamu wa shughuli za matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara kutoka Idara ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, barabara za Tomondo-Kungwe-Mvuleni,Togetero-Bamba na Kiroka-Kizinga ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziulizia kwa nini Serikali haitengi fedha za kuzikarabati barabara hizo za vijiji hivyo. Hivyo ni jukumu la vijiji husika kuzifanyia matengenezo barabara hizo kwa utaratibu niliosema.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo niliyatoa hapo juu ni wazi Serikali inaendelea na juhudi za ukarabati wa barabara zinazohudumia maeneo yanayozalisha matunda kwa wingi Wilayani Morogoro. Aidha, Serikali za vijiji katika maeneo yaliyotajwa zina wajibu wa kutengeneza, kukarabati na kujenga barabara za vijiji zinazounga kwenye barabara za Wilaya, Mkoa na barabara kuu kuhakikisha kuwa usafirishaji wa mazao ya matunda kutoka mashambani unafanywa kwa urahisi zaidi.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza katika jibu lao lilikuwa jibu na makengeza kidogo malyenge. Kwa sababu kijiji cha Mfumbwe hakihusiki kabisa na barabara ya Amini. Lakini hata hivyo inaendelea kutengenezwa. Sasa je, kwa kuwa ametaja ni mashirika tu ya MVIWATA na maeneo mengine yaliyoshughulikiwa na *TASAF.* Inaonyesha kabisa barabara hii Serikali haijaleta hata senti tano, ndiyo inaweza kuwapongeza wananchi wa Tandae kuunda vikundi vyao ya ile barabara, anaweza akambia Waziri angalau kutoa *road toll* ya mwisho kwa barabara hizi zilizotajwa hapa?

Pili, hizi barabara za vijijini tayari wanavijiji wenyewe wa Bamba na maeneo mengine wanavilima wenyewe. Kuna kadaraja kadogo tu ambayo tayari nimeshapeleka mchango wangu, unaweza ukasaidia mchango huo ili kuimarisha daraja la pale Bamba, maeneo ya pale Kioka ili wananchi Roholole-Changa-Kibwaya-Mfumbwe-Logo-Uponda-Mifurwe-Heo Bagilo wakasaidia daraja hilo? Ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika barabara ambazo zimekarabatiwa kuna Mfuko wa *TASAF,* kuna msaada wa Ufaransa na vile vile kuna fedha za Halmashauri. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali haijatoa chochote katika barabara hizi. Na hata hao kuwashawishi Wafaransa kusaidia pale hata ule Mfuko wa *TASAF* vile vile ni juhudi ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali lazima tuipongeze kwa kufanya kazi kubwa katika eneo hilo.

Pili, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba ametoa mchango wa kujenga daraja katika kijiji alichokitaja, namshukuru sana na nampongeza sana kwa juhudi anazozifanya si kwa daraja hili tu na kwa misaada mingine mingi anayoitoa katika Jimbo lake. Nakushukuru sana na kwamba Serikali kupitia ule mradi wa *VTTP* nayo itaunga mkono katika hilo daraja. *(Makofi)*

Na. 286

**Posta Meatu**

**MHE. ROBERT K. MASHALA (K.n.y. MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Meatu haina jengo la Posta lililojengwa kwa makusudi hayo na kwa kuwa Shirika hupanga kwenye majengo yasiyo rasmi kwa ajili hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga jengo la Posta Wilayani Meatu?

(b) Je, tangu Shirika la Posta Wilayani Meatu lianze limetumia kiasi gani cha fedha?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani kuhusu jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tangu Shirika la Posta Tanzania lianze kutoa huduma zake Meatu, hadi kufika mwisho wa mwaka wa 2004 Shirika lilikuwa limetumia shilingi 3,360,000/= kama gharama za kukodi Jengo la Posta Meatu. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mulyambatte kwamba Shirika litaweka mradi wa ujenzi wa Posta Meatu katika mpango wake wa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Mwanhunzi, Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu ni mji mdogo ulipangwa na kusanifiwa vizuri sana hapa nchini. Ni mji ambao unachanganya pamoja *(blend)* uoto wa asili, miti na majengo. Hivyo basi itabidi katika kusanifu jengo la Posta, Shirika litilie maanani mazingira mazuri ya Mwanhunzi.

Tarehe 19 Septemba, 2003 Mheshimiwa Mulyambatte na viongozi wa Wilaya ya Mwanhunzi walipata nafasi ya kutembelea na kukagua Posta ya Mwanhunzi.

Mheshimiwa Mulyambatte, kwa kushirikiana na uongozi na wananchi wamefanya kazi kubwa kusukuma maendeleo ya Meatu katika sekta ya mawasiliano na naomba wananchi na wapiga kura wake walielewe hilo na kuendelea kumpa moyo wa kufuatilia kero hizo. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Meatu linalingana sana na tatizo la Wilaya ya Bukombe. Wilaya ya Bukombe nayo haina kabisa jengo la Posta. Lakini wananchi wake wanapata shida na inabidi wasafiri muda mrefu kupata huduma hiyo. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wilaya ya Bukombe na Wilaya zingine ambazo hazina huduma ya Posta kuhusu kuleta huduma hizo kwenye Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba Wilaya ya Bukombe na baadhi ya Wilaya nyingine nyingi hazina huduma ya Posta lakini juhudi zinafanywa pale ambapo Shirika la Posta linaweza kupata huduma ya kukodi kwa njia ya unafuu zaidi inafanya hivyo na pale ambapo pana ulazima wa kujenga Posta tunafanya hivyo hivyo vile vile.

Posta zitakazojengwa kwa mwaka 2005 ni Namanyere, Katesh, Namtumbo na Orukesmati na tunategemea huko alikokusema na kwingineko juhudi zitafanywa ili huduma za Posta zifikishwe katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumzia.

Na. 287

**Huduma za Simu za *Celtel***

**MHE. HAMISI J. NGULI (K.n.y. MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2004/2005 Kampuni ya Simu za mkononi ya *Celtel* ilitoa vipeperushi vikionyesha maeneo ambayo tayari yamepata

huduma ya simu za mkononi ya *Celtel* na kati ya maeneo/miji iliyoonyeshwa inapata huduma hiyo ni pamoja na mji wa Itigi ambao mpaka wakati wa kutayarisha swali hili, ulikuwa haujapata huduma hiyo pamoja na kufuatilia sana:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizoifanya kampuni hiyo kutoa taarifa ya jambo hilo ambalo kwenye maeneo mengine imeshindwa kulitekeleza?

(b) Je, ni lini basi huo mji mdogo wa Itigi utapatiwa huduma za simu za kampuni ya *Celtel?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail J.R. Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi zote za uchambuzi wa soko na mawimbi ya redio kwa eneo la Itigi imekwishafanywa na Kampuni ya *Celtel.* Aidha, Kampuni imeiweka Itigi kwenye mpango wake wa kuipatia huduma hiyo ya simu. Hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo ya kampuni hiyo, ni kwamba kwa sababu ambazo ziko nje ya uwezo wao inawawia vigumu kutamka tarehe halisi na muda maalum wa kutoa huduma hiyo Itigi hadi hapo utafiti wa kina utakapofanyika.

Mheshimiwa Spika, tunazipongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Iwvatta ya ufuatiliaji wa masuala ya simu katika jimbo lake na tunaamini makampuni husika yatashughulikia matatizo yake ipasavyo. Tunaomba wananchi wa Itigi wavute subira. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kwa mwaka jana walikuwa wameahidi kwamba watafikisha huduma hiyo katika mji mdogo huu wa Itigi na kwa kuwa baada ya kutamka hivyo, yawezekana kabisa makampuni mengine yalisita kufanya hivyo. Je, hiyo siyo kuwanyima wananchi wa Itigi kupata huduma hiyo kwa mapema kutoka kwenye makampuni mengine?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa huduma au kuchelewa kwa huduma za mawasiliano ya *Celtel* hakuinyimi nafasi huduma nyingine kutoa huduma zao pale. Napenda nimwambie Mheshimiwa Nguli mwaka jana tu huduma za *Vodacom* zilifika Itigi na tunategemea muda siyo mrefu huduma za *Celtel* zitafika pale. Tunachokiomba kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wananchi wa Itigi wavute subira huduma za mawasiliano zitafikishwa Itigi.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa kampuni ya *Celtel* ilipeleka minara yake pale Bukene na kwa kosa lisilojulikana ilihamishwa tena na kupelekwa Bugene. Sasa kampuni hii inawaambia nini watu wa Bukene kwa sababu imewavunja moyo?

**SPIKA:** Swali la msingi ilihusu Itigi, lakini kama Mheshimiwa Naibu Waziri una majibu ya Bukene yatoe.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Kahumbi kwamba mnara ambao ulipaswa kwenda Bugene kwa makosa ulipelekwa Bukene na kutokana na hilo waliubadilisha ule mnara na kuupeleka ambako ulipangwa.

Lakini tulishazungumza na Mheshimiwa Kahumbi kwamba tutaendelea kuwasiliana na wenzetu waone umuhimu wa kupeleka simu Bukene kwa sababu kuna wananchi wa kutosha na huduma hizi zinahitajika. Namwomba Mheshimiwa Kahumbi, japo anastaafu atakayekuja wataendelea kumpa huduma zinazohitajika. *(Kicheko)*

Na. 288

**Fedha za *STABEX***

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO (K.n.y. MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kutumia fedha za *STABEX* ya kahawa kuboresha kilimo cha kahawa na kujenga barabara za vijijini katika maeneo yanayolima kahawa:-

Je, Mkoa wa Kagera umefaidika vipi na mpango huo wa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Nilipojibu swali Na. 201 la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, katika kikao cha 21 cha Mkutano wa 20 unaoendelea sasa, nilitoa maelezo kuhusu matumizi ya fedha za *STABEX* ya kahawa. Aidha, maelezo mengine ya matumizi ya fedha hizo yalitolewa na Waziri wa Ujenzi alipojibu swali Na. 45 la Mheshimiwa Dr. Slaa katika Kikao cha tano na swali Na. 192 la Mheshimiwa Mutungirehi katika kikao cha 20 vyote Mkutano huu wa 20. Mkoa wa Kagera utafaidika na fedha za *STABEX* kama ifuatavyo:-

(i) Mkoa umetengewa *Euro* milioni moja kwa ajili ya matengenezo ya barabara zinazohudumia maeneo yanayolima kahawa. Barabara zinazotenezwa na *TANROADS* ni kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Bukoba: Bugorama hadi Kabingo yenye urefu wa kilometa 7.0; Ishoja hadi Rwaya Kibengwe yenye urefu wa kilometa 12.0; Kitobe hadi Kyabajwa yenye urefu wa kilometa 7.00. Wilaya ya Karagwe: Kagenyi hadi Kyerwa yenye urefu wa kilometa

12.95; Kakanja kupitia Kikukuru hadi Kitwe yenye kilometa 13.80; Rugu hadi Ruhita yenye kilometa 7.20; Nyakagoyagoye hadi Rwabwere yenye kilometa 9.50; na Kigarama kupitia Mabira hadi Kyerwa ujenzi wa sehemu korofi zenye urefu wa kilometa 5.1. Wilaya ya Muleba; Ruhanga hadi Nyakahama yenye urefu wa kilometa 19.10; Kanyambogo kupitia Rubya hadi Ibunga yenye urefu wa kilometa 11.9. Barabara zitakazofanyiwa ukarabati katika Mkoa wa Kagera zina urefu wa kiometa 123.55.

(ii) Jumla ya shilingi 32,245,625 zilitengwa kwa ajili ya utafiti. Tayari Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Maruku kimeanza kufanya utafiti wa ugonjwa wa mnyauko fusari wa kahawa aina ya Robusta ili kupata aina bora na zenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huo. Aidha, Kituo hicho kimenunua mashine ya kupukuchukua kahawa aina ya Robusta kwa kutumia njia inayojulikana kama *West Processing* ambayo hutoa kahawa yenye ubora wa juu. Jumla ya shilingi milioni 30 zimetumika katika kununua mashine hiyo.

(iii) Ukarabati wa maabara ya Kituo cha Maruku utaanza hivi karibuni. Maabara hiyo itakiwezesha Kituo kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mimea kwa urahisi na kwa ufanisi mkubwa. Mkoa wa Kagera utaendelea kunufaika na fedha za *STABEX* baada ya kukamilika kwa mwongozo wa kutumia fedha hizo kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Naipongeza Serikali kwa kumpatia Mheshimiwa Dr. Kamala Mbunge wa Nkenge barabara tatu katika jimbo lake kutokana na fedha za *STABEX*. Fedha hizo zimekwishatengwa, lakini mkandarasi atakayehusika na utengenezaji wa barabara hizo hajapatikana. Je, mkandarasi huyo atapatikana lini? Pili, kwa kutumia fedha hizo za *STABEX* wakulima wa kahawa wanategemea kupatiwa aina bora ya miche ya mibuni. Je, miche mingapi ya aina bora ya mibuni imetengewa kwa wakulima wa jimbo la Nkenge?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nazipokea pongezi kwa Serikali kwa matengenezo ya barabara tatu. Nitazifikisha pongezi hizo kwa wanaohusika. Ya pili, amesema mkandarasi hajapatikana, ninachoomba Mheshimiwa Mbunge akubali kuwa taratibu zikishakamilika mkandarasi atapatikana. Vinginevyo naomba tufuate taratibu zile zile kwa kuuliza kupitia Halmashauri ya Mkoa kwa sababu masuala haya yamefanywa na *TANROADS* wa Kagera. Suala hili likizungumzwa huko ufumbuzi utapatikana. Kwa sasa nashindwa kutamka rasmi tarehe gani mkandarasi atapatikana. Lakini jawabu liko huko huko Mkoani ambako mipango hii ya barabara ilifanywa.

Pili, fedha za *STABEX* aina za miche. Miche ipo, lakini mgao haujafanyika bado. Lakini nitalifikisha suala hili kwa wanaohusika na tegemeo langu jawabu la ufumbuzi litapatikana. Kwa sasa hivi mara moja si rahisi kujua kwa sababu swali halikueleza miche itakwenda wapi na wapi.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali moja tu la nyongeza kwamba ukilinganisha hela zilizotolewa au ambazo zimetengwa *Euro* milioni moja

ukilinganisha na kiasi kizima kilichotolewa cha zaidi *Euro* milioni 40 kwamba ni kiasi kidogo kwa Mkoa kama Kagera ambao unatoa kahawa karibu kuliko sehemu nyingi za Tanzania. Je, Naibu Waziri atataka kuwahakikishia wananchi wa Bukoba kwamba kwenye mwongozo utakaotolewa utahusisha pia vijiji kama Kaololo, Bwembe, Chitendagulo, Nishambya na Kijiji changu cha Kibeta ambao ni wakulima wa kahawa na ambao katika mpango mzima hawajatengewa hata senti tano na hii si kuwadhulumu?

Mheshimiwa Spika, kweli kiasi cha fedha kilikuwa hizo milioni alizozitaja, lakini ni kiasi kidogo sana zilitengwa kwa ajili ya mkoa wa Kagera, hii ni imetokana na kuwa shughuli hizi waliotakiwa kuzipanga ni mikoa husika inayolima kahawa. Walivyopanga na kuleta pale mkoani na kuwasilisha kunakohusika ndio jawabu likawa hili kwa hivyo hata hivi hivi halivyoitaja pamoja na kijiji chake sisi hatukuvisahau waliosahau au waliotaka waiingize huko ni wahusika mkoani Kagera yaani Bukoba. Kwa hivyo namwomba radhi kuwa suala hili siwezi kulijibia hapa kwa sababu maamuzi yalifanyika mkoani huko mjini Bukoba, mkoa wa Kagera.

Lakini nakuahidi kuwa wanaolima kahawa sio Kagera peke yake kwa hivyo masula yote *it means* kujumuisha barabara zote na ziko hapa orodha ninayo, akizitaka baadaye naweza kumpa kuonyesha jinsi fedha zilivyotengwa, hazikupangwa na Wizara ya Kilimo au makao makuu ya Wizara ya Ujenzi, taratibu zote hizi zilitoka mikoani.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi kuuliza swali moja kubwa la nyongeza. Wilaya sita za mkoa wa Kagera zote zinalima kahawa, wilaya ya Ngara kwa kuwa na kahawa nzuri ambayo haimwagiliwi madawa sasa imepata hata bahati ya kujenga kiwanda cha kukoboa kahawa. Lakini katika orodha anayoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, wilaya ya Ngara haikutajwa, naomba niambie Serikali inaiambia nini wilaya ya Ngara na wakazi wake kwa kutokupata bahati kama hiyo ili kuendeleza zao la Kahawa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze wakulima wa Ngara kwa kilimo cha *organic coffee* naomba unifikishie pongezi zangu kwao.

Lakini pili wao kutokuhusishwa katika utaratibu huu ni kama nilivyojibu hapo awali mipango yote walioagizwa wilaya husika wapange na waiwasilishe mkoani sasa mkoani kama walipeleka na mkoani hawakuona ipo sababu basi hiyo ndio jawabu, lakini ukweli kuwa mipango yote imetoka mkoani huko huko. Kwa hiyo suala hili ningemwomba Mheshimiwa kama akiweza alirudishe kwenye *RCC* aulize ilikuwakuwaje Ngara ikasahauliwa hivyo? Nawapongeza hata hivyo kwa kilimo cha *organic coffee*.

Na. 289

**Fedha kwa Ajili ya Mradi wa *Health and Nutrition Project***

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO (K.n.y. MHE. DR. WILBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2001 ilionyesha kuwa kuna dola za Kimarekani 86,085 sawa na Shs.51,651,000/= wakati huo kwa ajili ya mradi huo ziliingizwa katika akaunti ya benki moja katika visiwa vya *Caribbean*:-

(a) Kwa kuwa fedha hizo zilitolewa na wafadhili kwa ajili ya mradi wa Afya na Lishe yaani *Health and Nutrition Project,* Je, mfadhili aliyetoa fedha hizo ni nani na anatoka katika nchi gani na zimeingizwa katika benki gani na ni katika akaunti gani?

(b) Kwa kuwa taarifa hiyo ya mwaka 2001 ilionyesha kuwa fedha hizo zimepotea na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huyo ya mwaka wa fedha iliyoishia tarehe 30 Juni, 2003 inaonyesha kuwa bado fedha hizo zimepotea. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya taarifa hizo?

(c) Kwa kuwa taarifa ya upotevu imetolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.. Je, Serikali imechukua hatua gani kufuatilia upotevu huo na waliohusika na upotevu huo wamechukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Health and Nutrition Project* ulikuwa sehemu ya mradi mkubwa zaidi uliokuwa unatekelezwa na Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu na Jiji la Dar es Salaam kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huo ulianza mwaka 1990 na kumalizika mwaka 1999. Kila sehemu ilikuwa na akaunti yake na fedha zilikuwa zinapelekwa moja kwa moja kwa idara husika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upotevu wa fedha katika mradi huo liligundulika na kuripotiwa katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulitokea upotevu wa fedha ulio gunduliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Watu wawili yaani Pascal Mwaja na Julius Kyaruzi wamefikishwa kwenye mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam kwa shauri la jinai namba 1360 la mwaka 1996 kwa tuhuma nne za kushirikiana kwa nyakati tofauti kuiba dola za Kimarekani 86,085.50 za mradi wa Afya na Lishe hizo kuwa Benki Kuu ya Tanzania, kwa njia ya udanganyifu na kughushi nyaraka. Shauri hili bado linaendelea kuko mahakamani.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini jambo ni la siku nyingi sana na hizi pesa ni za *World Bank* inasikitisha mpaka sasa ati hao watu bado hawajaweza kuhukumiwa na pesa

zenyewe kurudishwa kwa wenyewe. Je, shauri la namna hii yanaweza kuwa yametokea mengine ni mangapi kama waziri anaweza kutuambia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, baada ya tatizo hili kugundulika ufuatiliaji ulifanyika na kubaini waliohusika na hao niliowataja wawili ndio wamefikishwa mahakamani, na shauri kwa sababu liko mahakamani nisingependa kulizungumzia zaidi lakini kesi itasikilizwa tarehe 30 Agosti, 2005.

Mheshimiwa Spika, mashauri mengine ya namna hii ya ubadhilifu yapo na kulingana na taarifa ya mkaguzi na mdhibiti wa Serikali kwenye taarifa yake zipo, lakini kila linalotolewa linafuatiliwa na wahusika wanashughuliwa na Sheria na kanuni zinafuatwa kuwashughulikia aidha kuwapeleka mahakamani ama kuwasimamisha kazi ama vyote viwili.

Na. 290

**Mipango ya MMES/MMEM Kusaidia Shule Binafsi**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y MHE. RAPHAEL N. MLOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha mipango mahususi ya MEM/MMES kwa lengo la kuboresha Elimu Nchini; lengo la mipango hiyo ni kwa faida ya watoto wote nchini lakini inalenga zaidi kwa shule za Serikali na za wananchi.

Je, Serikali ina msimamo gani juu ya ombi kwamba, shule binafsi na watoto wanaosoma katika shule hizo nao wafaidike na mipango hiyo kama wanavyofaidi wale walioko katika shule za Serikali za wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Na. 172 la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, katika kikao hiki, kuwa Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi katika kutoa elimu nchini. Aidha, malengo ya MEM 2002-2006 ni kuongeza wanafunzi wa rika la elimu ya msingi yaani wenye miaka 7-13 kufikia 100% ifikapo 2006 na mpango MMES 2004-2009 unalengo la kuongeza waliojiunga na sekondari kufikia 50% ya wahitimu wa darasa la VII, na vilevile 50% ya wahitimu wa kidato cha nne kujiunga kidato cha tano kila mwaka ifikapo 2010. Ili kufikia malengo hayo, hatua mojawapo ya Serikali ni kusaidia sekta binafsi inayotoa elimu ili iboreshe shule zake kwa sababu sekta hiyo inasaidia Serikali katika

kutoa elimu nchini. Kwa kuzingatia kuwa kupanga ni kuchagua Wizara yangu imepanga kutekeleza kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa ruzuku ya Maendeleo kwa mwenye shule asiye Serikali aliyeidhinishwa na Afisa Elimu kiongozi kwa ajili ya ujenzi wa shule za wanafunzi wenye ulemavu kwa viwango sawa na ile inayotolewa kwa ajili ya sekondari za Serikali zinazojengwa na wananchi. Viwango hivyo ni shilingi milioni 7.0 kwa darasa na shilingi milioni 9.0 kwa nyumba ya mwalimu.

(ii) Kutoa ruzuku ya uendeshaji wa shule yaani *capitation grant* kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia ya shilingi 10,000/= kwa mwanafunzi kwa sekondari zisizo za Serikali ambazo haziendeshwi kibiashara na siyo seminari. Inatarajiwa utoaji wa ruzuku hiyo utaanza katika Bajeti ya mwaka huu wa 2005/2006.

Aidha Serikali inaendelea kusaidia shule binafsi katika; kuandaa walimu, mitaala ya kufundishia, ukaguzi wa shule, usajili wa shule na huduma ya mitihani ya kitaifa.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniapa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa mpango huu wa MEM na MMES unaisaidia sana shule za Serikali na shule za watu binafsi ambazo wananchi wengi ambao wana uwezo mdogo na wenyewe inabidi wapeleke watoto wao. Kwa nini Serikali isitoe ruzuku kwa ajili ya watoto hao wakapunguziwa ada na wenyewe katika maeneo yale?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali inatambua umuhimu wa shule za sekondari za binafsi, kwa sababu shule hizi zinasomesha watoto hawa hawa Watanzania na ndio maana katika jibu la msingi nimesema kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha Serikali itatoa ruzuku kwa shule binafsi ambazo si za kibiashara na ambazo si za *Seminary* na ruzuku hiyo nimesema ni shilingi 10,00 kwa kila kichwa cha mwanafunzi. Kwa hiyo, kwa ruzuku hiyo ni matumaini yetu kwamba wale wenye shule za binafsi watatazama vilevile taafifu hii vilevile imfikie mzazi kwa maana ya kupunguza ada, kwa sababu sehemu ya gharama ni shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi Serikali itawapatia kama ruzuku.

**MHE. MONICA W. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya maswali yote mawili aliyotoa sasa hivi Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza kama kwa kuongezea swali la pili, pamoja na kwamba Serikali inatoa ruzuku, ruzuku hii ni kwa ajili ya majengo na pamoja na kwamba wanatoa shilingi 10,000 kwa kila mtoto. Lakini 10,000 hii kwa shule binafsi ni ndogo sana na huko katika shule binafsi kumekuwa na watoto ambao ni yatima, labda amefika kidato cha pili au cha tatu mzazi amefariki lakini yuko katika shule za binafsi;

Je, Serikali itakubali kwamba hao ambao wanakumbwa na uyatima katikati wakati anasoma, Serikali ichukue jukumu la kumalizia kumlipia ada mwanafunzi huo ili aweze kumaliza shule?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema ruzuku shilingi 10,000 ni kidogo, lakini tukumbuke kwa miaka mingi ilikuwa ni sifuri.

Mlheshimiwa Spika, hizi shule za binafsi zilikuwa hazipati hata senti tano kama ruzuku kutoka Serikalini. Kwa hiyo, kwa mwaka huu kuanza kuwapa shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa sababu kweli ni hatua, ni hatua kubwa tu na jinsi ambavyo uchumi wetu utazidi kuongezeka na mapato ya Serikali yatazidi kuongezeka nina hakika hii shilingi 10,000/= ambayo tumeanza nayo, nayo itakuwa inaongezeka.

Kuhusu watoto yatima, sasa hivi Serikali inawasaidia watoto wa aina hii kwenye shule za Serikali kama unavyojua Halmashauri zinasaidia watoto maskini na watoto yatima kuwasomesha na Serikali kuu vilevile nayo kuanzia mwaka juzi na mwaka jana ameongezeka ule mfuko kwenye Waheshimiwa Wabunge, uko utaratibu kwa watoto yatima kwenye shule za sekondari za Serikali. Sasa kuhusu wale ambao katika shule za binafsi hilo nalo tutalitazama, tuombe tu kwamba hali ya uchumi iendelee kuwa nzuri zaidi ili Serikali ipate uwezo wa kuhudumia Watanzania kwa ubora zaidi.

Na. 291

**Kufukuzwa kwa Wanafunzi wa Kike Mashuleni**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa sensa ya watu wa mwaka 2001 imeonyesha kwamba idadi ya wanawake ni kubwa kulinganisha na wanaume; na kwa kuwa idadi ndogo ya wasichana imekuwa ikipata nafasi kwenda sekondari na idadi ndogo zaidi inafanikiwa kuhitimu elimu ya sekondari nchini kutokana na kufukuzwa kwa kupata mimba mashuleni; na kwa kuwa mtoto wa kike naye ana haki sawa na wa kiume katika kupata elimu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba Sheria ya kumfukuza mtoto wa kike moja kwa moja kutokana na kosa la watu wawili ni kuwadididimiza wanawake wote?

(b) Je, Serikali haioni kwamba inamwadhibu mtoto au watoto watakaozaliwa ambao hawakushiriki katika kutenda kosa?

(c)Je, Serikali inakubaliana nami kwamba kumsababisha mwanamke mmoja kukosa elimu ni kuliangamiza Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, mbunge wa Muleba Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 iliyotungwa na Bunge hili, kifungu cha 60(o) imempa uwezo Waziri mwenye dhamana ya elimu kutunga kanuni inayoainisha makosa yanayopelekea mwanafunzi kufukuzwa shule. Kwa kuzingatia Sheria hiyo Waziri ametunga kanuni iitwayo The *Education Expulsion and Exclusion of Pupils from Schools Regulations* 2002 inayotamka kuwa mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule ikiwa:-

(i) Mwanafunzi ataendelea na tabia za utovu wa nidhamu ambao unahatarisha na kuharibika kwa tabia za wanafunzi na kuharibu jina zuri la shule;

(ii) Mwanafunzi atajihusisha katika makosa ya jinai kama vile wizi, kuharibu mali ya umma, umalaya, madawa ya kulevya na kwenda kinyumbe cha maadili mema; na

(iii) Mwanafunzi atajiingiza katika ndoa. mwanafunzi wa kike anayepata mimba na mwanafunzi wa kiume anayempa mimba ni ishara ya kutosha ya kwenda kinyume na maadili mema kwa hiyo wote mvulana na msichana wanafukuzwa shule. Kwa kuwa Sheria hii inawaadhibu wote msichana anayepata mimba na mvulana aliyempa mimba mwanafunzi mwenzake au yeyote mwingine haiwezi kuwa inawadidimiza wanawake tu.

Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kifungu (35) (4) Waziri ametunga kanuni iitawayo *The Education Imposition of Penalties to Persons Who Marry or Impregnate a School Girl Rules* 2003 kanuni hii inatoa inayotoa adhabu ya kifungo cha miaka 3 na faini kati ya sh.300,000/= na 500,000/= kwa mwanaume yeyote anayempa mimba mtoto wa shule.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mfumo na taratibu zilizopo mwanaume anayempa mimba mwanamke yeyote anawajibika kumtunza mama na mtoto anayezaliwa. Endapo utaratibu huo ukifuatwa, mtoto anayezaliwa hatakuwa anaadhibiwa, isipokuwa kisheria anatakiwa kulelewa vizuri sawa na mtoto mwingine yeyote. Sheria na kanuni zilizowekwa shuleni ni kulinda maadili mema ya jamii yanayoendana na utamaduni wetu.

(c) Mheshimiwa Spika, wote tunafanya kazi kwa nguvu na hekima yote ili tusiliangamize taifa. Tunapochukua hatua stahili kwa hao wachache wanaokosea utaratibu kwa bahati mbaya au kwa makusudi, tunajitahidi kudumisha maadili mema.

Aidha, kila mahali ikiwa ni pamoja na shuleni kuna utaratibu maalum uliowekwa kwa kila mhusika kuufuata. Kwa hiyo tukiendekeza uhuru wa kupita kiasi na hata kuvuka

sheria na taratibu zilizowekwa kulinda maadili mema kwa mujibu wa utamaduni wetu, huko ndiko kutakuwa kuliangamiza Taifa.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema watoto watalelewa vizuri ikiwa anajua kwamba baba na mama pengine wote walikuwa ni wanafunzi wamefukuzwa na kwa hiyo wamekosa elimu kuweza kuwapa ajira bahati mbaya hapo.

Mheshimiwa Spika, je, hao watoto watalelewa vizuri kwa misingi ipi?

La pili, sasa hivi watoto wanaokwenda shule ni watoto wachanga sana, miaka mitano mpaka sita, na kwa hiyo wakati wakiwa wanapovunja ungo wanakuwa hawajui hali yao inafananaje, na kwa hiyo wanatumbukia katika matatizo mazito ya kuweza kuingia katika vitendo ambavyo hawavijui;

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na umri wa mtoto kutambua maisha yake na kuweza kukwepa kudanganywa na mtu anayemzidi uwezo kutambua matatizo yaliyoko mbele yake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, iwapo wanafunzi wamepeana mimba jibu la msingi linasema wote wawili wanafukuzwa shule kwa sababu wamekwenda kinyume cha maadili mema ya jamii, sasa Mheshimiwa Mbunge anasema je tukiwafukuza shule huyo mtoto atakayezaliwa atalelewa vipi?

Mheshimiwa Spika, huyo mtoto atakayezaliwa baba na mama walikuwa wanafunzi, lakini katika jamii zetu za kiafrika kuna bibi, kuna babu, kuna baba mdogo kwa hiyo hawa watoto wawili waliopeana mimba watapata mtoto, basi wanawajomba babu, bibi, hao watawalea.

La pili Mheshimiwa anasema sasa hivi watoto wanaanza shule bado wadogo, miaka mitano miaka sita, wanavunja ungo wakiwa wadogo bado hawajui kinachoendelea.

Hili kwa kweli ni jukumu tu la wazazi na wazazi wengi wanajua hili kwamba akiona mtoto wake anaanza kubadilika badilika hivi basi wakinamama wana utaratibu wao kuanza kuwaeleza kwamba ukiona hili usishtuke. Ukiona hili ushtuke, kwa hiyo jamii inayomfumo wa kuwaeleza hawa mabinti jinsi ya kufanya wakishafika katika umri kama huo.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *statistic* zinaonyesha wasichana wanaopata mimba mashuleni ndio wanaofukuzwa na haijaonyesha ni namba ngapi ya wavulana au wazee wanaotia mimba wasichana. Mara nyingi huwa wanakataa wavulana na wakina baba wanaotia mimba. Je, kuna utaratibu gani wa Serikali au mahakama kuweka utaratibu wa kila atakayetamkwa ametia mimba uende kufanya *DNA test* au *biological test* ili na yeye awajibike?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba mtu yoyote anayempa mimba msichana, kama ni mwanafunzi mwezake mvulana, ukweli ni kwamba akibainika anafukuzwa shule kama ni mtu mzima huko mitaani akibainika Sheria ipo na nimeitaja katika jibu la msingi kushughulika na mtu anayempa mimba mwanafunzi.

Sasa Mheshimiwa anasema lakini takwimu japo hakuzitoa sawasawa anasema takwimu zinaonyesha kwamba wanaume walio wengi hawaadhibiwi. Ukweli ni kwamba tatizo tunalolipata ni ushahidi, kwa sababu kwanza wakati mwingine wazazi wanapenda kumalizana huko huko na yule mtu aliyempa binti yake mimba.

Halafu la pili, wavulana wanakataa lakini sasa hivi nataka kuwaambia Watanzania kwa teknolojia tuliyonayo sasa hivi hii mitambo ya *DNA* sasa tayari ipo nchini, yoyote yule ambaye anakataa atapelekwa katika mtambo huu na itawagundua tu. Kwa hiyo, nasema Watanzania wajue huu mtambo upo anayekataa watuletee tutampima na huu mtambo.

Na. 292

**Wananchi Walioathirika na Milipuko ya Upasuaji Miamba Bukoba Vijijini**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE (K.n.y. MHE. ALI SAIDI SALIM)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi ya upasuaji miamba imesababisha milipuko mikubwa katika maeneo kadhaa ya Bukoba Vijijini kikiwemo kitongoji cha Bulila, Kijiji cha Kanazi Kata ya Katerero, na kwa kuwa milipuko hiyo imesababisha kuathirika kwa namna tofauti kwa wanakijiji wapatao 20, na kwa kuwa wahusika wa *TANROADS* walifika kwenye maeneo kuona uharibifu uliofanyika na kufanya tathmini ya hasara yote hapo tarehe 13/12/2002 lakini hadi leo Serikali haijasema chochote kuhusu maafa hayo kwa wananchi husika.

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa wananchi wa maeneo hayo waliathirika kutokana na milipuko hiyo?

(b) Kama hivyo ndivyo. Je, kwa nini Serikali imekuwa kimya kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili baada ya tukio?

(c) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutoa fidia kwa wananchi hao masikini walioathirika?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Saidi Salum, Mbunge wa Ziwani, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kwa ifuatavyo:-

Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara kuu ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe iliyokuwa ya changarawe kwa kiwango cha lami. Sehemu ya fedha hizo zilitoka kwa wafadhili wakishirikiana na Serikali ya Tanzania.

Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami ni sehemu ya mtandao wa Barabara Kuu za Mkoa wa Kagera. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Kagera na Nchi jirani ya Uganda. Aidha, barabara hii ipo katika ukanda wa nne (4) wa mtandao wa barabara za Afrika Mashariki unaounganisha Uganda na Tanzania na Nchi za Kusini mwa Afrika. Barabara hii ina urefu wa kilomita 112.

Ni kweli kuwa sehemu nyingi za Bukoba ziliathirika na milipuko ya upasuaji wa miamba wakati wa ujenzi wa barabara hii. Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Kagera imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana suala hili na iliishatembelea sehemu husika ikiambatana na Mkandarasi pamoja na Mhandisi Msimamizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Saidi Salum, Mbunge wa Ziwani , lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilifahamu kuwa wananchi wa maeneo hayo waliathirika kutokana na milipuko hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilimwagiza Mkandarasi alipe fidia hizo kupitia kwa Mhandisi Msimamizi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi alikuwa tayari kulipa fidia hizo baada ya kupokea tathmini halisi ya uharibifu huo kutoka kwa Mthamini wa Serikali. Mthamini wa Serikali alianza kazi hiyo mwanzoni mwa mwaka 2003 na bahati mbaya kabla hajakamilisha ripoti yake mthamini, alifariki mwishoni mwa mwaka huo huo wa 2003. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, baada ya kifo cha Mtathimini huyo wa kwanza, Serikali haikukaa kimya, bali iliendelea kutafuta Mtathimini mwingine ili kuendeleza kazi ya utathimini. Mtathimini wa Serikali ameshapatikana na ameshaanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa vijiji vilivyoathirika kutokana na milipuko hiyo ambavyo vimeshafanyiwa tathimini ni Bugorora, Katoma, Kyakailabwa, Rwamishenye, Kibeta, Ibaraizibu, Bwizanduru, Kanazi (ikiwemo Bulila), Kangantebe, na Muhutwe. Mwezi Aprili 2005 Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Kagera imewalipa waathirika wote kwenye vijiji vyote vilivyofanyiwa tathmini na Mthamini wa Serikali.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba ni mtaalamu wa mifupa, lakini ningeomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo;

Kwamba ukiachilia mbali hivyo vijiji vilivyotajwa katika swali la msingi vya Kata ya Katelelo, sasa kuna vijiji vingine ambavyo amevitaja viko Bukoba Mjini vya maeneo ya Kaikairabwa, maeneo ya Kagondo na Rwamishemi na baadhi ametaja kwamba wameshalipwa.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo sawa ni kwamba baadhi wamelipwa na wengi hawajalipwa na kwa bahati mbaya wamekuwa wanapigwa chenga wanaambiwa waende kwa mkandarasi, mkandarasi ameshamaliza kazi yake, waende ujenzi wanapigwa danadana na watendaji wa Serikali.

Je, Waziri anawaagiza nini watendaji wa Serikali na hasa walioko katika ofisi ya *TANROAD* ili wawape majibu sahihi watu hao wanaofuatilia malipo ambayo kimsingi mimi kama Mbunge wao naamini wako wengi ambao hawajalipwa tofauti na alivyozungumza Mheshimiwa Waziri ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli niko hapa sio kama mtaalamu wa mifupa, niko hapa kama Waziri. Kama nilivyoeleza kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi kwamba tathimini ilifanywa na vijiji vyote vilivyohusika vimelipwa fidia halali.

Sasa suala la kulipa vijiji vingine ambavyo havikufanyiwa tathimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Lwakatare kwamba vijiji hivyo havipo, havikuathirika na

kama anaona kwamba kuna matatizo basi tutafanya harambee ya kuwachangia kwa sababu ni kuwasaidia ndugu zetu na wajukuu wetu. *(Makofi)*

Na. 293

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa Barabara – Ruvuma**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafanya kazi inayostihili pongezi kwa kuweka mtandao mzuri wa barabara katika Mkoa wa Ruvuma na Wilaya zake, na miradi ya *RUSIRM, African Development Bank* pamoja na *Road Fund* imefanya kazi kubwa kwa upande wa Wilaya ya Songea lakini zipo kazi ambazo zimebaki kiporo hazijakamilika, zikiwemo barabara ya Songea Mitomoni – Kuvukia Msumbiji ambayo ilichongwa kutoka Songea – Kijiji cha Mhukuru barabarani, barabara ya Wino – Ifunga, barabara ya Peramiho – Litumba Ndyosi ambayo ina utata kwa sababu inapita eneo la *mission* ya Peramiho na ilikuwa ikitunzwa na *mission* lakini Serikali ilipochukua jukumu la kufanya matengenezo imeacha vipande muhimu kwa *mission* hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuichonga barabara ya Songea – Mitomoni hadi mpakani mwa Msumbiji?

(b) Je, Serikali iko tayari kuipa barabara ya Wino – Ifinga msukumo unaostahili kwa kuiwekea mradi kabambe utakaosimamiwa na Ujenzi toka Dar es Salaam?

(c) Je, Serikali iko tayari kuifanyia *realignment* barabara ya Peramiho Litumba Ndyosi ili iwe Likuyu – Fusi – Peramiho na ile iliyotawa katika sehemu (a) na (b) iwe Kalagano – Litumba Ndyosi – Kingole Wilaya ya Mbinga.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwsa Prof. Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Songea hadi Mitomoni yenye urefu wa Km. 133 ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala la Barabara Mkoa wa Ruvuma.

Hali ya barabara hii ni ya kuridhisha kutoka Songea hadi kijiji cha Mhukuru barabarani Km. 70, na kutoka kijiji cha Mhukuru barabarani hadi Mtongani (Km. 63) ipo katika hali mbaya hasa ile ya mwisho kiasi cha Km. 8 iendayo sehemu iliyopendekezwa kujenga mojawapo ya madaraja ya kuunganisha Tanzania na Msumbiji. Serikali kupitia Wizara yangu imeendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida barabara hiyo. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2003/2003 jumla ya shilingi milioni 46.7 zilitumika kwa kuchonga barabara, kuweka kifusi sehemu korofi na kufukua mifereji ya maji.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005 kazi zifuatazo zinaendelea kufanyika, ujenzi wa daraja la Bomba Mbili kwa gharama ya shilingi milioni 28, matengenezo ya sehemu korofi eneo la Lupapila kwa gharama ya shilingi milioni 17.48 na kurudishia mbao kwenye madaraja ya chuma na magogo kwa gharama ya shilingi milioni 6.7. Aidha Wizara katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 imepanga kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii kutoka kijiji cha Mhukuru hadi Mitomoni kwa kutumia Mfuko wa Maendaleo wa Mradi wa *RUSIRM.*

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Wino hadi Ifinga yenye urefu wa Km 46.9 ni barabara ya Wilaya inayosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Barabara hii ilifunguliwa kwa kukata milima na kuweka baadhi ya Makalvati. Barabara hii inahitajika kujengwa upya kwa kiwango cha changarawe. Ingawa barabara hii ni ya Halmashauri ya Wilaya, lakini kutokana na umuhimu wake Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2004/2005 ilitenga fedha shilingi milioni 70 kusaidia ujenzi wa barabara hii ambapo kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na kukata kilima eneo la Kipata, kusafisha barabara (*site clearance*) Km 11, kujenga kwa kiwango cha changarawe Km 3 na kujenga mifereji ya maji. Aidha Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kadri itakavyokuwa inawezekana ili kusaidia, matengenezo ya barabara hii.

(c) Mheshimiwa Spika, barabara ya Likuyufusi – Peramiho – Litumba Ndyosi hadi Paradiso ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi. Aidha napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa uongozi *mission* ya Peramiho kwa kusaidia kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara sehemu ya Km. 8 ya barabara hiyo kati ya Likuyufusi na Hospitali ya Peramiho. Barabara ya kutoka Litumba Ndyosi hadi Kingole nayo pia ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Hivyo hakuna ulazima wa kuifanyia mchepusho (*re-alignment*) barabara hizo kama inavyopendekezwa.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kuzikumbuka hizo barabara ambazo zilikuwa za *Mission* na sasa imechukua Serikali. Labda kubwa na nzito ni ile ya kuwa-*time* ile ya kufanya hiyo kazi kama kweli utafanya barabara ya udongo kila mwaka tutaishia nusu ya barabara. Lakini kama ile ya Wino mpaka Ifinga inahitajiwa nguvu kubwa sijui kama Serikali itaweza kuchukua hiyo barabara kwa mara moja badala ya kusema awamu kwa awamu kwa kuwa awamu zile zitarudiwa mara mbili, mara tatu, mara nne bado barabara haijaisha. Kwanza nitoe hizo shukrani na pili hiyo ya kuchukua barabara ya Wino mpaka Ifinga kwa mkupuo.

**SPIKA:** Naona hayo ni mapendekezo tu siyo swali, lakini Waziri kama unaweza kumsaidia Mheshimiwa Mbunge fanya hivyo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, ambaye amefanya kazi nzuri sana kuanzia mwaka 1995, kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Songea hususani Peramiho kwa muda mrefu wamejitolea na wamebeba

mzigo mkubwa katika ukombozi wa Bara la Afrika hususani Msumbiji, sasa lazima wahudumiwe katika miundombinu, Prof. Simon Mbilinyi amefanya kazi kubwa. Lakini nataka nimhakikishie kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu huo na mchango wake, fedha zilizotengwa kwa barabara ya Songea Mitomoni kwa mwaka huu ni shilingi milioni 80 na barabara hii sasa itapitika bila matatizo kwa sababu barabara hii ni ya kihistoria. Hii ndio barabara viongozi wa *FRELIMO* wakati wa haraka za ukombozi waliitumia na tunataka kuiweka barabara ya historia. Barabara ya Paradiso, Kingole, Peramiho, Litumba Ndosyi *tender* imeshafunguliwa, itaenda itafunguliwa tarehe 26 mwezi huu wa saba na jumla ya shilingi 290 zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo. Hivyo basi Serikali itajitahidi na *inshallah* Mwenyezi Mungu akitujalia barabara alizopendekeza hizo zitawekwa lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha hakuna vikao vya Kamati vilivyopangwa leo na hakuna tangazo lingine lolote. Kwa hiyo, tunaendelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/20006

### Wizara ya Fedha

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi iliyowasilishwa hapa Bungeni leo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likae kama Kamati ili likubali kujadili na kupitisha Makadirio na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa kwa kupoteza Wabunge wenzetu walioaga dunia ambao ni Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mheshimiwa Thadeos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashiriki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Hayati Mheshimiwa Abubakar Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Hayati Mheshimiwa Margereth Bwana aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, CCM, Rukwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa jinsi mlivyoendesha kwa ufanisi mijadala ya bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006, tangu ilipoanza tarehe 8 Juni, 2005. Napenda pia kuchukua fursa hii kuzishukuru Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa uchambuzi wao wa kina wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara na Mikoa kwa mwaka 2005/2006. Shukrani za pekee nazitoa kwa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa kwa ushauri na mapendekezo waliyoyatoa kwa

Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali inathamini sana michango yao na tutayafanyia kazi ipasavyo maagizo na mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ni kiungo muhimu katika kubuni na kutekeleza sera ya mikakati ya mapato na matumizi ya Serikali; inayowajibika katika kusimamia, kudhibiti na kutoa hesabu za mapato na matumizi ya Serikali; kusimamia na kuhakikisha mali za Serikali na kudhibiti Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu hayo, ninaomba sasa kutoa taarifa ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2004/2005, pamoja na malengo ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya Sekta ya Fedha, pamoja na mafanikio niliyoyaeleza katika hotuba ya bajeti, mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu ni:

(i) Kuanzishwa kwa utaratibu wa *"Cash Budget"* na mtandao wa kompyuta wa kutayarisha bajeti na kufanya malipo yote ya Serikali *(IMFS)* ambavyo vimeimarisha udhibiti wa matumizi ya umma;

(ii) Kuanzisha Mpango wa Bajeti ya Muda wa Kati *(MTEF)* na mashauriano na wadau kuhusu matumizi ya umma *(PER)* pamoja na hatua za kodi ambavyo vimeongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya umma;

(iii) Kutayarisha na kutekeleza mkakati wa kusimamia misaada toka nje *(TAS)* na mkakati wa kudhibiti madeni *(NDS)* kumeboresha mahusiano na Wahisani na kudhibiti ukuajia wa deni la taifa;

(iv) Kufanya mageuzi katika mfumo wa kodi na usimamizi wa kukusanya mapato, hatua ambazo zimeongeza ukusanyaji wa mapato;

(v) Kutangaza kwenye vyombo vya habari fedha zinazotolewa kwenye Wizara, Mikoa na Halmashauri pamoja na taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ambayo inaimarisha uwazi na uwajibikaji; na

(vi) Kuanzisha mpangilio wa kasma za matumizi unaozingatia mfumo wa kimataifa *(GGS)* ambao umeboresha uchambuzi wa matumizi ya umma.

Mheshimiwa Spika, mageuzi haya yamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio tuliyopata katika ukusanyaji mapato, udhibiti wa matumizi na ukuaji wa deni la Taifa, utoaji takwimu sahihi za misaada na mikopo, kurejesha uhusiano mzuri na wahisani, kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya umma pamoja na kuibua ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Bajeti ya Serikali, Mapato ya Ndani, kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2005/2006, Wizara yangu imeendela kusimamia kwa makini ukusanyaji wa mapato na kupata mafanikio makubwa. Takwimu za awali zinaonyesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2005, makusanyo ya mapato ya ndani yamefikia shilingi 1,772.0 bilioni ambayo yamezidi malengo ya mwaka 2004/2005 kwa asilimia moja (1%). Kati ya kiasi hicho shilingi 1,625.2 bilioni ni mapato ya kodi na shilingi 146.8 bilioni ni mapato yasio ya kodi. Napenda kuwapongeza *TRA* kwa kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuongeza bidii katika kubuni na kutekeleza hatua zaidi za kuongeza mapato ya ndani. Baadhi ya hatua zitakazochukuliwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ni:

(i) Kuongeza idadi ya walipa kodo wakubwa *(Large Taxpayers),* ambapo kufikia Juni 2005 idadi yao imeongezeka kutoka 114 mwaka 2001 hadi 208;

(ii) Kuimarisha utaratibu wa kukusanya mapato yote kwenye kituo kimoja *(One Stop Centre).* Mpaka kufikia Juni 2005, jumla ya Wilaya 66 na Ofisi zote 23 mikoani zilikuwa na *'One Stop Centre'.* Aidha, katika Makao Makuu Idara ya Kodi ya Mapato ya Ndani imeanzishwa kwa kuunganisha Idara ya Kodi ya Mapato na ile ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT).* Kwa hiyo, kuanzia Julai, 2005 huduma ya *One Stop Centre* inapatikana kwenye ofisi zote za Mamlaka ya Mapato;

(iii) Kurekebisha usimamizi wa kodi ya forodha kwa lengo la kupunguza muda wa kupitisha bidhaa;

(iv) Kuendelea kutumia *fuel flow metres* katika bandari ya Dar es Salaam ili kudhibiti uingizaji wa mafuta pamoja na kuziba mianya ya ukwepaji kodi kwenye bidhaa za mafuta; na

(v) Kutoa elimu kwa walipa kodi ili kuongeza ridhaa ya kulipa kodi na kupunguza ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, misaada ya mikopo ya nje, Wizara yangu inayo majukumu ya kutafuta na kuratibu misaada na mikopo nafuu kutoka nchi marafiki na mashirika ya fedha ya kimataifa kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali. Hii ni pamoja na kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati inayolenga kuhakikisha kuwa Serikali inamiliki na kuongoza ajenda nzima ya usimamizi wa misaada na mikopo na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Misaada Tanzania kwa kuweka kipaumbele kwenye maeneo ya kuongeza uhakika wa upatikanaji misaada *(aid predictability),* kuweka takwimu sahihi za misaada na kuongoza kiwango cha misaada inayotolewa kupitia mfuko mkuu wa Serikali *(Exchequer Accounts).* Pia, Wizara ikishirikiana na wadau imekuwa ikiandaa Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada *(Joint Assistance Strategy – JAS)* unaolenga katika kuimarisha zaidi uwezo wa Serikali wa kusimamia mapato na matumizi ya rasilimali za nje kulingana na maeneo ya

kipaumbele kama yalivyoainishwa katika sera na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, takwimu za awali zinaonyesha kuwa tumepokea misaada na mikopo nafuu kutoka nje yenye jumla ya shilingi 1,321.4 bilioni kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya Serikali. Kiasi hicho ni asilimia 95 ya makisio ya shilingi 1,367.0 bilioni. Wizara yangu pia iliweza kulipa kwa wakati michango ya Serikali yenye thamani ya shilingi 9.1 bilioni kwenye Mashirika ya Kimataifa ambako Tanzania ni mwanachama kwa lengo la kudumisha uanachama au kuongeza hisa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu inalenga kufanya mazungumzo na Wafadhili mbalimbali kwa lengo la kupata misaada na mikopo nafuu kiasi cha shilingi 1,631.3 bilioni kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kusimamia Misaada Tanzania, kukamilisha Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada, kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kusimamia misaada na miradi ya maendeleo, kuimarisha uanachama wetu katika mashirika ya Kimataifa na kuchangia juhudiza kupunguza deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya zingine na kikanda. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika kufanikisha kuridhiwa na Bunge la Tanzania, Itifaki ya Ushuru wa Forodha wa Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 9 Novemba, 2004 iliyoanza kutumika rasmi tarehe 1 Januari, 2005. Aidha, Wizara yangu ilishiriki katika mikutano yote ya kikanda na kimataifa hususan katika masuala ya fedha pamoja na kufanya tathmini za pamoja kati ya Serikali na Jumuiya hizo kwa lengo la kuboresha ufanisi na manufaa ya ushirikiano. Kwa mwaka 2005/2006, Wizara itaimarisha zaidi ushiriki wake katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa matumizi ya fedha za Serikali. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara ilitekeleza yafuatayo:

(i) Kufuta sheria ya ununuzi ya mwaka 2001 na kutunga sheria mpya ya ununuzi ya mwaka 2004;

(ii) Kuendelea na utaratibu wa *'cash budget'* na matumizi ya mtandao wa malipo kwa kutumia Kompyuta katika kutayarisha Bajeti na kufanya malipo *(IFMS);* na

(iii)Kuendelea na ukaguzi wa matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa madeni na mikopo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Deni la Taifa pamoja na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 na marekebisho yake. Mwongozo wa Utekelezaji wa Mkakati wa kusimamia madeni umeandaliwa na Wizara yangu na

kuridhiwa na Kamati ya Taifa ya Kusimami Madeni. Aidha, Kamati hiyo inaendelea kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya mikopo na madai mbalimbali yaliyowasilishwa. Katika mwaka 2004/2005; Kamati hiyo ilichambua mapendekezo na madai yenye thamani ya shilingi 118.9 bilioni na kupendekeza mikopo mipya na madai yenye thamani ya shilingi 111.1 bilioni. Mikopo mipya ni kwa ajili ya miradi kwenye sekta za mawasiliano na usafirishaji, nyumba, maji na huduma nyingine za jamii. Madai yanatokana na huduma mbalimbali ambazo zilitolewa na malipo hayakuwa yamefanyika kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itatekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kutafuta mikopo kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu ambayo inalenga katika kutusaidia kujenga uwezo wa kujitegemea hatua kwa hatua pamoja na kutusaidia kutekeleza kwa haraka mikakati ya kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali juu ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 na marekebisho yaliyopitishwa na Bunge lako katika kikao chake cha Aprili, 2003; na

(iii) Kufanya mazungumzo na nchi wahisani ambazo bado hazijatoa msamaha wa madeni hususan kundi lisilo la Paris ili kupata misamaha ya madeni chini ya mpango wa Msamaha wa Madeni kwa Nchi Maskini.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha *(JFC),* katika mwaka wa fedha 2004/2005, Tume imetekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kumtafuta mtaalamu wa kuchambua vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za uendeshaji wa mambo ya Muungano. Aidha, Tume imeweza kufanya uchambuzi wa Wizara, Idara na Asasi za Muungano kwa lengo la kubaini gharama za uendeshaji wake. Vilevile, takwimu za madeni baina ya pande mbili za Muungano zilifanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa fanisi, Sheria ya Tume Na.14 ya mwaka 1996 imefanyiwa mapitio ili kuiboresha. Katika mwaka huu wa fedha 2005/2006, Tume inakusudia kupitia ripoti za kazi zilizotajwa hapo juu na kutoa ushauri wake Serikalini. Aidha, Tume itaandaa semina kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ili kupata maoni juu ya mahusiano ya kifedha katika masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa fedha na mali ya umma, usimamizi wa fedha za umma. Wizara yangu itaendelea kuboresha mtandao wa malipo kwa kutumia Kompyuta *(IFMS)* ili kuboresha malipo, kudhibiti wizi na ubadhirifu wa fedha na mali ya umma. Vilevile, Wizara yangu itaimarisha uwezo wa Serikali na kuendela na shughuli za malipo pindi itokeapo dharura au ajali kwenye mtandao wa malipo kwa kuhakikisha kwamba *Disaster Recovery System* inafanya kazi ipasavyo. Aidha, nafasi zilizo wazi kwenye kada ya Ukaguzi wa Ndani ambayo tayari muundo wake umekamilishwa, zinatarajiwa

kujazwa katika mwaka wa fedha 2005/2006, kutoka kwenye soko *(labour market)* na vilevile Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imerekebisha utaratibu wa kuajiri watumishi ambapo kila Wizara, Idara au Mkoa hutakiwa kutangaza nafasi zake za kazi kwenye vyombo vya habari. Utaratibu huu unatumika katika ajira za kada zote. Hata hivyo, kufuatana na umuhimu uliopo katika eneo la usimamizi wa fedha za umma, bado kada za Uhaisibu na Ukaguzi wa Ndani zitaendelea kusimamiwa na Hazina kwa kipindi cha miaka miwili zaidi kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006. Hi ina maana kuwa Wizara yangu itaendelea na mamlaka yake ya kuwapanga na kuratibu shughuli za Wahasibu kwa lengo la kuimarisha kada ya uhasibu na ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana 2004/2005 nilieleza lengo la Wizara yangu kudhibiti na kuboresha mapato yatokanayo na Visa. Tayari mzabuni amepatikana na mkataba umesainiwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa utaratibu huu wa visa za kisasa tayari umeanza katika Ubalozi wetu uliopo Uholanzi kama awamu ya kwanza. Aidha, vituo vya Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, Zanzibar, Balozi zetu za London, Paris, Washington na Roma zitahusika katika majaribio ya awamu ya pili. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha ubora wa Visa hizo na kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza kabla ya kusambaza utaratibu huo kwenye Balozi zetu zote.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma, mabadiliko ya Sheria ya Ununuzi wa Umma yaliyoanza katika mwaka 204/2005 yalikamilishwa, na Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 ilipitishwa kuchukua nafasi ya Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2001. Mabadiliko makubwa katika Sheria hiyo ambayo imeanza kutumika rasmi mwezi Mei, 2005 ni:-

(i) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Zabuni *(Public Procurement Regulatory Authority);* na

(ii) Wizara na Taasisi kupewa Mamlaka kamili ya maamuzi yote ya Zabuni.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, pamoja na masuala mengine Wizara yangu itaanzishw kada ya wataalam wa ununuzi Serikalini *(Procurement Cadre)* na kuweka utaratibu wa kuanzishwa kwa vitengo vya ununuzi *(Procurement Management Unit)* katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma. Aidha Wizara itaandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wanaoshughulikia ununuzi wa umma na kukagua manunuzi *(Procurement Audit)* yaliyofanywa na Serikalini na Taasisi zake ili kubainisha kuwa yamezingatia Sheria na Kanuni. Pia, Wizara inatayarisha mwongozo utakaoelimisha Umma juu ya namna ya kufikisha malalamiko na migogoro kwenye Mamlaka ya Rufaa za Zabuni. Napenda kutoa taarifa kuwa Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imeanza kazi rasmi mwezi Septemba 2004 na kanuni za utekelezaji wa sheria ya ununuzi

zipoa katika hatua za mwisho za maandalizi tayari kwa kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili ziweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, huduma za rufani za kodi, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Bodi ya Rufaa za Kodi, ilipokea rufaa 69 ambazo zilijumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*. Kati ya hizo, rufaa 64 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Vilevile, Baraza la Rufani za Kodi lilipokea rufaa 30 na kati ya hizo rufaa 28 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na usikilizaji wa rufana za kodi, Bodi na Baraza zimeendelea kutoa elimu kwa wananchi katika Mikoa mbalimbali juu ya utaratibu mzima wa ufunguaji wa rufaa katika vyombo hivi. Wafanyakazi kadhaa wamehudhuria mafunzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Bodi na Baraza zitaendelea kusikiliza rufaa zilizokwisha pokelewa na kusikiliza rufaa zitakazofunguliwa na kuzitolea maamuzi mapema iwezekanavyo. Zoezi la kuendelea kuelimisha wananchi katika mikoa na Wilaya mbalimbali litaendelea pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ioli kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa mali ya Serikali, Serikali hutumia fedha nyingi katika ununuzi wa vifaa ikiwa ni pamoja na magari, mitambo, pikipiki na vifaa vvingine. Wizara yangu imeendelea na utaratibu wa uhakiki wa mali hizo kwa lengo la kutambua vifaa sinzia, chakavu na vile vuluvyo katika hali nzuri ya kuridhisha. Aidha vifaa ambavyo vinagundulika kuwa ni sinzia au chakavu hufutwa kutoka kwenye vitabu na kuuzwa kwa njia yam nada. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, shilingi milioni 475.5 zilikusanywa kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na zoezi la kutathimini mali zake. Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2004/2005, Wizara nane tayari zilikuwa zimepatiwa mthamini ambaye alipatikana kwa njia ya ushindani. Kazi ya uthamini katika Wizara hizo imeshaanza. Aidha mthamini kwa Wizara nyingine kumi na mbili atapatikana hivi karibuni kufuatia kufunguliwa kwa zabuni zilizopokelewa. Kundi lingine ambalo ni la tatu na la mwisho litajumuisha Wizara na Idara 12.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Wizara yangu kuwa zoezi la kuthamini likikamilika Serikali itakuwa katika nafasi nzuri ya kujua mali zake. Aidha zoezi hilo litaiwezesha Serikali kusimamia vyema mali zake kwa kuanza kutumia njia za kisasa zinazotumia kompyuta katika kudhibiti mwenendo na matumizi ya mali zake.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa rasilimali za Serikali katika mashirika ya umma, katika mwaka 2004/2005. Wizara ya Fedha iliendelea kusimamia hisa za Serikali katika mashirika mbalimbali pamoja na taasisi za umma kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 418 *(Treasury Registrar Ordinance - Cap 418)* na Sheria ya Mashariki ya umma ya mwaka 1992. katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali

ilitarajia kupta gawio la shilingi bilioni 9.9 kutoka katika mashirika ambayo Serikali bado ina hisa pamoja na marejesho ya mikopo na mapato mengine ya shilingi 35.2 bilioni.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005 mapato yatokanayo na gawio ya kiasi cha shilingi 12.5 bilioni yalipokelewa ktuoak Benki Kuu ya Tanzania, Kampuni ya Bia, Kampuni ya Sigara, Tanzania *Development Finance Limited, National Bank of Commerce Limited, Kilombero Sugar Company Limited* na Kampuni ya Saruji Wazo. Aidha shilingi 15.1 bilioni zilipatikana kutokana na marejesho ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi na udhibiti wa hesabu za Serikali, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu yameainishwa chini ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, ambapo anawajibika kukagua hesabu za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma. Aidha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amepewa uwezo wa kuteua wakaguzi binafsi kukagua hesabu za Mashirika ya Umma chini ya ungalizi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, ofisi ya Mkaguzi Mkuu ilikagua hesabu za Wizara 47, Mikoa 21, Halmashauri 117 na Ofisi zote za Ubalozi. Aidha mashirka 40 ya umma yaliwasilisha hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na kukaguliwa, ofisi imewapatia watumishi wake mafunzo mbalimbali ndani na nje ili kuboresha utendaji kazi. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, ofisi imelenga kukagua hesabu 47 za Wizara na Idara za Serikali, Mikoa 21 ya Tanzania Bara, Halmashauri 117 za miji na Wilaya na Balozi 10 za Tanzania. Aidha hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma 140 na kuhakikisha kuwa vitendea kazi vinaboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Wafanyakazi, Ajira na Mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya watumishi 107 waliajiriwa katika fani ya Uhasibu, Uchumi, Utawala, Habari, Komputa, Uhakikimali, Usimamizi wa Fedha, Uchambuzi kazi, Uwakili wa Serikali na Dereva. Aidha watumishi 319 walipewa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 288 walipewa mafunzo ya muda mrefu watumishi 288 walipewa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, asasi za mafunzo, katika mwaka wa fedha 2004/2005 vyuo vimetoa wahitimu katika fani mbalimbali wapatao 1,299. Aidha katika mwaka 2005/2006, vyuo hivyo vinatarajia kutoa wahitimu 1,668. Wizara ilitoa udhamini wa wanafunzi 1,719 katika mwaka 2004/2005, ambao kati yao 1,059 walikuwa watarajali na imepanga kudhamini wanafunzi 2,300 katika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara, mkakati wa ufanisi na usalama wa malipo kwa wafanyakazi, mwaka jana nilizungumzia waraka ambao ungetoa utaratibu mpya unaoainisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za mishahara, waraka huu umeshatolewa na ulianza kutumika Julai 2004. Utaratibu huu mpya umesaidia kudhibiti matatizo yaliyokuwepo na Wizara yangu inaendelea kuufanya tathimini, kwa lengo la kuuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya mishahara na posho mbalimbali za watumishi, kwa kutumia utaratibu huu mpya jumla ya shilingi 18.4 bilioni zimetumika kulipa malimbikizo ya mishahara ya Walimu, Watumishi wengine wa Halmashauri kwa

sekta zinazopata ruzuku toka Serikalini pamoja na watumishi wengine wa Serikali Kuu. Kati ya fedha hizo shilingi 11.1 bilioni zilitumika kulipa malimbizo ya mishahara ya Walimu na shilingi 7.3 bilioni zilitumika kulipia malimbikizo ya mishahara ya watumishi wengine wa Halmashauri. Aidha, madai ya posho mbalimbali za watumishi wengine wa Serikali yataanza kulipwa pale tu yatakapowasilishwa na kuhakikiwa na kuthibitishwa kuwa ni madai halali.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa wastaafu, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kupunguza adha inayowapata wastaafu. Moja ya hatua hizo ni ile ya kuwarudisha wastaafu waliochukua mafao yao kwa mkupuo katika daftari la malipo ya kila mwezi, zoezi ambalo lilianza rasmi mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2004 hadi Juni, 2005 tumafanikiwa kulipa wastaafu 54,047 kiasi cha shilingi 46.3 bilioni. Aidha, katika mwaka 2004/2005 wastaafu 14,547 walijiandikisha na kati ya hao wastaafu 10,881 walifanikiwa kurejeshwa kwenye madaftari na kulipwa. Wastaafu 3,666 waliobaki hawakurejeshwa kwenye daftari kwa wakati kwa sababu zoezi la kupitia kumbukumbu zao limechukua muda mrefu kuliko ilivyotegemewa. Wastaafu wanaostahili wataendelea kurejeshwa kwenye daftari na kulipwa kila kumbukumbu zao zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na zoezi la kuwarejesha wastaafu kwenye daftari kufanikiwa kumekuwepo na mapungufu yafuatayo:-

(i) Wengi wa waliojiandikisha walitumia namba ambazo sio sahihi na nyingine zilikuwa ni za wastaafu wengine ambao ni marehemu;

(ii) Wengine waliojiandikisha ni wale wasiostahili kurejeshwa kutokana na masharti yao ya kazi ya awali kama wale waliokuwa kwenye *"Operational Service"*. Wastaafu waliokuwa chini ya utaratibu huu hulipwa mafao yao yote pale wanapostaafu na hawastahili pensheni; na

(iii) Wengine waliojiandikisha ni wale ambao hawakutimiza masharti kwa kuwa hawakuwa wametimiza miaka kumi au zaidi kuanzia tarehe waliyostaafu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF),* katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF)* ulikamilisha maandalizi ya Mpango wa Miaka Mitano (2005/2006 – 2009/2010) pamoja na Miongozo ya Utawala wa Fedha. Hatua hii imerahisisha usimamizi wa michango ya wanachama, uendeshaji wa Mfuko wa kuweka taratibu nzuri za uwekezaji wa fedha za wanachama. Mpango huu ndiyo utakuwa dira ya Mfuko kwa kipindi chote cha miaka mitano kuanzia Julai 1, 2005. Hivi sasa Mfuko unapitia upya Sheria iliyoanzisha Mfuko (Cap. 51 ya 1942) kwa lengo la kutayarisha sheria mpya itakayokidhi mahitaji ya sasa. Mazungumzo yanaendelea baina ya Wizara na Mfuko ili kuandaa taratibu zitakazowezesha wastaafu wote walio katika masharti ya akiba kulipwa mafao yao yote kupitia katika Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004.2005, Mfuko umeendelea kupokea wanachama pamoja na michango yao kama ifuatavyo: Wanachama wapya ambao walijiunga na Mfuko hadi kufikia Juni 2005 walikuwa 2,200 hivyo kufanya jumla ya wanachama wote kuwa 17,000. Hadi kufikia Juni 2005 Mfuko umekusanya jumla ya shilingi 5.5 bilioni kutoka kwa wanachama na shilingi 4.05 bilioni zinatokana na michango ya wanachama na shilingi 1.5 bilioni zinatokana na vitega uchumi. Thamani ya Mfuko inakadiriwa kufikia shilingi 24.1 bilioni ifikapo Juni 2006 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 22 ikilinganishwa na Shilingi 19.6 bilioni zinazotarajiwa kufikiwa mwezi Juni 2005.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini pamoja na kulipa mafao umejiwekea utaratibu wa kuwaazima wanachama michango yao kwa lengo la kuitumia kuandaa maisha yao ya baadaye bado wangali kazini. Kwa mwaka 2004/2005, Mfuko ulitenga shilingi 200.0 milioni ambapo hadi kufikia 30 Juni, 2005, kiasi cha shilingi 180.0 milioni sawa na asilimia 90 ilikwishatolewa kwa wanachama kwa utaratibu huo. Ni matarajio ya Wizara kuwa mikopo hiyo inawasaidia wanachama kuandaa mazingira mazuri ya kustaafu. Vilevile, Mfuko unakamilisha taratibu zitakazowezesha kuwapatia wanachama taarifa kuhusu akiba zao katika Mfuko kila mwaka zikionyesha michango ya mwajiri na faida iliyotolewa na Mfuko kama gawio la mapato yanayotokana na kuwekeza michango yao. Kwa kuanzia taarifa hizi zitaanza kutolewa katika robo ya tatu ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF),* Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma uliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili, kuhifadhi kumbukumbu za wanachama, kukusanya michango na kuwekeza. Wastaafu wa kwanza wa Mfuko huu walianza kulipwa tarehe 1 Julai, 2004 baada ya kuamlizika kipindi cha mpito tarehe 30 Juni, 2004. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005, jumla ya wastaafu 1,512 walikwishalipwa mafao ya kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi kiasi cha shilingi 21.2 bilioni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005, thamani ya Mfuko ilifikia shilingi 392.2 bilioni. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Mfuko unatarajiwa kuongezek kwa kiasi cha shilingi 49.7 bilioni na hivyo kufanya thamani yake kufikia shilingi 378.9 bilioni tarehe 30, Juni, 2006. Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006, kiasi cha shilingi 57.3 bilioni zimetengwa kwa ajili ya mafao ya wastaafu 1,916.

Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* umeongeza Makusanyo ya mapato kutoka Shilingi 15.44 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 55.48 bilioni mwaka 2004. Wakati huo huo thamani ya Mfuko imekua kutoka Shilingi 20.3 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 198.1 bilioni mwaka 2004. Matarajio ni kwamba thamani ya Mfuko itafikia Shilingi 220.8 bilioni mwaka 2005. Aidha mafao ya wastaafu yameongezeka kutoka Shilingi 2.1 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 14.0 bilioni mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, mfuko utaendeleza mkakati wa kupanua wigo wa wanachama wake kwa kurekebisha sheria ya PPF ya mwaka 2001,

kuanzisha mafao mapya kama mafao ya Elimu *(Education Benefit),* kushiriki katika mipango ya kuendeleza makazi, kutumia tekinolojia ya kisasa kurahisisha utoaji wa huduma, kujenga majengo ya biashara na kushirikisha wanachama katika shughuli za mfuko. Katika mwaka 2005/2006 Serikali imeazimia kutayarisha sera itakayoongoza shughuli za uwekezaji wa mifuko ya pensheni ili iweze kushiriki kwa ufanisi zaidi katika mikakati ya kukuza uchumi na wakati huo kuhakikisha kuwa mafao ya wanachama wake yapo salama.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieza Bunge lako wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha imedhamiria kulipa mafao ya Watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mapema iwezekanavyo kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais. Napenda kutoa taarifa kuwa, zoezi la kukokotoa kiasi cha pensheni kwa kupitia jalada kwa jalada limeanza chini ya Usimamizi wa Mhasibu Mkuu wa Seriali. Zoezi hilo linategemewa kukamilika haraka iwezekanavyo. Walengwa wote watatangaziwa kupitia vyombo vya habari tarehe na sehemu malipo yatakapofanyika.

Mheshimiwa Spika, habari, Elimu na Mawasiliano, wizara yangu kwa mwaka 2004/2005, iliendelea kutekeleza kikamilifu sera ya uwazi na ukweli kwa kutoa habari muhimu za matukio mbalimbali yanayotokea ndani ya Wizara na sekta ya fedha kwa ujumla. Wizara yangu imeendelea kuimarisha mawasiliano na wadau wake. Katika mwaka 2005/2006, imeazimia kuelimisha wananchi, wajibu wa Wizara ya Fedha, sera na mikakati bora inayotekelezwa kwa manufaa ya taifa letu. Lengo ni kuongeza uelewa zaidi wa huduma zinazotolewa na Wizara na asasi zake na hatimaye kujenga hali ya utendaji kazi ya uwazi, ukweli na uwajibikaji. Uzinduzi wa jarida la Wizara na machapisho mengine ni hatua za mwanzo tu za utekelezaji wa azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, mikakati dhidi ya rushwa, Wizara yangu tayari imekamilisha rasimu ya kuhuisha mkakati wa kupambana na rushwa katika wizara yangu ambayo itaingizwa katika mkakati wa kitaifa wa kupambana na rushwa kwa kipindi cha 2005 – 2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kutekeleza mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa katika ukusanyaji wa mapato na katika matumizi ya Serikali. Msisitizo katika kipindi kijacho cha kutekeleza mkakati wa kupambana na kero ya rushwa 2005 – 2010 utaekelezwa katika kuzishirikisha katika vita dhidi ya rushwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara na sekta ya fedha ili kuhimiza uwazi na uadilifu katika kusimamia mwenendo wa mapato na matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Jinsia, Wizara yangu ni miongoni mwa Wizara zinazotoa kipaumbele kwenye masuala ya Jinsia. Katika utoaji wa madaraka kwa maafisa wanawake, Wizara yangu imeshavuka lengo la asilimia 30 lililowekwa na nchi za *SADC*. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imepata mialiko mbalimbali kwenda kuelezea jinsi tunavyotekeleza na kuainisha masuala ya jinsi tunavyotekeleza na kuainisha masuala ya jinsia katika Bajeti ya Serikali. Aidha kwa ajili ya kuweka mkazo zaidi katika jambo hilo, Wizara yangu imeteua Afisa anayeshughulikia masuala ya jinsia kwa kila Idara. Mwaka 2005/2006, Wizara itawapa mafunzo maafisa hao ili kuimarisha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu ikishirikiana na *UNDP* na *TACAIDS* ilikamilisha kuandaa taarifa ya tathimini ya hali ya UKIMWI ndani ya Wizara. Taarifa hiyo imetoa mapendekezo ya hatua gani zichukuliwe. Hatua zilizopendkezwa ni pamoja na:-

(i) Kudhibiti kuenea virusi vya UKIMWI kwa kushawishi wale ambao hawajaadhirika wasiathirike.

(ii) Kuwapa motisha Wafanyakazi wapime kwa hiari ili waweze kusaidiwa Wizarani.

(iii) Kuwapa uwezo wa kuishi kwa matumaini wale walioathirika.

(iv) Kuwa na mikakati ya kuzuia maambukizi mapya na;

(v) Kuwapa uwezo wa kuishi kwa matumaini walioathirika pamoja na kuongeza kuhamasisha Wafanyakazi wote na kuwafundisha stadi za maisha zitakazowawezesha Wafanyakazi wabadili tabia.

Mheshimiwa Spika, mpango ulipendekezwa katika taarifa ya tathmini ni pamoja na kutoa msaada kwa wale walioathirika kisaikolojia (ushauri nasaha) na kumudi maisha (lishe na njia ya kuongeza mapato); aisha Wizara kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) itawasaidia waathirika kwa kutoa huduma majumbani pale muathirika anaposhindwa kwenda kazini *(Home Based Care).*

Mheshimiwa Spika, huduma za kiuchumi zinazotolewa na sekta ya fedha, huduma za kibenki. Huduma za kibenki na Taasisi nyingine za fedha zimeendelea kukua na kuongeza ubora mwaka hadi mwaka. Mazingira ya utoaji mikopo kutoka katika Mabenki yameboreshwa sana, ambapo riba imeshuka kutoka zaidi ya asilimia 26 hadi asilimia 14.4 hivi sasa. kushuka kwa riba ni matokeo ya ongezeko kubwa la Mabenki kutoka Benki mbili mwaka 1995 kufikia Benki 26 zilizopo hivi sasa. aidha Taasisi nyingine za fedha zimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufanisi uliotajwa, Benki Kuu inaandaa mwongozo wa uendeshaji wa sekta ya micro finance ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya uboreshaji wa shughuli za vyama vya Ushirika vya kuweka na kukopa (*SACCOS*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu itaendelea kuweka mazingira mazuri ili kuhamasisha ongezeko la mikopo kutoka mabeni kwa Sekta Binafsi. Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 2004 na kuongezeka kwa kasi ya upimaji wa viwanja kutaiwezesha ardhi itumike kama dhamana kwa mikopo ya Mabenki.

Mheshimiwa Spika, Benki za Umma, *National Microfinance Bank (NMB), NMB* iliyoanzishwa mwaka 1997 iliendelea kutoa huduma za kibenki kwa wateja wadogo

ambapo hadi kufikia mwisho wa mwaka 2004, ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 91.15 bilioni ikilinganishwa na Shilingi 236.8 milioni mwaka 2000 ilipoanza kutoa mikopo. Aidha Benki hiyo imeendelea kuwa na mtandao mkubwa kuliko Benki nyingine nchini kwa kuwa na matawi yanayofikia 108. Kati ya matawi hayo matawi 36 yameshaunganishwa katika mtandao wa kompyuta na yaliyobaki yanatarajiwa kuunganishwa katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, *NMB* ilipata mapato ya Shilingi 34.9 bilioni kutokana na riba ya mikopo na Shilingi 20.48 bilioni kutokana na shughuli nyingine za kibenki. Pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, Benki hii imeendelea kupata faida kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 1999 ambapo mwisho wa mwaka 2004 benki hiyo ilipata faida ya Shilingi 18.57 bilioni baada ya kodi. Kulingana na mpango wa biashara, Benki inatarajia kuendelea kupata faida.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB),* mikopo inayotolewa na Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* imeongezeka kutoka Shilingi 957 milioni mwaka 1995 hadi kufikia Shilingi 16.55 bilioni mwaka 2004. Aidha thamani ya Benki hii imekua kwa kiasi kikubwa kutoka Shilingi 1.97 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 44.23 bilioni mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali *TIB* itarekebishwa kwa lengo la kuifanya kuwa Benki ya maendeleo *(Development Bank).* Lengo ni kuiwezesha kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa uwekezaji katika miradi mikubwa ya maendeleo kwa kutoa mikopo kufikia Shilingi 27.00 bilioni ifikapo mwishoni mwa mwaka 2005. Aidha amana za wateja zinatarajiwa kukua na kufikia Shilingi 40.00 bilioni ili kuchangia katika sera ya Serikali ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta Tanzania *(TPB),* Benki ya Posta imekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika kipindi chote ambapo ukusanyaji wa amana yameongezeka kutoka Shilingi 20.4 bilioni mwaka 1995 hadi kufikia Shilingi 52.0 bilioni mwezi Aprili, 2005. Idadi ya wateja wa Benki imekuwa kutoka wateja 840,000 mwaka 1995 kadi wateja 1,128,438 hapo Aprili, 2005. Aidha uwekezaji katika vitega uchumi uliongezeka kutoka Shilingi 16.8 bilioni mwaka 1995 hadi kufikia Shilingi 42.9 bilioni mwezi Aprili, 2005.

Mheshimiwa Spika, shughuli ya kutoa mikopo ya aina mbalimbali ikiwemo mikopo ya biashara, mikopo ya Watumishi na mikopo midogo midogo imeongezeka hadi kufikia Shilingi 13.1 bilioni mwezi Aprili, 2005 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 419.1 milioni kilichotolewa mwaka 1998. Ufanisi huu umewezesha *TPB* kupata faida ya Shilingi 1,136.6 milioni kwa mwaka 2004. Katika mwaka 2005/2006, *TPB* imelenga kukuza amana za wateja na vitega uchumi, kuongeza utoaji wa mikopo midogo kwa wateja wake na kuboresha mtandao wake wa kompyuta ili kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, *Twiga Bankcorp Limited*, kufuatia mabadiliko ya jina na muundo, Benki hii ambayo ni ndogo kuliko zote imeanza kuimarika. Mtaji wake

umeongezeka kutoka Shilingi 1.7 bilioni mwanzo wa mwaka 2004 hadi Shilingi 2.4 bilioni mwezi Juni 2005. Aidha, amana za wateja zimeongezeka kutoka Shilingi 11.3 bilioni mwaka 2004 hadi Shilingi 13.9 bilioni Juni 2005. Katika kipindi hicho Benki hii iliweza kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 6.0 bilioni na kupata mapato ya Shilingi 3.0 bilioni na faida ya Shilingi 565.0 milioni. Twiga *Bancorp* inalenga kuongeza amana za wateja na kutoa mikopo zaidi kwa wateja wake.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa fedha haramu *(Anti-Money Laundering),* baada ya kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, Wizara yangu imewasilisha Serikalini rasimu ya awali ya Waraka wa Baraza la Mawaziri yenye mapendekezo ya kutunga sheria mpya na madhubuti ya udhibiti wa Fedha haramu pamoja na vitendo haramu vinavyoambatana na fedha hizo. Aidha hatua hii ni katika kukidhi matakwa ya itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya uhalifu wa Kimataifa yaani *The united Nations Convention Against Transnational Organized Crime* 2000. Ni matumaini yangu kwamba Bunge lijalo chini ya Muswada na kuwa sheria. Vile vile, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama na Makao Makuu ya Sekretarieti ya Umoja wa Nchi za Mashariki na Kuisni mwa Afrika za Udhibiti wa Fedha haramu yaani *The Eastern and Southern Africa Anti- Money Laundering Group (ESAAMLG).*

Mheshimiwa Spika, Huduma za Bima, maendeleo ya sekta kwa ujumla, kufuatia biashara ya bima hapa nchini kufanywa huria, idadi ya Makampuni ya bima imeongezeka kutoka Makampuni mawili (2) mwaka 1995 hadi 14 mwisho wa mwaka 2004. Aidha, Kampuni za madalali zimeongezeka kutoka Kampuni moja (1) hadi Makampuni 47 na wakala kufikia 350. Pato la Bima nalo limeongezeka kutoka Shilingi 32.0 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 83 bilioni mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma kwa wateja, madai yameongezeka kutoka Shilingi 14.0 bilioni kwa mwaka 1995 hadi kufikia Shilingi 29.0 bilioni mwaka 2004. Malipo halisi kati ya Januari, hadi Machi 2005 yalifikia Shilingi 21.0 bilioni. Vitega uchumi katika sekta ya bima vimeongezeka kutoka Shilingi 87.0 bilioni hadi Shilingi 124.0 bilioni kwa kipindi hicho hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, pato la shughuli za bima linatarajiwa kukua kwa asilimia 15 kutokana na kuendelea kupanuka kwa shughuli za bima mikoani, kuendelea kuimarika kwa bima za mtawanyo na kuanza kwa bima ya kinga ya majanga ya kisiasa *(political risks)* pamoja na bima za mikopo *(credit risk insurance)* inayotolewa na *Africa Trade Insurance Agency*. Bima hii inatarajiwa kuwezesha bidhaa za Kitanzania kuvutia waagizaji walioko nje.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa *(NIC),* Shirika la Bima la Taifa linakabiliwa na madai mengi na ya muda mrefu ambayo ni kero kubwa kwa wateja wake. Hata hivyo Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na *PSRC* imekuwa inasimamia taratibu za upatikanaji wa fedha zinazotumika kulipa madeni yanayothibishwa na kupunguza deni hilo. Aidha, Wizara yangu imekopesha *NIC* jumla ya Shilingi 4.0 bilioni ili ilipe madai haya mara moja.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kuondokana na tatizo la *NIC*, ni pamoja na kuendelea kubainisha mali za kuuza ili kupunguza madai ya bima. Aidha, kwa kushirikiana na *PSRC*, Wizara inakamilisha mkakati wa kubinafsisha Kampuni hii kama biashara moja au biashara tofauti za Bima ya Maisha (*Life*) na Bima isiyo ya Maisha *Non Life*).

Mheshimiwa Spika, asasi za uwekezeshaji wananchi kuwezesha, mamlaka ya masoko ya mitaji na dhamana. Kuanzia mwaka 1995 hadi 2005, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na dhamana (CMSA) ilifanikiwa kuandikisha katika soko la Hisa, hisa za Kampuni saba ambazo ni Kampuni za Bia Tanzania (*TBL*), Sigara Tanzania (*TCC*), Usindikaji Chai (*TATEPA*), Gesi ya Oksijeni *(TOL),* Saruji Tanga, (Simba na Kampuni ya Mizigo Viwanja vya Ndege (*DAHACO*). Aidha, Mamlaka ilitoa kibali kwa Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam kuuza hisa zake kwa wananchi kupitia soko la Hisa. Katika kipindi hicho, hatifungani za Serikali pamoja na sekta binafsi ziliuzwa ili kujipatia mtaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa soko la hisa ni utaratibu mpya hapa nchini, Mamlaka imekuwa ikiendesha programu ya Elimu kwa umma ili kuongeza uelewa na ufahamu kwa wananchi juu ya masuala ya uwekezaji katika soko la hisa. Aidha, Mamlaka inasimamia uwekezaji wa pamoja, kutafiti jinsi ya kuboresha Miundo mbinu ya kuendesha masoko ya mitaji kuhusia na kodi, utumiaji wa tekinolojia ya kisasa na kuweka taratibu na mfumo wa soko la mitaji hapa nchini na nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio ya uchumi wetu, Makampuni ya nje ya Kenya *Airways* na *East African Breweries (EABL)* nayo yamejiandikisha katika soko letu. Aidha, Kampuni binafsi na za Kimataifa kama *PTA Bank, East African Development Bank (EADB), BIDCO Oil Company, Barclays Bank (Tanzania)* na *Standard Chartered Bank (Tanzania)* nazo zimeandikisha hatifungani zake katika soko la hisa la Dar es Salaam zote zikiwa na thamani ya Shilingi 280 bilioni.

Mheshimiwa Spika, asasi ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania *(Unit Trust of Tanzania – UTT)* iliyoanzishwa rasmi mwaka 2003, tarehe 16 Mei, 2005 ilizindua mfuko wa mwanzo wa uwekezaji wa pamoja uliopewa jina la Mfuko wa Umoja *(Umoja Fund*). Mfuko huu ni mpango wa kwanza wa uwekezaji wa pamoja kuanzishwa hapa nchini. Taarifa za awali zinaonesha kuwa tangu mauzo yaanze hapo tarehe 16 mei, 2005 jumla ya vipande 11,947,378 vyenye thamani ya Shilingi 7.83 bilioni vimeuzwa. Lengo la mfuko huo ni kutoa fursa kwa wananchi wote kushiriki katika umiliki wa makampuni ya umma yaliyobinafsishwa, kuhimiza uwekaji akiba na kuchochea ongezeko la ushiriki katika masoko ya mitaji na hisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kwa kutambua umuhimu wa chombo hiki ilitenga na kuikabidhi *UTT* umiliki wa asilimia 2 ya hisa katika Kampuni ya Bia *(TBL)* sawa na Shilingi 9.8 bilioni na asilimia 1 katika Kampuni ya Sigara *(TCC)* saa na Shilingi 1.8 bilioni kama mtaji wa awali *(seed capital).* Aidha, Wizara pia imeidhinisha *UTT* kutoa punguzo la bei ya ununuzi wa vipande (units) kwa asilimia 30, zitakazouzwa awali *(Initial Public Offering – IPO)* kwa lengo la kuhamasisha wananchi walio wengi kuwekeza katika mpango huu mpya. Bei ya kipande inauzwa kwa Shilingi 70.00 badala

ya Shilingi 100.00 katika mwaka 2005/2006, *UTT* itaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha zaidi shughuli ya uwekezaji pamoja.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya udhamini wa mikopo, Wizara yangu kupitia Benki Kuu imeendelea kusimamia uendeshaji wa mfuko wa dhamana kwa mikopo inayosaidia wauzaji bidhaa nje *(ECGS)* na ule wa dhamana kwa mikopo midogo na ya kati *(SME – CGS)*. Itakumbukwa kwamba mfuko wa *ECGS* ulianzishwa Julai, 2002 ukiwa na mtaji wa Shilingi bilioni 6.5. Hadi kufikia Desemba, 2004 mfuko huu umeongezeka na kufikia Shilingi bilioni 21.1. kati ya mtaji huu Shilingi bilioni 18 zimetolewa na Serikali na Shilingi bilioni 1.5 zimetolewa na Benki Kuu ya Tanzania na Shilingi bilioni 1.6 bilioni zimetokana na riba pamoja na ada ya udhamini. Kwa mwaka 2004/2005, Shilingi bilioni 2.0 ziliuwa zimetengwa kwa ajili ya mfuko wa miradi midogo na ya kati yaani *SME – CGS.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, mfuko wa *ECGS* ulitoa dhamana kwa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.3 bilioni kwa vyama vikuu vya ushirika na Shilingi bilioni 11.9 kwa miradi inayozalisha kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi. Wakati huo huo, mfuko wa *SME – CGS* umekamilisha taratibu zote za uendeshaji wake na utaanza kutoa dhaman katika mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, vile vile, wizara yangu inakamilisha taratibu za kuanzisha mfuko kwa ajili ya miradi mikubwa *(DFGF)* ambao unategemewa kuanza kutoa dhamana katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za ukusanyaji madeni, Mfuko wa Udhamini wa Mikopo na Madeni *(LART)* katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005 umekusanya jumla ya shilinig bilioni 21.8 kutokana na akaunti za madini yaliyorithiwa kutoka zilizokuwa Benki ya taifa ya Biashara *(NBC)* na Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini *(CRDB)*. Aidha, kufuatia marekebisho ya Sheria inayounda *LART* ambayo yaliongeza wigo wa Taasisi na makampuni yanayoshughulikiwa na *LART*, madeni mengine yeney thamani ya Shilingi bilioni 34.0 yaliongezwa. Kutokana na madeni haya, *LART* iliweza kuilipa Serikali jumla ya Shilingi bilioni 14.1 pamoja na kulipa wadai wengine jumla ya Shilingi bilioni 3.6. aidha, jumla ya Shilingi bilioni 13.47 zimekusanywa katika ufilisi wa makapuni.

Mheshimiwa Spika, *Consolidated Holdings Corporation (CHC),* kufuatia marekebisho ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)* mwaka 1997, Shirika la *Consolidated Holdings Corporation* lilianzishwa ili kusimamia, kuuza mali, kukusanya madeni na kusimamia hisa za Serikali katika benki mbili zilizoanzishwa yaani *NBC Limited* na *NMB Limited*. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005 shirika limeweza kuuza mali 436 kwa jumla ya Shilingi bilioni 25.7 na kukusanya Shilingi bilioni 22.3. kiasi cha Shilingi bilioni 2.8 kilichobaki kinaendelea kulipwa na wanunuzi kulingana na mikataba kati ya shirika na wanunuzi hao.

Mheshimiwa Spika, kati ya madeni ya Shilingi bilioni 83.03 ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara, Shilingi bilioni 46.0 ni mikopo na Shilingi bilioni 37.1 ni riba inayotokana na mikopo hiyo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005 shirika liliweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 17.0 ikilinganishwa na lengo la Shilingi bilioni 13.3 na kuweza kuwasilisha Serikalini jumla ya Shilingi bilioni 18.0.

Kuhusu biashara ya michezo ya kubahatisha, Bodi ya Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Board of Tanzania)* ilianza kazi ya kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa biashara za michezo ya kubahatisha hapa nchini tarehe 1 Julai, 2003. Bodi hii imeundwa chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003 kwa kufuta sheria za *Pools* and *Lotteries* ya mwaka 1967 na *National Lotteries* ya 1974. kwa mantiki hiyo shughuli zote za kibiashara za michezo ya kubahatisha ikiwemo Bahati Nasibu ya Taifa na Casino, zimeachwa ziendeshwe na Sekta Binafsi na Bodi imebaki na jukumu la kuratibu na kautoa leseni kwa waendeshai. Hadi sasa Bidu unetia leseni sita za kuendesha casino na 292 za michezo ya mashine *(slot machines)* katika Miji ya Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Moshi, Shinyanga, Morogoro na Songea. Aidha, Bodi imetoa leseni mbili kwa ajili ya kuendesha michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa, Lotto na Papo Hapo *(Instant lotteries).* Shughuli hizi zimeingiza Shilingi milioni 681.0 mwaka jana.

Katika mwaka 2005/2006, Bodi imedhamiria kuingia katika hatua ya pili ya kitaalam kwa matumizi ya teknolojia ya mfumo wa menejimenti ya mchezo ya kubahatisha *(Gaming Management System)* katika casino. Hatua hii itasaidia kudhibiti kwa uhakika uendeshaji wa casino na kudhibiti mapato. Kuhakikisha kuwa biashara za mcihezo yote ya kubahatisha inaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Lengo la mwaka 2005/2006 ni kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 1.7 ikilinganishwa na Shilingi milioni 860.6 kwa mwaka 2004/2005. Makadirio na Matumizi kwa mwaka 2005/2006, Maombi ya Fedha. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yaliyobainishwa katika Mpango na Bajeti hii na kufikia malengo yanayokusudiwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 ninaomba Bunge lako liidhinishe bajeti kama ifuatavyo: -

**Fungu 50**

**(a) Matumizi ya kawaida Sh.243,294,291,700/=. Kati ya fedha hizo:**

- Sh. 44,535,249,400/= – Matumizi ya kawaida ya idara zote.
- Sh. 75,153,688,000/= – Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha.
- Sh.123,605,354,300/= – Matumizi maalum.

**(b) Miradi ya maendeleo Sh.21,406,260,000. Kati ya fedha hizo:**

- Sh. 4,272,000,000/= – Fedha za ndani
- Sh.17,134,260,000/= – Fedha za nje.

**Fungu 23**

**(a) Matumizi ya kawaida Sh.85,898,872,300/=. Kati ya fedha hizo: -**

- Sh.1,021,335,700 – Usimamizi wa Deni la Taifa,
- Sh. 2,304,870,500 – Udhibiti wa Matumizi,
- Sh. 69,706,534,600 – Usimamizi wa Fedha na Utawala,
- Sh. 8,445,596,500 – Mfumo na Ukaguzi wa Ndani,
- Sh. 3,970,891,800 – Hazina Ndogo,
- Sh. 449,643,200 – Pensheni na *Gratuity*.

Kati ya Sh.85,898,872,300 zilizotengwa kwa ajili ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, kiasi kikubwa kitatumika kwa kuboresha Mfumo wa Uhasibu na huduma kwa Serikali pamoja na mahitaji mengine ya Kitaifa kama ifuatavyo:-

- Shs.10,000,000,000 – Huduma za Benki,
- Shs.22,461,740,500 – *Treasury Voucher,*
- Shs.20,456,910,000 – *National Health,*
- Shs. 8,445,596,500 – Mtandao wa *IFMS*,
- Shs. 7,378,000,000 – *VISA Stickers,*
- Shs. 2,500,000,000 – Mafunzo kwa Wahasibu,
- Shs.14,656,625,300 – Matumizi ya kawaida kwa Idara.

**(b) Miradi ya Maendeleo Sh.7,773,489,200**

- Sh. 347,000,000 – Fedha za Ndani.
- Sh. 7,426,489,200 – Fedha za Nje.

**Kwa Fungu 22: Deni la Taifa Sh. 523,234,528,000.**

**Kwa Fungu 45: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi:**

**(a) Matumizi ya Kawaida – Sh. 8,147,420,200.00.**
**(b) Miradi ya Maendeleo – Sh. 1,521,000,000.00.**

- Sh. 209,000,000.00 – Fedha za Ndani.
- Sh. 1,312,000,000.00 – Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha itatekeleza majukumu yanayobainishwa katika Mpango na Bajeti hii kupitia Idara, Vitengo, Taasisi zake, pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, namalizia kwa kuwashukuru Manaibu Waziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Wabunge wa Makunduchi na Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu kwa ushirikiano mkubwa walionipa miaka mitano iliyopita na wakati wote wa maandalizi ya makadirio haya. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Mashirika yake chini ya Makatibu Wakuu Bw. Peniel M. Lyimo, Naibu Katibu Mkuu Bw. Ramadhani M. Khijjah, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Benki Kuu ya Tanzania na Asasi nyingine zote zilizofanikisha maandalizi ya Hotuba hii. *(Makofi)*

Mwisho kabisa ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kuniteua na kunipa fursa ya kuitumikia nchi yangu katika nafasi ya Waziri wa Fedha katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Aidha, nakushukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano na msaada mkubwa mlionipa katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita. Nimejifunza mengi kutoka kwenu wote. Asanteni sana. Pia, shukrani za pekee ninazitoa kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Rombo ambao kwa kunichagua kuwa Mbunge wao wameniwezesha kulitumikia Taifa langu katika nafasi hii ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha katika mwaka wa fedha 2004/2005, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 81 kifungu kidogo cha 1 ya kanuni za Bunge toleo la 2004, naomba kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2004/2005, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2005/2006.Awali ya yote naomba kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi na kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Mwanza napenda kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wote wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa CCM na Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum CCM Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi Amina.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Juni, 2005 kamati yangu ilikutana na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil P. Mramba Mbunge, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali za Wizara hiyo ambapo kamati ilipata fursa ya kupitia, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa

mwaka 2004/2005 na taarifa ya shabaha na malengo ya Wizara hiyo kama ilivyo kwenye makadirio ya matumizi ya mwaka 2005/2006. Baada ya majadiliano ya kina Kamati imempongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Abdisalam Issa Khatibu, Mbunge na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. Mbunge wengine ni Makatibu Wakuu ndugu Grayson Ngonja na Ndugu Peniel M. Lyimo pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao mzuri waliotoa kwa Kamati katika kuteleza majukumu yao. Kamati haitamsahau Mama Blandina Nyoni Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa ushiriano wake mzuri na Kamati hii. Wizara ya Fedha ni Wizara kiungo muhimili ambayo ina majukumu ya kusimamia na kuendeleza uchumi imara kwa kubuni, kusimamia utekelezaji wa sera, ukusanyaji mapato na matumizi ya Serikali pamoja na kusimamia uratibu dhibiti wa mapato na matumizi ya Serikali pamoja na kusimamia uratibu, udhibiti wa mfumo wa Taarifa za kihasibu Kiserikalini. Aidha, Wizara ina jukumu pia la kusimamia vitega uchumi vya Serikali katika Makampuni na Mashirika ya Umma na kusimamia udhibiti wa deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu haya, Kamati imebaini kuwa Wizara imepata mafanikio katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali. Aidha, nchi yetu imeendelea kuwa na mahusiano mazuri na Wahisani, matumizi ya Umma na hivyo kufanikisha ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana 2004/2005 Kamati yetu ilitoa maagizo miwili kwa Wizara ya Fedha kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wizara kuendelea kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha za Serikali kupitia utaratibu wa *IFMS* **.**

Pili, Wizara iimarishe utendaji na uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu katika kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali kwenye ngazi zote, Wilaya mpaka Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata majibu ya kutosheleza juu ya utekelezaji wa maagizo yake kama ifuatavyo:-

Wizara ya Fedha inaendelea kudhibiti mianya au upotevu wa fedha kwa kuimarisha mtandao *IFMS*. Aidha, Wizara inatoa mafunzo ya *Accounting Manual* na *Internal Audit Manual* kwa watumishi wa Serikali pamoja na kuimarisha *Audit Trail*. Hata hivyo ni vyema ikaeleweka kuwa licha ya uimara wa ubora wa *IFMS* iwapo watumishi watakula njama bado upotevu utatokea, hivyo sambasamba na uimarishaji wa *IFIMS* masuala mengine kama maadili na vipato vya watumishi yanaboreshwa.

Wizara inaendesha mafunzo kwa Watendaji wa Kamati za Ukaguzi. Zoezi hili liendelee na inalenga kuleta uwajibikaji katika Serikali. Aidha, Wizara imeandaa kanuni za tozo ambazo zimeanza kutumika. Kanuni hizi zinalenga kuchukuliwa hatua na kupewa adhabu kwa Afisa yeyote anayekiuka Sheria na Taratibu za Fedha. Hapo awali kanuni kama hizi hazikuwepo na ni mategemeo ya Wizara kuwa kuwepo kwake kutakuwa changamoto kwa Watendaji kufuata utaratibu. Wizara inatoa miongozi na nyaraka kwa Maafisa Wahasibu na Watendaji wengine ikielezea namna ya kushughulikia masuala

mbalimbali ya udhibiti na usimamizi wa matumizi. Utaratibu huu unalenga kuimarisha utendaji na kuleta ubora katika taarifa kutoka *MDAs*.

Wizara vilevile imechukua hatua za kuwaunganisha Maafisa Wahasibu wote kwenye Mtandao wa *IFMS* ili kuwawezesha kupata taarifa mbalimbali haraka kila wanapohitaji. Kitendo hiki kinalenga kuimarisha ubora wa maamuzi wa Maafisa Wahasibu kutoka masuala ya fedha na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara ya Fedha imetekeleza kazi zifuatazo:-

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi;
- Kugharamikia udhamini wa wanafunzi *Pre-Service* 1500 kwenye Vyuo vya *TIA, IAA* na *IFM;*

- Kukamilisha ukarabati na kuweka vifaa katika jengo la Ofisi ya Idara ya Pensheni;

- Kuimarisha Vyuo vya *TIA, IAA* na *IFM* kwa ukarabati majengo na kununua vifaa mbalimbali;

- Kuimarisha utendaji na kununua *Computer* na vifaa vingine vya Ofisi kwa Idara mbalimbali;

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa *cadre* na fani mbalimbali;

- Kufanya majadiliano na Wahisani mbalimbali kuhusu misaada na mikopo ya nje;

- Kulipa mishahara ya watumishi wote wa Umma;

- Kuwalipa wastaafu 48,469 na kati yao 10,813 ni wastaafu waliokuwa wamechukua malipo yao ya mkupuo ambao marejesho katika *payroll* ya wastaafu kuanzia mwaka 2004/2005;

- Kuimarisha usimamizi wa matumizi na kutoa mafunzo ya *Audit Manual* kwa Wakaguzi wa ndani wa Wilaya, Mikoa na Idara za Serikali zinazojitegemea. Aidha, kutoa mwongozo wa kuunda Kamati ya Ukaguzi *Audit Committee* kwa Wizara, Mikoa na Idara za Serikali.

- Kuwasomesha watumishi wa *Cadre* ya Uhasibu 296 kati ya hao watumishi 138 ni kutoka Serikali za Mitaa ili kuboresha ufanisi wao wa kazi;

- Kutoa na kuendesha mafunzo kwa Wajumbe wote wa Kamati za Ukaguzi ili kuwapa uelewa na majukumu yao;

- Kutoa mafunzo ya matumizi ya mtandao kwa watumishi 96 wa Wizara na Idara za Serikali;

- Kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Umma ya ununuzi wa 2004 kwa wadau mbalimbali;

- Kuimarisha mtandao kati ya Hazina ndogo na Ofisi za Makatibu Tarafa Tawala wa Mikoa; na

- Kutayarisha taarifa ya kupambana na *UKIMWI* ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Mapato. Kamati imeridhika na Taarifa ya Wizara ambayo imeonyesha kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwezi iliyofikia zaidi ya malengo kwa kiasi cha asilimia 103 kwa mwezi. Kamati imetoa pongezi za dhati kwa Wizara na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA* ) Kamati inashauri kasi mpya ya ukusanyaji wa mapato ianzishwe na kuzingatia mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Mwaka 2004 na Sheria ya Manunuzi ya Bidhaa ya Huduma mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa matumizi ya Serikali ni muhimu katika kufanikisha maendeleo ya nchi. Kamati inaipongeza Wizara katika kuihusisha Kamati kushiriki utekelezaji wa azma hii baada ya kuanzisha utaratibu wa *Mid Year Budget Review.* Hata hivyo, Kamati inazidi kupongeza kuwa katika siku za usoni ili kuwe na uelewa mpana na Bajeti Kuu ya Serikali ni vyema Kamati ihusishwe katika hatua zote za maandalizi ya Bajeti ya Serikali na Bajeti za Wizara zote.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwepo kwa fedha za amana nyingi katika mabenki hapa nchini. Aidha, Taasisi hizo ni zile ambazo zipo chini ya Wizara ya Fedha hususan Mfuko wa Hifadhi za Jamii. Ni jambo zuri la kutunisha Mifuko ambayo hutumika katika kuwekeza katika majengo na amana za Serikali, lakini hali hii inainyima Jamii ya Watanzania walio wengi kutumia fedha hizi kwa kupatiwa mikopo midogo midogo na mikubwa ili kuwekeza katika shughuli za biashara na maendeleo hususan katika kutekeleza hatua za awali za MKUKUTA ili wananchi wapewe mikopo kwa masharti nafuu na waweze kuwekeza katika Sekta halisi za uzalishaji mali kwenye kilimo, viwanda, madini, uvuvi, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linaloambatana na suala hili la kuwepo fedha nyingi katika vyombo vya fedha ni kuwepo kwa fedha nyingi katika takribani zaidi ya bilioni 106 katika mabenki ya kigeni na haziingii katika mzunguko kiuchumi. Taarifa zilizopatikana ni kwamba baadhi ya Benki hizo zimeanza kutafuta wakopaji katika Maofisi mbalimbali ya Serikali na Mashirika ili waweze kukopa. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu kuweka mikakati na miongozo ili Benki hizi zipate wateja wengi kwa kutoa elimu na mikopo kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu la Wizara ni kusimamia mashirika, Bodi na Asasi zilizo chini yake na kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kama yalivyofanya kwenye sheria zilizoainisha Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 92 (iv) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004. Kazi za Kamati yangu ni kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji wa hesabu zilizokaguliwa za Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha, Kamati katika uhai wake ilipata fursa ya kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa hesabu zilizokaguliwa za Mashirika yote. Katika kufanya kazi hiyo, Kamati iliridhika na hali ya utendaji na ufanisi uliofikiwa na Mashirika hayo.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama yafuatayo:-

Mashirika yote yameendelea kuboresha utendaji na ufanisi kwa kuweka na kuandika taarifa za hesabu, utendaji na kuzingatia taratibu, misingi na kanuni za kiutendaji, kiutalaam na kiuhasibu. Aidha, hali ya utunzaji nyaraka, kumbukumbu kwa kutumia mtandao wa *Computer* umeimarika na hivyo kuyapatia sifa ya kupata Hati Safi za Ukaguzi.

Na kuwa na taarifa za wakati kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi wa Mashirika hayo, Wakurugenzi Watendaji Wakuu wote, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mashirika hayo kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Kamati inashauri, kwa yale Mashirika yaliyofanya vizuri zaidi ni vyema Viongozi wakatunukiwa wasifu kwa heshima nzuri kwa taswira ya kuyaongoza Mashirika yao kwa mafanikio yaliyopatikana. Aidha, Mashirika hayo yote yanaongozwa na Watanzania wenye sifa, maadili na moyo kujituma bila kuchoka.

Mheshimiwa Spika, naomba niyataje Mashirika hayo kama ifuatavyo:-

Benki Kuu ya Tanzania, Benki ya Raslimali Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Benki ya Posta, *Twiga Bank Corp.*, Mamlaka ya Mitaji ya Dhamana, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu, Shirika la Bima Tanzania, Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Uhasibu Arusha, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Bodi Kuu ya Tenda, *Unit Trust of Tanzania*, *Insurance Supervisory Department*, Raslimali *Limited, Gaming Board of Tanzania,* Tume ya Rais ya kurekebisha Sekta ya Umma, Chuo cha Mipango Dodoma, Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki, *Tanzania Investment Centre, Consolidated Holding Corporation*, Bodi ya Bima na Dhamana na *Loan Advances and Realisation Trust*. Haya ni Mashirika ambayo yamepata hati safi na tunaomba na Kamati nyingine ziige mfano wa Kamati hii kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala wa ulipaji wa mafao ya waliokuwa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki umekuwa ukitawala katika kila hoja inayoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Suala hili tuliwahi kulitolea maoni katika taarifa ya

Kamati hii mwaka jana 2004 na hata mwaka huu 2005 imejadiliwa tena katika ngazi ya Kamati. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kukamilisha zoezi la kulipa mafao ya wastaafu hao kabla ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na utekelezaji wa kazi za Wizara ya Fedha katika kuimarisha uwezo wa kusimamia ukuaji wa uchumi na kuimarisha ufanisi wa wafanyakazi wa Wizara hiyo kwa kutoa mafao yanayolenga katika kuongeza taaluma katika Sekta ya Fedha, kurekebisha na kuboresha mifumo ya kukusanya kodi na ushuru kwa nia ya kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza shughuli zake, Wizara ya Fedha inaomba fedha kama ifuatavyo:-

Fungu – 50 Sh.243,294,291,700/= ni matumizi ya kawaida na Sh.21,406,260,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Fungu 23 Sh.85,898,872,300/= ni matumizi ya kawaida na Sh.7,773,889,200/= ni miradi ya maendeleo.

Fungu 22 Sh. 523,234,528,000/= ni deni la Taifa.

Fungu – 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Sh.8,147,420,200/= ni matumizi ya kawaida na Sh.1,521,000,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Bunge hili liidhinishe maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii tena nimshukuru Waziri Mheshimiwa Basil Mramba Mbunge, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Makatibu Wakuu, watalaam wote kutoka Idara na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha jinsi walivyotusaidia Kamati kufanya kazi zake kwa maendeleo na ufafanuzi kwa kujibu hoja zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii niwapongeze kwa dhati kabisa Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa michango, maoni kwa kufanya kazi zote za Kamati bila kuchoka. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina yao mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Njelu M. Kasaka Mbunge – Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy Gembe – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Elias Mollel, Mheshimiwa Idd Simba, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Abdulatif Ismail, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Issa Salim na Mheshimiwa Rostam Aziz. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kabisa nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kutoa miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza kabisa Katibu wa Bunge - Ndugu Damian Foka na Ndugu James Warburg - Katibu wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kuiwezesha kuipa Kamati yetu nyenzo katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nachukua nafasi hii kwa kuwa ni mara yangu ya mwisho kusimama katika Bunge hili la muda wa miaka mitano, niwashukuru sana wanawake wa Wilaya ya Ukerewe, Wilaya ya Sengerema, Wilaya ya Geita, Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Misungwi, Wilaya ya Magu, Wilaya ya Ilemela na Wilaya ya Nyamagana kwa kuomba tena tarehe 7 mwezi 8 nitasimama tena kuomba kura ili waweze kunirudisha tena Bungeni nikishirikiana na Wabunge wenzangu tunaomaliza nao mwaka huu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Anne Makinda - Mwenyekiti wetu wa Wabunge wanawake Bungeni hapa, ametuwezesha kutupa semina na kutufundisha *computer.* Mimi hapa sasa naweza nikafanya kazi zangu vizuri tu. Ninaomba wananchi wa Jimbo la Njombe mumrudishe mama yetu ili tuendelea kuwa naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanangu watatu, Dorica Nyawazwa, Alex Nyawazwa na Naomi Nyawazwa kwa kunivumilia kwa muda wa miaka mitano, muda mwingi nimekuwa nikiwahudumia akina mama wa Mkoa wa Mwanza wameweza kunivumilia. *(Makofi)*

La mwisho, naomba niwatakie kheri Wabunge wenzangu na nina uhakika kwamba mtarudi kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nikupe salam kutoka vijana wa CCM wa Mkoa wa Mwanza wako kwenye Kambi kule Bukoli Geita wanamtakia kheri sana Mheshimiwa Kikwete kwamba wana uhakika atashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya

Upinzani naomba mpokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (b) (c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wakuu wa Vitengo na asasi zilizo chini yao, wote tunawapongeza kwa kuratibu ukusanyaji wa mapato hadi nchi yetu kuweza kujijengea sifa ya kuwa pahala pazuri pa kuwekeza katika raslimali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ni Wizara yenye jukumu kubwa la kuhakikisha mapato ya Serikali yanapatikana na kusimamia matumizi yake. Katika kutekeleza majukumu yake hayo Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu 153 kimeanzisha akaunti ya fedha ya pamoja ya Jamhuri ya Muungano ambayo pia imo katika Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu: "Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambapo kutawekwa fedha yote itakayochangiwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja ya fedha kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano."

Aidha, Serikali imepitisha sheria ya kuanzishwa kwa Tume hiyo ya pamoja na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuipongeza Tume hiyo kwa kazi nzuri iliyoanza kuifanya kwanza kujua matatizo tuliyonayo, kujifunza kutoka kwa wenzetu namna tunavyoweza kutumia uzoefu wao katika kupata *formula* nzuri ya kukusanya na kugawana mapato na namna bora tunayoweza kutatua migogoro yetu katika mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu aliahidi kuwa angeyamaliza matatizo ya Muungano katika kipindi cha miezi sita mara tu baada ya kuchaguliwa tena mwaka 2000 lakini pamoja na nia yake nzuri haikuwezekana na mbaya zaidi imekuwa hata mambo ambayo yangeweza kusaidia katika uchumi wetu kama vile mafuta kwa upande wa Zanzibar hadi leo imeshindikana kutafutiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa Tume ya Mheshimiwa Shellukindo imejifunza vya kutosha na hasa itaanza kutekeleza kwa vitendo vile vifungu vya Katiba nilivyotangulia kuvisema kuwa wapo wanaodai kuwa mafuta siyo jambo la Muungano kwamba liliingizwa kinyemela ndani ya Katiba halikuwahi kupitishwa ndani ya Bunge hili.

Wapo wanaodai kuwa kama mafuta ni ya Muungano mbona *Gas* nayo ni ya Muungano, lakini Zanzibar haikushirikishwa wala kujulishwa wakati wa utafutaji, uchimbaji na hata kwa matumizi yake?

Wapo wanaodai kuwa *TPDC* siyo chombo cha Muungano, ni vipi kisimamie *gas* na mafuta ambavyo ni vya Muungano na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, pia yapo malalamiko juu ya uajiri wa baadhi ya vyombo vya Muungano kama vile *BOT* ambapo kati ya Wakurugenzi 18 na Manaibu 47 hakuna Mtanzania mwenye asili ya Zanzibar hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, mifano ya aina hii ni mingi kwa kuwa wenzetu katika kipindi cha miaka 40 wameshindwa kuyatatua. Kambi ya Upinzani kwa kuweka maslahi ya Taifa mbele mara ipatapo ridhaa ya Watanzania itahakikisha kuwa:-

Kwanza, vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Zanzibar ambavyo vinazungumzia Tume ya Pamoja ya Fedha vinatekelezwa kikamilifu katika mwaka wa kwanza wa bajeti.

Pili, masuala yote ye Muungano ambayo yanaleta manung'uniko yatajadiliwa kwa uwazi na upana ili ufumbuzi upatikane bila ya kuchelewesha maendeleo ya Taifa.

Tatu, katika kutekeleza hilo la A na B hapo juu maslahi ya Taifa na Umoja wetu ndiyo msingi mkuu wa masuala ya maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutumia fursa hii kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri iliyofanya ya kukusanya mapato na kuzidi lengo kwa asilimia 103. Huu ni mwanzo mzuri hauna budi kuendelezwa kwa madhumuni ya kuwa na ufanisi zaidi na hasa katika kumtoa Mtanzania katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya mapato yanatokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani *VAT* ambayo ni asilimia 20 hivi sasa na kodi za Ushuru wa Forodha na bidhaa zinazozalishwa nchini. Kwa mfano *VAT* imechangia karibu Shilingi bilioni 71, Ushuru wa Forodha Shilingi bilioni 42, bidhaa za ndani Shilingi bilioni 28, Kodi ya Mapato Shilingi bilioni 43, Kodi nyingine Shilingi bilioni14, Mapato ya *Income Tax* Shilingi bilioni 16, mapato yanayotokana na ubinafsishaji katika Taarifa ya Hali ya Uchumi inaonyesha katika kipindi cha miaka miwili 2003/2004 na 2004/2005 hakuna mapato yaliyopatikana. Pamoja na kwamba yapo Mashirika yaliyouzwa, wanunuzi hawajamaliza madeni yao, mfano ni Mgololo Kiwanda cha Karatasi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa urari wa kibiashara una naksi kubwa; je, Serikali haioni kuwa kuingia kwa bidhaa nyingi kutoka nje pamoja na kuongezeka kwa mapato kunaua nguvu za uzalishaji wa viwanda vyetu?

Mbili, Kwa kuwa Ongezeko la Thamani (*VAT)* ni kubwa kuliko nchi jirani si tunapunguza nguvu za ushindani katika biashara?

Tatu, si tunawapunguzia uwezo wa kununua watu wetu hasa tukitilia maanani kuwa watu wetu bado wako katika dimbwi la umaskini wa kipato cha chini ya Dola moja kwa siku hivyo kuzifanya bidhaa zetu tushindwe kuziuza nje na ndani, matokeo yake bidhaa za nje zinakuwa na soko zaidi kwa sababu ni rahisi?

Nne, kwa kuwa bado usumbufu na msururu wa mambo yanayohitajika katika kutoa mizigo hapa kwetu inachukua muda si chini ya siku 10, siku utapunguza mapato na kuongeza ughali wa bidhaa na kufanya uchumi kuwa ghali kwa vile muda unaotumika katika kutoa bidhaa bandarini ni mwingi mno?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maswali haya ni marudio katika kipindi hiki cha Bunge lako, Kambi ya Upinzani inawashauri Watanzania wawape ridhaa yao ili tupunguze kiwango cha *VAT* kiwe na uwiano wa washiriki wenzetu wa Kenya kisizidi asilimia 17.

Pili, tuzidi kupunguza kodi katika Sekta za Uzalishaji hawa viwandani ili kuweza kuuza bidhaa zetu nyingi nje na kuwawezesha watu wetu kumudu kununua badala ya kununua mitumba ya *TV*, *Video*, nguo, magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kubuni utaratibu wa kutumia mtandao wa *IT* kwa kutoa mizigo kama vile vinavyofanya Singapore ili kuokoa muda, usumbufu na pia kupunguza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia utaratibu wa *Cash Budget* Serikali imejitahidi kubana matumizi. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, tunaomba kumpongeza Mlipaji Mkuu wa Serikali yaani *Pay Master General* na Wasaidizi wake wote na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kusimamia vyema matumizi ya Serikali pamoja na mapungufu fulani kama yafuatayo:-

Kwa kuwa, kiwango kidogo cha kima cha chini cha mshahara, hakuna sababu ya kima cha chini kisiwe angalau Sh.100,000/= wakati fungu la 50 linalosimamiwa na Wizara hii mishahara katika kipindi cha miaka mitatu ni kama ifuatavyo:-

Mishahara ilikuwa 913 milioni wakati marupurupu ni Shilingi bilioni 2.6, mwaka 2004/2005 mishahara ni bilioni 1.3 na marupurupu ni Shilingi bilioni 3.6, mwaka 2005/2006 inakisiwa mishahara ni bilioni 1.4 wakati marupurupu ni bilioni 6.9.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali ishindwe kupandisha kima au inaogopa kulipa kiinua mgongo kikubwa pamoja na kwamba itakapolipa mishahara mikubwa itakuwa na uwezo wa kupata kodi ya uhakika kutoka kwa wafanyakazi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutumia utaratibu wa *Cash Budget* lakini Serikali imeendelea kuwakopa wafanyakazi hasa Walimu, Wakunga na Askari wa chini ambao hata mafao yao ya likizo, *Operation* wakati mwingine huhamishiwa kwenye miradi ya maendeleo kinyume na utaratibu bila hata kulipwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote duniani ndiyo tajiri mkuu katika nchi, ndiyo mkusanyaji mkuu wa mapato na ndiyo mtumiaji mkuu. Sehemu moja kuu ya matumizi ya Serikali ni katika utoaji wa huduma na ujenzi wa miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo hili ndilo linaloiwezesha Serikali kuwa na utawala mzuri au mbaya. Hivyo hata rushwa hapa ndipo penye mbolea yake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kutokana na udhaifu wa kununua huduma na vifaa na udhaifu katika kusimamia mali za Serikali manunuzi hewa yalikuwa Shilingi bilioni nane. Manunuzi ya bila idhini ya *Central Tender Board billion 4.3* na vifaa visivyoingizwa katika vitabu na kupatiwa udhibitisho bilioni 8.8.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona ipo haja ya kurekebisha kasoro hizi kwa:-

- Kuunda Idara maalum itakayokuwa na wataalam, uzoefu, kusimamia na kufuatilia mali za Serikali;

- Kuimarisha ukaguzi wa ndani; na

- Kuwa wazi wakati wa kuuza mali za Serikali hasa hisa.

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kama tulivyowahi kuambiwa hapa Bungeni kuwa kama kuna mbia ni lazima kwanza umuuzie yeye hizo hisa ndiyo unafanya hivyo baada ya kupata *market value* na siyo kama ile ya kuuziwa *Celtel International Cell Tanzania* au hisa 25 za Serikali kuuziwa *Williamson* kwa Dola 180,000/=.

Kulishirikisha Bunge katika kuuza mali za Serikali kwa niaba ya wananchi katika ngazi zote siyo kama walivyonyang'anywa *TPDC* jengo lao kinyemela.

Kuwa na Wahasibu na maboharia wenye ujuzi na kulipwa vizuri ili iweze kuweka kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikosa mapato kutokana na yenyewe kutokuheshimu Sheria ya Manunuzi *Procurement Act* hivyo kuingilia Taasisi Zabuni bila kufuata taratibu. Ipo mifano mingi Zabuni ya Vitambulisho vya uraia, Zabuni ya Mchele kutoka Japan, Zabuni ya kuweka Mtandao Serikali za Mitaa Kampuni iliyoshinda *Micronix* imeenguliwa na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, waathirika huamua kwenda Mahakamani hatimaye Serikali hulazimika kulipa fidia na gharama za Mahakama. Eneo moja ambalo Serikali ingeweza kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi yasiyoipatia faida Serikali *Nugatory Expenditure* ni kwenye Zabuni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Serikali ililipa malipo katika mafungu mbalimbali jumla ya Shilingi bilioni 2.4 na Dola 104,000/= ambayo hayakuisaidia chochote Serikali zaidi ya kuiingizia hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili kwa kupitia Kamati ya Hesabu za Serikali ilishauri tutumie utaratibu wa *Electronic Procurement* ambao utapunguza urasimu,

rushwa, utatoa ushindani wa wazi hivyo kuongeza ufanisi, utaipunguzia gharama ya manunuzi ya Serikali si chini ya asilimia 15 ya manunuzi, hivyo kuiongezea uwezo wa Serikali wa kutoa huduma zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote hizo bado Serikali haijachukulia hatua jambo hili. Hivyo Kambi ya Upinzani inawaahidi Watanzania pindi mkiwapa ridhaa yenu itaanzisha utaratibu huu ili kupata manufaa tuliyoyaeleza hapo juu na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hazina ndiyo msimamizi mkuu wa raslimali za Serikali pamoja na Mashirika ya Umma. Aidha, ndiye Msimamizi Mkuu wa Hisa zilizoko kwenye Mashirika binafsi. Wakati wa uchumi hodhi, kitengo hiki kilikuwa na watumishi wachache sana. Watumishi hao ndio waliokuwa wakihudhuria Vikao vyote vya Bodi kwa niaba ya mwenye hisa yaani Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huu wa uchumi huria ni dhahiri tunahitaji Idara kamili yenye wataalam na uzoefu wa mambo ya kibiashara, vinginevyo tunachezewa mchezo wa karata tatu kama *Williamson Diamond*, *TVT* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiuza mali za Watanzania bila kujali kuwa mali ni za walipa kodi Watanzania wote, hivyo wanahitaji washirikishwe. Wawakilishi wa Watanzania ni Wabunge wao, hivyo mauzo yao yote ya raslimali za nchi ni lazima Bunge lishirikishwe kikamilifu katika hatua zote.

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia *ATC* inavyokufa hata zile nyumba za Masaki ameuziwa mgeni badala ya wafanyakazi. Naamini ifikapo mwaka 2006 *ATC* tutaizika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kufuatilia hisa zake zilizopo ndani ya Mashirika mbalimbali na hasa ya binafsi ndiyo maana imeshindikana kupata gawiwo katika *Williamson Diamond* toka mwaka 1996 hadi leo hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kamati ninayoingoza ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kumshukuru Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu, Bwana Thomas Kiama na Wasaidizi wake, kwa kuisaidia Kamati katika kutimiza wajibu wake uliokabidhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuwa na muda mfupi sana wa kufanya shughuli zake kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameweza kusaidiana na Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati yetu Bwana Anslem Mrema kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, kutokana na idhini yako, Kamati imeweza kuwa mwenyeji wa Mikutano miwili ya *Southern African Development Organization, Public Accounts Committee* mmoja uliofanyika Bagamoyo na wa pili Zanzibar ambapo nchi yetu imekuwa imepewa hadhi ya kuwa *Secretariate* katika kipindi cha miaka mitatu. *(Makofi)*

Aidha, wameruhusu pia kufanyika Mkutano wa *Workshop* wa *Eastern African Public Accounts Committee (EAAPAC)* pamoja na *SADCOPAC* mwezi huu tarehe 22 – 26/07/2005 hapo Kunduchi Dar es Salaam kwa madhumuni ya kutafuta njia ya kuvioanisha vyombo hivi viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kamati ya *PAC* nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wadhibiti na Wakaguzi Wakuu wa Hesabu za Serikali wa Serikali ya Muungano wa Zanzibar kwa kufanikisha Mikutano hiyo. Shukrani za pekee ziwaendee Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha ya Muungano kwa kufanikisha Vikao vyote hivyo nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, naomba mambo ambayo ni muhimu kuyazingatia katika kuangalia namna bora ya Kamati hizo kufanya kazi zake kwa ufanisi ni kama ifuatavyo:-

(1) Kwa Wakaguzi na Wadhibiti Wakuu walete taarifa zao moja kwa moja Bungeni badala ya kupitia kwa utawala yaani *Executive;*

(2) Kamati ya *PAC* ipewe muda ziada wa kufanya shughuli zake pamoja na rasilimali watu na fedha;

(3) Utaratibu wa *Auditing* ubadilishwe uwe asilimia 40 ya *Financial Auditing* na asilimia 60 *performance auditing*;

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unaweza ukaona watu wanapata *Clean Certificate* lakini hali halisi huko ndani ni nyingine; *(Makofi)*

(4) Wenye nia na haja ya kusikia mwenendo wa mahojiano ya Kamati na Maafisa Wahasibu yaani *medium* na *Stakeholders* waruhusiwe kuingia kwenye vikao hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki limekuwa kama donda ndugu. Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba ameomba hili suala lisigeuzwe kuwa la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliane naye, lakini ni vizuri tukajiuliza hivi ni nani aliyeligeuza kuwa la kisiasa? Ni Serikali iliyokuwa haiheshimu makubaliano au wastaafu wanaodai haki zao kwa kutumia Vikao, Waandishi wa Habari na Wawakilishi

wao,yaani Wabunge? Mbona wastaafu wa Kenya na Uganda hawakupata matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kulipwa mafao yao wastaafu tarehe mosi Mei, 2005 naye alisema: "Kipaumbele changu hivi sasa ni kuhakikisha kuwa tunatenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka 2005/2006 ili kama nilivyosema, tuanze kulipa japo kwa awamu kabla sijaondoka madarakani. Nisingependa mzigo huu nimrithishe Rais ajaye. Narudia, hesabu za awali zinazoendelea kuhakikiwa na kujadiliwa zinaonyesha kuwa deni ni kubwa na linaloweza hata kufikia Shilingi bilioni 400 kuzilipa zote kwa mkupuo ni sawa na kusema tusimamishe shughuli nyingine za Serikali.

Hivyo basi, nimeagiza kuwa baada ya madai kuhakikiwa na kukubaliwa Kamati ya Taifa ya Kudhibiti Madeni iandae utaratibu wa malipo na kumshauri Waziri wa Fedha juu ya utekelezaji wake. Lakini nawapeni ahadi yangu kwamba tutaanza kulipa kabla ya sijaondoka madarakani ili mradi tuafikiane na wastaafu juu ya viwango na utaratibu wa kulipa tutakaopendekeza." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango sahihi cha malipo yao ni kiasi gani baada ya kuhakikiwa ambapo kabla ya hapo Mheshimiwa Rais alisema inafikia Shilingi bilioni 400. Ni wangapi wanaostahili kulipwa? Itachukua muda gani kulipwa? Wale waliokuwa wamekwishafariki utaratibu wa kupata haki zao utakuwaje? Ni vigezo gani vinavyotumika katika kutoa hayo mafao kwa kutambua *currency* iliyokuwa ikitumia wakati huo? Wapo waliopo kazini hivi sasa; je, na wao watalipwa na kama hawatalipwa ni kwa nini Mikataba yao ni tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni maswali ambayo kama Serikali itashindwa kutoa maelezo basi hiyo ni dhahiri Serikali haina nia ya kuwalipa kama alivyoainisha aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa barua yake PMC/C.350/1 ya tarehe 11 Novemba, 1991 ambayo ilikataa kabisa kutambua madai ya wastaafu hao. Wangoje Serikali ya Kambi ya Upinzani itakapoingia madarakani tutawalipa haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga katika bajeti fedha zinazochangia kwa watumishi kama pensheni na *welfare scheme* katika bajeti ya 2003/2004 ilitenga Shilingi milioni 717,000 na kwa bajeti ya 2004/2005 ilitenga Shilingi milioni 1,917,496. Katika bajeti ya mwaka huu 2005/2006 hakuna fungu lililotengwa; je, imesahauliwa? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa hili, kwani watumishi wanafikisha muda wao wa kustaafu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii adhimu nimshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kupendekeza jina langu kwa Chama changu ili aniteue kuwa Mbunge mara tu baada ya muafaka. Hatimaye akaniteua kuwa Mbunge namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa yeye na Rais na Chama changu kunipa fursa hii, nimeweza kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara mbili kubwa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mipango na Ubinafsishaji. Aidha, nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali na Katibu Mkuu wa *SADCOPAC* na *EAAPAC*. Nawashukuru sana, kwa imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Kambi yangu ya Upinzani kwa imani kubwa walionayo juu yangu, wameuthamini mchango wangu mdogo nilioutoa katika Kambi, wamevumilia udhaifu wangu na hawakusita kunishauri na kunielekeza hasa Kiongozi wetu Mkuu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwashukuru Kamati yangu ya *PAC* hasa Makamu Mwenyekiti Profesa David Mwakyusa - Mbunge kwa kuviendesha Vikao pale ambapo nilipata dharura bila matatizo. Aidha, Wajumbe wote wa Kamati nao wamefanya kazi kwa kujituma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya *PAC* na *SADC* na *EAAPAC* walikuwa wananiuliza, hivi unawezaje kuendesha Kikao chenye Wajumbe asilimia 96 kutoka Chama kinachotawala? Jibu langu lilikuwa rahisi. Niliwaeleza kuwa sisi tuliingia katika mazungumzo ya kutafuta muafaka baina ya CCM na *CUF* na tukafikia muafaka huo baada ya kuweka maslahi ya Taifa mbele badala ya kuweka itikadi zetu mbele. Ni falsafa hiyo hiyo ndiyo inayotuongoza katika kuendesha Vikao vyetu vya *PAC* na ndiyo itakayotumika katika kuunda Serikali ya pamoja pindi tukipata ridhaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa sote tutampa zawadi Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ya kufanya uchaguzi ulio huru na haki na amani na Bunge lijalo liwe la kutanguliza maslahi ya Taifa na siyo itikadi zetu za Vyama. Hivyo, naamini itakuwa ni zawadi nono kwa Mheshimiwa Rais wetu kwani atapata nafasi ya kupumzika huku akiwa na matumaini ya kuendelezwa yale mazuri aliyoyaacha na kubuniwa mapya kwa mwelekeo wa kujenga umoja wa Kitaifa na kwa maslahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwombea afya njema Mheshimiwa Rais wetu yeye na familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wananchi wa Wawi kwa kunipokea, kuwa mgombea mteule wa Chama chetu katika nafasi ya Ubunge wa Jamhuri. Naahidi pindi nikipata ridhaa yao nitafanya kazi kwa karibu nao sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niwashukuru wanachama wenzangu wa Chama changu cha *CUF* na kuwaomba popote walipo tujitahidi kuendeleza na kuitunza na kuenzi amani na utulivu wa nchi yetu tusichokozeke hata kidogo, tuheshimu sheria na taratibu za nchi ili tuwe Walimu kwa wanaofanya kinyume na hayo. Mungu ibariki Tanzania!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hatua ya awali kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili niweze kutoa pole na rambirambi kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Iringa kwa ndugu, familia na wananchi wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na pia Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimesimama hasa kwa ajili ya kutoa ushauri. Naomba na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana na tena sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja Wasaidizi wake pamoja na Makatibu Wakuu na Wasaidizi wao pamoja na Wakurugenzi wao wote bila kumsahau Ndugu Blandina Nyoni kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuendesha shughuli za Wizara ya Fedha.

Pia, niungane na Mwenyekiti wa Kamati iliyojadili Wizara hii Kamati ya Fedha na Uchumi kuweza kuunga mkono kwamba hakika Asasi na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Fedha zimefanya kazi kubwa sana katika kipindi hiki na kwa maana hiyo basi, wapewe pongezi hata kwa kupelekewa barua ya kupewa shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameonyesha kwamba hakika Wizara ya Fedha katika kipindi hiki imekuwa na mafanikio makubwa sana na nisingependa kuyataja kwa sababu ya muda. Lakini niseme tu mafanikio hayo ambayo hasa yametokana na kuweza kusimamia vizuri makusanyo ya mapato na pia kusimamia matumizi kiasi kwamba Wizara hii imeweza kupata albaki ambayo imeweza kusaidia katika mambo mengine ambayo tunayaona kama kulipa wastaafu wa *East African Community* yameweza kufanyika na pia kulipa malimbikizo kama tulivyoambiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba malimbikizo ya Shilingi bilioni 18.4 yameweza kulipwa kwa Walimu na pia kwa watumishi wengine. Hakika wananchi wanafurahi sana na wanaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba imeweza kufanya kazi kubwa ambayo inawajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijikite kwenye upande wa huduma hii kwa wastaafu. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kutueleza kwamba wastaafu wameishalipwa kama alivyosema kati ya 14,000 waliokuwa wanadai, wamelipwa 10,000 na wengine 3,000 wako katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa, sasa naomba niseme hao 3,000

ni akina nani? Je, inawezekana wakalipwa hivi karibuni? Inawezekana wakalipwa lakini kama tulivyosikia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu swali katika wiki mbili zilizopita kwamba matatizo makubwa ambayo yanasababisha wastaafu wasilipwe ni ukosefu wa nyaraka. Hili hakika ni tatizo kubwa sana ambalo lipo katika Idara hiyo ya Pensheni ambapo pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri sana ambayo inastahili pongezi, lakini kwa sababu hakuna baadhi ya nyaraka, wameshindwa kulipa baadhi ya wafanyakazi waliostaafu.

Mheshimiwa Spika, naweza nikaelezea mambo mengi sana kulielezea tatizo hili ambalo wananchi wamekuwa wakililalamikia na linakuwa ni dosari kubwa kwa utendaji mzuri uliofanyika katika Wizara ya Fedha. Naweza nikalielezea kwa kitabu kizima labda chenye kurasa 100. Lakini naomba tu nitoe mfano kwamba ni kitu gani ninachotaka kusema. Tatizo ambalo lililopo katika Idara hii ya Pensheni linatokana na ukosefu wa nyaraka.

Mimi nimekuwa nikienda mara kwa mara pale Wizara ya Fedha na nimekuwa nikipeleka barua mbalimbali ambazo zinahusu madai hayo. Lakini zinashindikana kushughulikiwa kwa sababu mafaili hayaonekani na mafaili inawezekana yasionekane kwa sababu aidha pengine mfanyakazi alifanya kazi katika sehemu mbili tofauti au tatu katika Wizara. Inawezekana alikuwa Iringa, alikuwa Morogoro, alikuwa Rukwa huko, sasa kukusanya yale mafaili yakakaa katika sehemu moja inakuwa ni vigumu au zile taratibu kwamba lazima kuwepo na barua ya ajira na barua ya kuthibitishwa kazini katika faili lake zinakuwa mara nyingine hakuna.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa wale waliofariki, inawezekana cheti cha kifo hakipo katika faili na barua ile ikishaandikwa ikarudishwa kwa yule Mwajiri kwamba alete sasa vile vitu, basi inachukua muda mrefu sana na kwa kweli miaka inakwenda na wananchi wamekuwa wakilalamika kwa maana wajane wamekuwa wakihangaika, watoto yatima wamekuwa wakihangaika kwa sababu haki zao zinakuwa hazilipwi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nionyeshe mfano kwamba ni kitu gani nataka kusema. Kwa mfano hapa nina barua ya Ndugu Dick Simon Mgeni, ambaye ni wa Iringa anadai malipo yake ya kiinua mgongo toka mwaka 2004 mwezi wa Aprili, lakini mpaka leo hajaweza kulipwa kwa sababu faili lake nimefuatilia mara nyingi halionekani. Kuna malipo ya Marehemu Shella Mayagila huyu yupo Ualimu na huko faili halijafika kwa sababu faili lake halipatikani. Kuna mirathi ya Marehemu Martina Ngagisi nayo hii ipo Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa sababu faili lake halionekani. Mirathi ya marehemu Modestus Lupembe na hii toka mwaka 2004 nayo faili halionekani.

Mheshimiwa Spika, nina madai ya Marehemu Ernest Mwanga nayo hii kutoka mwaka 2002 hakuna kinachoonekana. Kuna mzee wangu mmoja anaitwa Cosmas Mtakimwa ameniletea barua anasema hebu fuatilia barua zangu kule Hazina kuhusu kupunjwa kwa fedha za pensheni kwa mwaka 1999 na mwaka 2000 faili lake pia halionekani. Kuna Pyelina Ngimba naye kutoka mwaka 2003 faili lake halionekani. Kuna Wanajeshi wengi ambao hawajalipwa kwa sababu tu mafaili yao hayaonekani.

Sasa kuna barua moja hapa anasema nilistaafu mwaka 1993 lakini nashangaa kuambiwa faili langu halionekani mpaka sasa sijapata fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini nilieleze shida tunazozipata sisi Waheshimiwa Wabunge tunapopewa kushughulikia matatizo ya hao watu ambao wamestaafu au wamefariki, nini wanadhani kwamba pengine sisi hatushughulikii inavyopaswa. Anakupa barua unapeleka hata ukifuatilia, unaweza ukaenda mara ya kwanza na ya pili na hata mara tatu au hata mara tano sasa huelewi imeshafikia hatua gani na iko kwa nani. Kwa maana hiyo basi, unabaki unakaa kimya lakini ukitegemea kwamba itajibiwa barua ile ili mtu yule aweze kupata majibu lakini barua ile haijibiwi na malipo yake hayalipwi. Kwa maana hiyo lawama zinakuja kwa wewe Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nisome barua moja ya mzee mmoja anaitwa Mzee Huliani Larika, anasema: "Barua zangu nilizokukabidhi Dodoma mwaka 1996 na mwaka 1998 hayo yalikuwa ni madai ya pensheni pia. Anasema hivi, kudhulumu mtu haki yake wakati watetezi mpo mnaona ni haki! Ananilaumu mimi. Anasema ninaomba majibu, Waziri alisemaje? "Daima mwenye kushiba hamjui mwenye njaa." Sasa barua kama hii unaletewa wewe Mbunge ambaye unapewa lawama kwamba vitu kama hivi haviendi. Lakini ni kwa sababu *document* hazionekani. Sasa nilikuwa nataka kutoa ushauri kifanyike kitu gani ili kuhakikisha kwamba matatizo kama haya yanapungua.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ambavyo ameisimamia sana Wizara hii na kuchukua maamuzi makubwa yaliyowezesha kufanikiwa mafanikio makubwa kama tunavyoyaona sasa hivi, achukue uamuzi ule ule wa kufanya operesheni nyingine. Operesheni hiyo itakayohusisha wafanyakazi wake watakaokwenda Mikoani kwenda kukutana na hao wote wanaodai malipo hayo wasikilize matatizo yao yanatokana na nini na kwa nini hawalipwi na itokee *cut off date* kwa mfano tunaweza kusema kwamba kuishia mwaka 2000 na kurudi huko nyuma hao wote *document* zao hazipatikani. Ichukulie hatua maalum ya kuweza kupunguza baadhi ya taratibu na sheria zinazohusu malipo ya pensheni ili hao watu waweze kulipwa. Ninaomba sana maana yake bila hivyo wajane, watoto yatima na wengine wataendelea kusikitika sana na kwa maana hiyo wanailaumu Serikali yao wakati imeshafanya mambo mazuri sana ambayo yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba niombe kama maombi mawili mengine. Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakumbuka nimekuwa nikifuatilia tatizo la wafanyakazi iliyokuwa *TANCUT* Iringa mpaka sasa hivi hawajalipwa mafao yao. Ni kwamba walichoathirika nacho ni Sheria ya mwaka 1952 ambayo inasema kwamba Shirika likishafilisika wanatakiwa walipwe Sh.4,000/=. Sasa mimi naomba tu kwamba hizo Sh. 4,000/= za mwaka 1952 basi igeuzwa sasa ionekane ni kiasi gani ili hao wafanyakazi waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna ombi la wafanyakazi ambao ni wastaafu kuhusu Mfuko huu wa Umoja *Fund* kwamba mwisho wa kununua vipande ni tarehe 29 Julai, 2005. Wafanyakazi waliostaafu kwa sababu wanapata fedha katika kipindi cha miezi sita, wanaomba uongezwe muda wa kununua vipande hivyo. Lakini pia hili lilikuwa ni

ombi lililotolewa katika Mkutano wa mwaka *ALAT* uliofanyika tarehe 17 Juni, 2005 kule Mbeya na mimi nikiwa Mjumbe wa Mkutano huo ambapo walitoa Azimio kuomba muda uongezwe ili wananchi wengi waweze kununua vipande hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine naomba Serikali itueleze kwamba hao *expertise* ambao wanafanya kazi chini ya Mashirika ya Dini kuna Mikoa mingine wamekuwa wakilipishwa kodi kutokana na mishahara wanayoipata na mishahara hiyo hailipwi hapa nchini inalipwa huko nje kwa maana ya wale Wafadhili ambao wanakuwa wanafadhili ile miradi. Je, wanatakiwa kulipa kodi hapa kwetu na wakati kule kwao wanalipa? Maana kwenye Mikoa mingine wanalipa na katika Mikoa mingine hawatakiwi kulipa. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru Serikali kwamba imetoa Shilingi bilioni nne kwa ajili ya Bima ili iweze kulipa wale wanaodai upande wa Bima. Kwa sababu nayo imekuwa ni kero kubwa sana ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukionekana kama vile tunaficha labda barua zao na nini kwa sababu Bima imekuwa ikikosa fedha za kuwalipa. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe kwa kutusimamia vizuri katika Bunge lako Tukufu na ninakuombea mwakani pia uweze kuchaguliwa kuwa Spika na ninawatakia kila la kheri Waheshimiwa Wabunge waweze kurudi na mimi ninawaambia wananchi wa Manispaa ya Iringa nitagombea tena kwa hiyo, naomba wanichague tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya Fedha. Kwanza, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha kwa asilimia mia moja kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Basil Mramba amefanya kazi kwa nguvu na sisi tumeona juhudi na jitihada ambazo kwa kipindi hiki ambacho amekuwa Waziri wa Fedha ameonyesha mabadiliko makubwa ambayo yanaleta matumaini kwa nchi yetu ya Tanzania aendelee namna hiyo. Sasa sijui Rais ajaye kama atamwona kwamba aendelee kwenye Wizara ya Fedha, hiyo sijui. Lakini mimi nampa kura yangu aendelee kuwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe tu kwamba katika mchango wangu nina mambo mawili tu ambayo yanaonekana kwamba kuna kero licha ya kwamba kero nyingi wameziondoa, kodi mbalimbali zimeondolewa ili kuleta unafuu kwa wakulima na wafanyakazi, lakini bado kundi la wakulima na kundi la vijana. Vijiwe vya vijana vimekuwa ni vingi kweli na vinatia hofu na mashaka, yaani sasa hivi tunatembea kwa woga kutokana na hivyo vijiwe vya vijana wenye umri wa miaka 12 kwenda mpaka miaka 25 ni wengi na hawana mahali pa kwenda na hakuna wazo au mkakati wa makusudi wa kuweza kuwaangalia kwa kina vijana hao.

Mheshimiwa Spika, vijiwe vya vijana ni vingi mno, kwa hiyo, tunaomba jitihada za makusudi za vyombo vya fedha kama mabenki kuwepo na mawasiliano ya wazi ili tuweze kupunguza kasi za ajira kwa hao vijana ambao wengi wao hawawezi kuwa na ajira nyingine bali zile za kujitegemea. Kama ni vikundi vya kilimo wapewe mikopo. Hiyo mikopo ya vijana bado ni kidogo sana inaonekana kama ni *tone* ndani ya bahari. Uchukue ndoo ya maji uweke kwenye Bahari ya Hindi wala haileti gharika wala ile gharika ya Nuhu hawezi kusikika hapo. Tunaomba kabisa, ukitazama Tanzania tu au kama ndiyo wimbi linalokua kwa vijana wa Kiafrika kila nyumba unakuta kuna vijana wawili, watatu hawana matumaini na mwelekeo sasa tunawapeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba mikopo iongezwe kwa vijana. Watakapokwenda kukaa watuletee jibu linaloeleweka kuhusu kundi kubwa la vijana ambao hawana ajira. Sasa inatia hofu baadaye wanaweza wakageuka wakaungana wakataka kupindua nchi. Hata kwa kuungana tu wakatembea wakapindua nchi sisi tukawa tuko juu.

Naomba hili kundi litazamwe kwamba je, tunawaona hao vijana, maana ni ngumu kweli.

Mheshimiwa Spika, wakulima nao licha ya mbolea kuondolewa kodi bado hali ni duni, yaani hakujatokea ubunifu uliokamilika kwa mkulima wa jembe la mkono kwani bado yuko hoi taabani. Sasa tunamwinuaje? Nimejaribu kutembelea baadhi ya Mikoa kutazama ulinganifu na nini katika hizi siku chache. Lakini unakuta kile kilimo cha zamani wanalichokuwa nacho angalau kiliweza kuleta matumaini kidogo wakalima pamba wakavuna kwa wingi, wakalima zao la kahawa wakavuna kwa wingi na zile fedha zikatosheleza mahitaji lakini sio sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kweli kuwepo mkakati wa makusudi ambao unaweza kufanana na nchi nyingine. Upo mfano wa Uganda. Uganda wana utaratibu mzuri tu kwa wakulima wao, upo mfano wa Kenya wana utaratibu mzuri kwa wakulima wao yaani mkulima mwepesi anaweza kwenda Benki akapewa mkopo. Lakini hapa kwetu mabenki bado yana kigugumizi hayajatambua vijana na wakulima.

Sasa mtu mwenye nyumba yenye hatimiliki anaipata wapi? Sasa mabenki wanawaona wenye nyumba ambazo zimejengwa kwa fedha nyingi, sasa vijana wasio na hati za nyumba tunawapeleka wapi? Wizara ya Fedha bado ina wajibu mkubwa kuweka ubunifu kwa kizazi chetu hiki kinachozidi kumangamanga. Kwa sababu vijana wale hawakwenda Shule wameishia Darasa la Saba hawawezi kupata ajira, sasa tunawapeleka wapi? Hawawezi kwenda kulima nyanya bila kuwa na mtaji, ataziuza wapi? Zinahitaji dawa na zinahitaji usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba kweli hili suala walitazame, vinginevyo watakuwa wanazua majina yasiyoweza kutusaidia MKUKUTA hili haliwezi kutusaidia. Tunaomba sasa hivi majina mengi ambayo hayana malengo yapungue. Hilo ni agizo Mheshimiwa Waziri wa Fedha baadaye utanijibu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba deni la Taifa linapofikia bilioni 523, hivi Mkoa wa Kigoma, Lindi, Mtwara, Tabora na Shinyanga linawahusuje deni lote namna hii? Maana mimi ningesema hivi kwa kipindi chote ambacho mimi nimekaa kama deni hili lipo la namna hii. Deni la Taifa haliendi sambamba wengine tunadaiwa tu kizazi au watoto wetu kwa Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine iliyo duni kama Rukwa halituhusu hebu lihamie katika Mikoa mingine ambayo wao wamekula hizo fedha. Mimi nabebeshwa hili deni la Taifa sasa nalipa huko wakati hakuna kitu kilichofanyika kwa Mkoa huo tangu nimekuwa Mbunge kwa muda wa miaka 15. Sasa mimi naomba maelezo baadaye. Sasa huwezi ukawa na deni la muda mrefu ambalo wewe unalipa, walipe Mikoa hiyo ambayo imepiga hatua.

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria mimi nasafiri kwenda Mkoa wa Kigoma siku mbili na hiyo njia ninayotumia kwa siku muda mbili alijenga Mjerumani. Hilo deni nadaiwa na Mjerumani? Mimi napenda kuuliza hilo. Hilo deni nadaiwa na Mjerumani? Hebu deni la Taifa lijenge barabara sasa ya lami kutoka hapa Dodoma, Singida, Itigi, Tabora mpaka Kigoma ili tuweze kusafiri kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam kwa siku moja siyo siku mbili. Sasa leo unakuwa umenibebesha deni la Taifa na lingine linazidi kuja deni la Taifa. Sasa deni la Taifa watabeba watu wengine ambao wanalipa tu hawawezi kusema na wao wamenufaika kwa njia ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sasa hivi ni wakati muafaka keki ya Taifa isambae kwa uwiano unaolingana. Siyo keki ya Taifa wale wengine na wengine waishie kupiga makofi tu. Mimi nafikiri Mkoa wangu unapiga makofi tu. Sasa jambo hili hatuwezi kukubaliana kamwe. Hiyo keki tuile kwa uma na kisu kila mtu akiwa anajimegea sehemu yake na kama yupo anayegawa, basi atambue watu wengine. Naomba Mkoa wa Kigoma kwamba haujatambulika kikamilifu kwa sababu kama hauwezi kupata umeme, barabara na maji, basi utabaki kuwa maskini, lakini hili deni la Taifa tutaendelee kulilipa sisi kinyemela tu.

Mheshimiwa Spika, niombe la mwisho sipendi sana kuchukua muda niungane na wenzangu waliozungumzia wastaafu. Hao wastaafu wametumikia Taifa la Tanzania kwa nguvu, yaani wao wamelitumikia kweli tusiwasahau. Sasa hivi kuendelea kuwalipa Sh. 20,000/= ni kidogo sana zisizolingana na mahitaji ya sasa tuwaongezee angalau kwa asilimia 75, inawezekana tu. Mimi sielewi ni kitu gani kinacholeta kigugumizi.

Mimi ningeomba kwamba wastaafu wametumikia Taifa hili na mishahara yao ilikuwa ni midogo yapo mambo mengi ambayo yameelezwa hapa lakini bado wanahitaji watambuliwe siyo kuwalipa Sh. 20,000/= tu. Halafu wanazichukua baada ya miezi sita angalau ziongezwe ziwe Sh. 40,000/= zinaweza zikawasaidia. Kwa sababu wastaafu hao walikuwa wanasomesha watoto wao na kwa hiyo, hawana kitu kingine ambacho wanajivunia isipokuwa kuwalipa hiyo posho, lakini ipandishwe kutoka Sh.20,000 kwenda Sh. 40,000/=. Kwa hiyo, haya ni mapendekezo yaliyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na kumtakia afya njema Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili atakapokuwa anajibu basi niweze kufurahi katika majibu atakayoweza kuyatoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha. Lakini kabla sijasema neno napenda kumpongeza sana Waziri wa Fedha, jirani yangu Mheshimiwa Basil Mramba na Manaibu wake wawili pamoja na Makatibu Wakuu wake wawili, Bwana Mgonja na Bwana Lyimo, pamoja na Wakurugenzi wote na Wakuu wa Idara na watumishi wote kwa ujumla wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi cha miaka 10 kwa kusema kweli. *(Makofi)*

Umepata pongezi nyingi sana Mheshimiwa Waziri, Wasaidizi wako na Watumishi wote kwa kuweza kufanya kazi kwa bidii hasa kwa kuongeza mapato ya Tanzania kwa kila hali. Naipongeza *TRA* ambayo iko chini yako ambayo wamekusanya fedha kwa nguvu zao zote. Hatujasema ni mwisho, bado wako njiani kwa sababu uwezo mkubwa bado upo wa kukusanya ila tulikuwa tumelala. Lakini Wizara hii imetuamsha sana na imeleta nafuu kubwa sana kwa nchi hii.

Mimi nilipokuwa nikianza Bunge mwaka 1990 ruzuku ya Serikali ilikuwa haizidi Shilingi milioni mbili au tatu katika Wilaya. Lakini leo fedha nyingi zinamiminika Wilayani. Zinamiminika sana. Wabunge wa zamani wanalaumiwa sana wanasemwa hawakuleta maendeleo lakini sio kwamba hawakuleta maendeleo umaskini ulikuwa umetuzidi sana. Mradi wa darasa moja linakuwa linajengwa kwa mwaka mzima na wananchi. Lakini sasa hivi wanajenga madarasa 50, 60 kwa mpigo. Kwa hiyo, kuna matunda makubwa na Waziri umefanya kazi nzuri sana.

Lakini kuna mambo ya kufanya. La kwanza ni juu ya mishahara. Bado hatujazingatia mishahara ya watumishi, bado inaleta mianya mikubwa katika rushwa. Unazungumzia rushwa usitoe rushwa wakati wewe unampa mtu mshahara wa majuma mawili, majuma mawili tu amekaukiwa sasa atakula wapi? Wewe umepanga mshahara wake ni wiki mbili iishe atakula wapi. Hii ni lazima uweze kuelewa kabisa kwamba wewe unaleta ushawishi wa watu kuiba unamkabidhi mtu fedha wakati unamlipa wiki mbili, lazima akuibie.

Sasa huu uaminifu unaotaka kumjengea mtu bila kumlisha mpaka mwisho wa mwezi kwa nini usitarajie angalau basi fikisha wiki tatu akazane kwa wiki moja basi. Kima cha chini bado ni hatari kabisa. Kima cha mshahara cha kuishi ni bado chini kabisa. Marupurupu yamekuwa makubwa zaidi kuliko mishahara ambayo baadaye unaogopa kumlipa mtu kiinua mgongo kikubwa au pensheni kubwa ili umdanganye. Kwa hiyo, mimi naona unamdanganya, unampa pipi. Sasa wakati huo utakapomwachisha kazi atakufa haraka. Atazimika haraka kwa sababu ulikuwa unampa marupurupu, sasa kitu cha kupeleka nyumbani itakuwa ni shida.

Kwa hiyo, mimi naomba sana suala la kima cha chini lizingatiwe sana kipandishwe. Kama sasa hivi kuna tofauti kubwa kati ya Mashirika ya Umma na Serikali. Kima cha chini katika Mashirika kinakwenda mpaka Sh.200,000/= au Sh.300,000/=.

Mtumishi sasa hivi wa Serikali anapata Sh.50,000/=, Sh.60,000/= sijui namna gani. Watanzania ndio wako pale pale. *Graduate* anaacha *University* sasa hivi tunakosa Madaktari kule Wilayani wanakwenda katika *private* kwa sababu ya mishahara, huduma hatupati. Kwa hiyo, hii Awamu ya Nne inayokuja na nadhani itaingia kwa nguvu zote ya kupandisha na kupambana na huu umaskini. Hilo ndilo naomba kabisa kwa Serikali la mishahara ipandishwe. Kwa kweli bila kupandisha mishahara itakuwa ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kwa ajili ya watumishi ambao wako katika mazingira magumu ni Walimu. Tunashughulikia suala la Sekta ya kuondoa umaskini, afya, elimu na maji. Hawa watu wako Vijijini watumishi wao kwa nini wasiende sambamba na maslahi ya watumishi? Unajenga nyumba nzuri, unajenga Shule nzuri lakini mshahara wa Mwalimu na mshahara wa Muuguzi anayekaa Vijijini ni mbaya sana. Hawalipwi marupurupu yao, wanakaa *night* na watumishi bado kuna matatizo.

Kwa hiyo, naomba sana katika Wizara hii iangalie tena hasa kima cha chini cha hawa watumishi. Bado nipo kabisa pale pale kima cha chini katika Walimu, Waganga na Wauguzi walioko Vijijini. Kwangu Kiteto bado wanadai, wanalala wanakwenda kwenye matibabu ya kipindupindu wanapokuja kudai maslahi yao ni matatizo. Nashukuru sana Walimu wameshughulikiwa kikamilifu lakini nendeni katika Idara nyingine wana matatizo kama hayo hayo ya Walimu. Hakuna watu wanaowasemea. Wabunge wanajaribu kusemea, lakini juu juu hakuna Tume inayoundwa, wanaogopa Walimu kwa sababu ni jeshi kubwa. Mimi ni Mwalimu peke yangu. Ni jeshi kubwa lakini wengine wananyanyaswa, hawapati maslahi yao. Kwa hiyo mimi naomba hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilitaka kuzungumzia wakati sikuwepo, ni la kutoa fedha nyingi Wilayani. Unamwaga kama mchanga. Hatuna shida ya fedha sasa hivi shida ni namna ya kutumia, namna ya kuangalia, zinatosha. Lakini sijaona Idara yako inakuja kufanya ukaguzi. Kama hizi fedha zinatumika ipasavyo kwa kweli fedha hizi ambazo zinakwenda Wilayani zinatumika kama ipasavyo anza kuunda sasa Idara muhimu ya kufuatilia fedha hizi Wilayani katika miradi. Sio kwamba inasubiri Kamati ya Fedha itembelee kuangalia *value of money* au Kamati ya Bunge. Kuwepo na Kamati au Idara ambaye inayoshughulikia sasa miradi ambazo zinatumwa fedha. Tuna matatizo makubwa sasa hivi ya kwamba tusipoangalia badala ya fedha zinavyokwenda kusaidia wananchi zinakwenda kusaidia watu binafsi.

Kwa hiyo, naomba sana Idara ianze kuundwa ya kwenda kusimamia fedha hizi ambazo zinakwenda. Hakuna haja ya kuwangojea wale halafu uwashtaki. Maana yake sasa ndio unawategea, kuleni tuwapeleke Mahakamani, wananchi watakuwa wameumia sana. Kinga ni bora zaidi kuliko kutibu ndiyo tunachotaka sisi. Sasa hivi kuna *communication* nzuri. Pale Kiteto siku hizi hatuandiki *voucher straight* inakwenda mpaka Hazina. Hongereni sana Wizara ya Fedha kwamba mnaweza kudhibiti.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni suala la *VAT*. Ebu chunguzeni utaratibu wa *VAT*. Nani anaumia katika *VAT*, ni mlaji wa mwisho ambaye mwananchi maskini. Wengine

wote wanakusanya tu. Anayeumia kwenye *VAT* ni yule maskini mlipaji wa mwisho, huyu wa katikati na kumtoza yeye anakusanya, huyu wa mwisho ndio anaumia. Ebu angalieni *VAT* kwa makini mnaweza mkatuletea umaskini halafu mnakusanya. Mtu wa Vijijini ataumia. Nasema hivyo kwa sababu msipoangalia huu mfumo wa *VAT* tutaumia.

Halafu muangalie Ofisi zenu hamuwezi mkatajirika Ofisini zenu huko juu yakawa mazuri. Pale Kiteto Ofisi ya Mapato hawana kiti, ukienda unakalia kwenye kimbao tu. Pale Ofisi yetu ya Wizara ya Fedha ni mbaya mrekebishe. Kwa hiyo, nawaombeni sana katika suala hili kwa kweli bado nazidi tu kusema kwamba hayo ni masahihisho tu najaribu kufanya lakini kazi mliyofanya Wizara ya Fedha ni nzuri na nawapongeza sana. Hayo najaribu kuboresha tu lakini sifa iko pale pale. Naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Mramba kwa vile ile lami imeshatengenezwa sasa ile barabara utaingia hapa na Awamu ya Nne utaingia hapa. Nakutakia kila la kheri na tuko jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakutakia kila la kheri, nimepata afya njema sana. Mwakani sisi tutajitahidi kuja na tutaingia. Kwa hiyo, tunakutakia afya njema tukutane hapa hapa tena. Nakushukuru sana naunga mkono. (*Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, lazima kwanza niseme kwamba katika haya ninayotaka kuzungumza kuna mambo binafsi yamenigusa. Tunakwenda ibara ya 68 ya hoja hii huduma ya Bima. Mimi nilikuwa mtumishi wa Bima. Ninachotaka kuzungumzia ni mambo yanayoihusu Sekta ya Bima.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mramba binafsi, Naibu Waziri Festus Limbu na Abdisalaam Issa Khatib, Makatibu Wakuu Bwana Mgonja, Bwana Lyimo na Manaibu. Hawa watu nimefanya nao kazi bega kwa bega na linapotokea jambo linanikera tunaelezana na hasa Waziri anajaribu kunituliza. Lakini sasa imefikia wakati ninavyoona mambo haya kwa sababu ana majukumu mengi huenda wanaomsaidia au hizo Idara zake wanamtegeshea.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la wafanyakazi takribani kama 200 wa Shirika la Bima ambao hawana ajira. Huu ni mwaka kama wa nne wamepeleka masuala yao Mahakamani, kila Mahakama inaposema kwamba walipwe inakatwa rufaa. Kila inaposema walipwe inakatwa rufaa. Mimi mwenyewe pia nilikwenda kivyangu wao walikwenda Mahakama nyingine lakini mimi ninaposema nilipwe nikienda wanakata rufaa, sasa bado rufaa moja tu labda kwa Mungu. Lakini kwa Mahakama za hapa Tanzania mimi nafikiri zimejitahidi kufanya haki lakini Menejimenti ya pale haifanyi inavyopaswa.

Lazima tukumbuke kwamba hawa walikuwa wafanyakazi waaminifu, wamefanya kazi miaka mingi na miaka ya 1980 Shirika la Bima lilikuwa linategemewa na Hazina,

kama kuna matatizo ndio walikuwa wanachukua fedha kule, leo wafanyakazi ambao walijitahidi kufanya hivyo wananyanyasika kama vile nchi hii haina masuala ya utawala bora. Utamhamishaje mtu nyumba anayokaa bila kumpa haki zake? Kesi iliyokwenda Mahakamani hata mtu ambaye alisoma mwaka wa pili Chuo Kikuu anaweza akajua kwamba kuna mtindo Menejimenti imeamua kuwakomoa hawa wafanyakazi.

Mkataba wa hiari uliosainiwa Mahakama ya Kazi. Ule Mkataba ulikuwa unaelezea juu ya kuwapandishia wafanyakazi marupurupu. Hakuna mahali uliposema kwamba ongezeko la mshahara huu litapatikana endapo Shirika litafanya faida. Lazima kuwe na *provision* kwa sababu waliosema Sheria na Mkataba unavyosainiwa ndivyo unavyotakiwa kutekelezwa.

Lakini nasikitika bahati mbaya hii leo nimeshtukizwa maana yake tunajua Wizara hii inakuwa mwisho wa Bunge. Lakini tumegundua leo mimi nilivyoingia humu ndani nikakuta voti 50. *Diskette* yangu iko ninakokaa.

Sasa nataka kuzungumza mambo ya msingi ambayo naomba Mheshimiwa Mramba yeye ni Waziri kusema kweli, siwezi kummaliza kwa sifa lakini jasiri, muadilifu, hana mizengwe wala hana tuhuma katika miaka yote kwa sababu Shirika la Fedha kama unapiga miaka 10 bila *scandal* wewe ni mwanaume. Lakini hapa bwana Mheshimiwa huyu hana *scandal*. Hana *scandal* ya fedha wala hana *scandal* ya Mitaani, nyumba ndogo na kadhalika. Ni mtu mwadilifu ambaye sisi wote tunamheshimu.

Kwa hiyo, tunajua hili jambo lazima uliundie Tume liweze kumalizika kabla hata wakati huu haujakwisha kwa sababu siwezi kukwambia waliokuwa wanadai walikuwa wangapi na sasa wamebakia wangapi. Kwa sababu watu wameondoka homa ya manjano, homa ya kisasa, ugonjwa tulionao na kadhalika.

Kwa hiyo, mimi ninachoomba, tafadhali sana nitakubaliana na Mheshimiwa Mramba katika hoja hii hapo atakavyoniambia kwamba kuna Tume ya kulimaliza hili jambo angalau la watu watatu au wanne ili kwanza ifanye kazi ya kuokoa maisha ya hawa watu ambao wanachezewa mchezo. Pili, ifanye pia njia ya kutafuta namna ya kuliwezesha hili Shirika liweze kwenda vizuri kwa sababu hizo Shilingi bilioni nne zilizotoka kwenda pale ni kwa ajili ya upande wa *life* haziwezi kusaidia lolote.

Mheshimiwa Spika, kama tunazungumza, katika wahimili watatu wa dola, Mahakama, Bunge na *Executive*,lakini sasa inafikiaje wakati kama mimi Mkurugenzi ananiambia kwamba suala lako tutalimaliza mimi nitakulipa, mwingine anasema aah nikikulipa wewe wengine watasema vibaya.

Lakini mimi *issue* yangu ninachosikitika ni kwamba nimekuwa kama nimedhalilishwa kwa sababu kwanza tulizungumza na sio kwamba nilisema nilipwe kama Mbunge, waende kinyume lakini tulikubaliana hili jambo lifikie mwisho kwa sababu mtu akidai Shilingi milioni 50 au 200 kama ukiweka zaidi ya mwaka mmoja itakuwa milioni 500. Mimi tulikubaliana lazima kama Mkurugenzi yupo nataka kutoa ushahidi aliniambia bwana nitakulipa nusu, nusu baadaye.

Mheshimiwa Spika, tumekutana Nairobi *on transit* mimi nakwenda Hongkong yeye anakwenda Addis Ababa kwenye Mkutano, akaniambia tafadhali ukirudi Hongkong njoo uchukue fedha yako. Nikajua sasa na mimi mambo yangu ya Jimbo yatakuwa mazuri. Nimerudi Hongkong nikamfuata Ofisini anasema tume-*appeal*.

Sasa nasema hii uta-*appeal* mara mia ngapi katika mambo kama haya? Sitaki kwenda *into detail* Mheshimiwa Waziri mimi naomba kwa kusaidia jambo hili kwa sababu nilitaka kuzungumza zamani sana *PM* akaniambia *don't do that,* kama wewe una maneno zungumza na Mramba. Barua hiyo aliyoniandika *PM* ninayo.

Sasa leo nazungumza nusu nusu, ninachotaka Mheshimiwa Waziri uunde Tume ya kurekebisha hili jambo ili angalau tuokoe maisha hayo ya Wapigakura, hawa watu waaminifu ambao wamefanya mambo mengi kwa ajili ya lile Shirika leo wanateseka. *Details* zake utazipata kwa hawa watu utakaowachagua. Hilo ndilo linanikereketa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niseme tu kwamba kwa mtu ambaye anazungumzia juu ya hili Shirika, wanasema hapa mpaka mwaka jana 2004 madeni yalikuwa Shilingi bilioni 14 halafu tukaenda mpaka mwezi Machi madeni yaliyolipwa yalikuwa ni Shilingi bilioni 21 na wakati faida tulipata Shilingi bilioni 29 kwa maana kwamba kulikuwa na faida Shilingi bilioni nane. Halafu kwenye vitegauchumi tumekwenda mpaka tumepata faida ya Shilingi bilioni 124 kwa upande wa vitegauchumi.

Sasa hii *deficit* inatoka wapi? Mimi kusema kweli sielewi, lakini kwa sababu sio mchumi. Lakini kwa mwingine anayeona anaweza kusema sasa hili tatizo la fedha kweli Shirika linakuwakuwaje? Hilo nafikiri baadaye kwa sababu wasomi wenyewe ndio Mheshimiwa Waziri umebobea kwenye suala hilo utaweza kunielekeza.

Halafu jambo la mwisho niseme kwamba kama Shirika linafuata maelekezo na kwamba halitaki kufanya mambo labda likaonewa kwamba wao wanafanya mambo ya ovyo, lakini hawa Menejimenti, watu wachache walijistaafisha wakajilipa marupurupu wakaanzisha mtindo wa kuingia kwenye Mikataba miaka miwili miwili, hivi jamani tunaweza tukafika mahali kwenye Shirika la Umma tukafanya mambo ya utaratibu kama

huu? Sasa hii kwa kweli wale watu ambao wanapenda haki hawawezi kusemea vichochoroni, lazima tusemee hapa!

Mimi nasema kwamba nitakuwa mtu wa kwanza kukuunga mkono hoja yako kama utanielezea kwamba utaunda *consultancy team* hata kama *Parliamentarians* wapo kuweza kuona hili jambo ambalo linaweza kumalizika ndani wiki mbili au tatu likatolewa jibu na dawa zake zikapatikana, kuliko huu mtindo wa kucheza na Mahakama. Mahakama inasema ulipe wewe unasema tuna *appeal*. Sijui kama Bwana Chenge anaweza akaruhusu suala hili likimalizika labda kwenye Mahakama zake liende *The Hague,* Uholanzi huko nafikiri ndio labda wanaweza kufanya mambo haya mapema.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nimshukuru Waziri kama wanavyoshukuru Watanzania wengine kuwalipa Walimu. *Payroll* yangu ya Wapigakura wangu au wa Wilaya yetu ya Kilwa bahati mbaya kesho kutwa wiki ijayo wale jamaa wanapeleka tena madai mengine kwa sababu yalitokea matatizo ya kawaida kwenye kompyuta ambayo baadhi ya Walimu wanadai madai yao. Kwa hiyo, naamini kwa umahiri wa Hazina kwa sababu hawafanyi kazi ovyo ovyo watawamalizia hawa Walimu madai yao ili hizi kero ziweze kupungua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naamini Mheshimiwa Waziri ataweza kunieleza hali ilivyo kuondoa hali ya unyanyasaji au ya udhalilishaji kwa watu tusiokuwa na hatia. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Fedha.

Napenda nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo ameisoma asubuhi hii. Aidha, nimpongeze Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Makatibu Wakuu na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya ili tuwe katika hali nzuri ya kuweza kuendesha Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *TRA* pamoja na watumishi wake kwa kazi nzuri ambayo mmefanya ya kukusanya mapato. Bila mapato tusingesimama hapa kuzungumza na bila mapato tusingepata mafanikio yoyote. Kwa hiyo, tuwapongeze kwa kweli kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niungane na Wabunge waliotangulia kuchangia. Wamechangia vizuri sana na mimi nisingependa kurudia. Naunga mkono yale yote ambayo wameyazungumza. Sasa na mimi naomba nichangie machache yafuatayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza na malipo ya pensheni kwa wastaafu. Wastaafu wanatoa shukrani nyingi sana na kubwa kwa Serikali kwa ujumla na hususan

kwa Wizara ya Fedha kwa mambo mawili. Moja kwa utaratibu wa kuendelea kuboresha pensheni hasa ya kiwango cha chini.

Tulikuwa na pensheni ya kiwango cha chini kabisa ambao wastaafu walishindwa hata kuifuata Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu nauli ilikuwa kubwa kuliko pensheni waliyokwenda kuifuata. Lakini Serikali ya CCM ikawa na busara kubwa ya kuweza kuongeza pensheni. Hivi sasa kiwango cha chini cha pensheni ni Sh.20,000/= kwa mwezi. Kwa hiyo, napenda kuwashukuru au kuishukuru sana Serikali kwa kufanya busara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia uamuzi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi uliofanyika hivi karibuni ya kuwarudisha wastaafu waliochukua pensheni kwa mkupuo nao ni uamuzi mzito. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wastaafu wanaishukuru sana Serikali kwa uamuzi huo. Hivi sasa wastaafu wale ambao walikwishakata tamaa kwa kweli sasa wamepata nuru ya kuweza kupata angalau fedha kidogo ya kuweza kuboresha maisha yao. Kwa hiyo, kwa niaba yao na hasa kwa niaba ya wastaafu wa Jimbo la Kondoa Kusini napenda niishukuru sana Serikali kwa maamuzi hayo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo, wastaafu hao wana maombi mawili. Moja limekwishatajwa na napenda nirudie na mimi kwamba kiwango cha Sh.20,000/= kwa mwezi ni kidogo sana. Wanaomba angalau wafikiriwe tena kuboreshewa kiwango hicho, hili ndio ombi la kwanza. Ombi la pili, Sheria ya Pensheni inasema wastaafu lazima walipe kila mwezi lakini kwa kutumia busara Waziri wa Fedha aliyepita na huyu wa sasa waliona kwamba hii pensheni ni ndogo sana.

Kwa hiyo, tudundulize ama tukusanye kidogo kidogo mpaka ifike miezi sita ndiyo tuwalipe angalau fungu hilo litakalopatikana kwa miezi sita. Lakini sasa hii wastaafu hawa kwa kweli wanalalamika kwamba huu muda ni mrefu mno kusubiri pensheni kwa miezi sita ni muda mrefu sana.

Kama nilivyosema hapo awali kwamba Sheria ya Pensheni inasema mstaafu analipwa kila mwezi lakini tulitumia busara kusema kwamba tulipe kwa miezi sita kwa sababu kiwango ni kidogo mno na hakitoshi hata nauli ya kufuatilia kule Wilayani. Sasa kwa kuwa tumeboresha, mimi naomba na wastaafu wanaomba kwamba angalau tupunguze ule muda, wasingependa kulipwa kila mwezi lakini angalau kwa robo mwaka miezi mitatu mitatu, hebu tufikirie.

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana 2004 niliwahi kutoa pendekezo hili na yeye akaafiki akasema aah nitakwenda kuliangalia. Lakini kwa matokeo ambayo tunayo sasa hivi ama kwa hali tuliyonayo sasa hivi ni kwamba bado hajalifanyia kazi. Namkumbusha kwamba wastaafu wanaendelea kusisitiza kwamba muda wa miezi sita ni mrefu sana wa kusubiri pensheni wana matatizo mengi, wanataka matibabu hapo hapo katikati. Kuna mahitaji mbalimbali tunaomba

tupunguze muda huo uwe wa miezi sita, kwa hiyo, walipwe kila baada ya miezi mitatu. Naomba sana Serikali pamoja na Wizara kwa ujumla tuangalie ombi hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia suala la pensheni, sasa na mimi niungane na Wabunge waliotangulia kuzungumza juu ya Shirika la Bima la Taifa. Lakini mimi nitazungumzia kuhusu kero wanazopata wateja wa Shirika hili. Waziri mwenyewe ukurasa wa 38 ibara ya 71 amekiri, napenda kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika naomba ninukuu. Anasema "Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa limekabiliwa na madai mengi na ya muda mrefu ambayo ni kero kubwa kwa wateja wake."

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Waziri kwa kukiri wazi wazi kwamba hili Shirika lina matatizo makubwa na ni kero kwa wateja wake. Mimi nakubaliana naye. Sasa kama ni kero tunafanya nini? Mimi napenda niseme tu kwamba kila mteja wa Bima anapokwenda kukata Bima ana malengo yake. Kama mimi nakata Bima ya gari maana yake nategemea nikipata ajali kwa bahati mbaya ama gari langu likipata ajali kwa bahati mbaya nilipwe mara moja ili niweze kuendelea na huduma ya gari. Lakini kama gari linapata ajali silipwi kwa miaka 10 maana yake nini? Si kama mnanitapeli?

Mheshimiwa Spika, nisingependa kutumia neno hilo lakini bahati mbaya naomba unisamehe, kwa sababu ndivyo inavyooneka kiutendaji, kwamba kama vile tunawatapeli wateja na hatuwatendei haki, tunakalia haki za wateja wetu kwa muda mrefu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hilo shirika lina faida gani? Hilo shirika lina faida kama tunakalia haki za wananchi ama wateja, mimi sioni shirika hilo kama linafaida. Kwa sababu lengo la shirika ni kusaidia wateja wake ili waepukane na majanga ama waweze kufikia malengo yao, ninayo hapa orodha ya Walimu 200 wa Wilaya ya Kondoa, bima zao zimeiva miaka mitano iliyopita kila siku wanaambiwa njoo kesho, njoo kesho. Hivi njoo kesho tutafika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mapendekezo aliyotoa hapa. Pendekezo la kwanza ni kwamba ameamua kwamba Serikali sasa ichukue hatua ya kulikopesha shirika hili ili liweze kupunguza madeni yake.

Pale tumeambia kwenye ukurasa wa ngapi sijui, amesema kwamba amewakopesha shilingi bilioni 4 kupunguza madeni. Sasa mimi nasema na nashauri kwamba shilingi bilioni 4 ni kidogo mno. Tutoe pesa za kutosha, tuondoe kero hiyo na tuwalipe wateja wa Bima kama mna utaratibu, kwa sababu bado ni Shirika la Taifa kama mna utaratibu muendelee kulilea hilo shirika mpaka litakapo kufa, tutenge fedha za kutosha tuondokane na hao wateja wanaotukera.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba sisi Wabunge ndiyo tuliowahamasisha hawa wateja kuja kwenye shirika letu la Bima kukata Bima aina mbalimbali na hasa zile za maisha. Mimi nimeshauri sana Walimu wangu wachukue Bima lakini sasa nimekuwa ni adui wao kwa sababu nimewauza. Wananilaumu kwamba wewe umetupeleka kwenye shirika tapeli sasa tumetapeliwa, sasa naomba basi mnisafishe jina naWabunge wengine

wa aina yangu, tunaomba mtusaidie. Mimi naomba kabla ya uchaguzi haujafika mlipe Bima ya wateja wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba Waziri karibu miaka mitano anaendelea kutuambia kwamba wanaendelea kuchambua mali za shirika hili wauze ili waweze kulipa madeni. Huu uchambuzi utaisha lini?

Mheshimiwa Spika, leo anasema hivyo hivyo, mali ziko nyingi na hatuna sababu ya kuendelea kuchambua, pigeni minada watu wapate haki zao. Hatuna sababu ya kuendelea kuchambua, unachambua nini? Lile ghorofa la uchumi pigeni mnada hilo, ama lile la Ubungo, pigeni mnada watu walipwe haki zao. Kwa nini tunakalia haki za watu?

Naomba kwa kweli tufanye hilo ili tuweze kunusuru watu ambao wengine walikuwa wanalenga kusomesha watoto, wamekwama, wengine walilenga kujenga nyumba wamekwama, wengine walikuwa wanalenga kufanya biashara na gari lake kama ni mfanyabiashara wamekwama.

Sasa kweli tunatenda haki hivyo, shirika hilo mimi nilikuwa naliheshimu sana na mimi bado ni mteja, naendelea kuwa mteja lakini pindi nitakapopata ajali kwenye gari yangu najua sitalipwa, lakini ninaimani na shirika na hasa ninaimani na Serikali kwamba inaweza kusaidia kunilipa madai yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme la mwisho naomba niungane na Mheshimiwa Benedict Losurutia, ambaye amezungumza vizuri sana kuhusu uwezo wa Serikali ama uwezo wa Halmashauri zetu sasa wa matumizi ya pesa na mimi naungana na Mhehimiwa Benedict Losurutia kusema kwamba Serikali kweli inajitahidi sana kuleta fedha nyingi katika Halmshauri zetu. Lakini usimamizi umekuwa ni mbovu kwa sababu hatuna wataalam hasa wahasibu na hasa Waweka Hazina hatuna.

Sasa nasemea hapa kwa sababu Wizara hii ndiyo inayosomesha wataalam wa aina hiyo, mimi nitoe ombi langu rasmi hapa kwamba Halmashauri ya Wiliya Kondoa haina Mweka Hazina kwa miaka zaidi ya mitano. Naomba tupatie Mweka Hazina na msinipe masharti kwamba tangazeni, hawapatikani ukitangaza. Nipeni kutoka Wizarani ili aje asimamie pesa na mimi na Halmashauri yangu imekosa pesa kwa kukosa Mweka Hazina. Sharti mojawapo la wafadhili ni kwamba kuwe na Mweka Hazina. Sasa unawaadhibu wapiga kura wangu kwa kutokunileta Mweka Hazina mwenye sifa na wafadhili wanakataa kutoa pesa zao, kwa hiyo, maendeleo ya Wilaya yangu na Jimbo langu yanazidi kudidimia kwa sababu sina ama hatuna Mweka Hazina. Sasa naomba nipate jibu kuwa lini tutapata Mweka Hazina mwenye sifa na mimi nitakuunga mkono sana kwenye hotuba yako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa kuwa tuna nafasi nyingine labda utatupa ya kuchangia tutakupa pongezi na tutakuomba uendelee kuwa Spika wetu katika kipindi kijacho, kwa hiyo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha ipite kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo katika Wizara hii. Kabla sijafanya hivyo naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuzungumza nimpongeze sana Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niipongeze Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato *(TRA)* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwa muda wote na kuiwezesha Serikali yetu kuwa na uwezo mzuri na kuweza kufanya kazi nzuri, natoa pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwanza nilikuwa naomba nianze na ombi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri atakumbuka tuliwahi kukutana naye sisi Wabunge tunaotoka katika Mikoa ambayo imekuwa ikipata Bajeti ndogo, nimwombe kwamba Mkoa wa Singida autazame vizuri kwa kuuongezea bajeti hasa bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati anajibu hoja za Wapinzani Mheshimiwa Waziri wakati ule tunapitisha ile bajeti ya fedha ya nchi nzima, alijaribu kufafanua ni namna gani alivyoweza kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mikoa mbalimbali na baadhi ya Mikoa ambayo imekuwa ikipata bajeti ndogo lakini bahati mbaya hakuwa ameelezea namna alivyosaidia Mkoa wa Singida kuweza kuipatia bajeti ya maendeleo. Sasa inawezekana mikakati yake haijawa sawa sawa kwa hiyo, akawa hana la kusema kwa Mkoa wa Singida. Lakini kwa kupitia Bunge hili sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajaribu kuweka mikakati ya kutafuta hiyo fedha.

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano, alikuwa ametoa na yeye mfano wa barabara ambazo amezitafutia fedha, sasa katika Mkoa wa Singida tunaishukuru Serikali kwamba imeamua kutujengea barabara ya rami kutoka Babati mpaka Singida, naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Serikali imeamua kujenga barabara ya lami kutoka Mbeya mpaka Makongorosi na hiyo barabara itajengwa mpaka Rungwa. Lakini nilikuwa nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba hizo barabara mbili ninazozizungumza kutoka Mbeya mpaka Makangorosi mpaka Rungwa ndiyo hiyo hiyo inayokuja mpaka Itigi mpaka Singida na kuunganisha na Babati. Sasa kama tutajenga barabara nzuri kutoka Kusini tukaishia katikati na kutoka Kaskazini tukaishia katikati bila kuunganisah hicho kipande kwa kweli nchi hii na hasa Mkoa wa Singida tutakuwa hatuutendei haki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine huwa kunakuwa na uwezekano wa kuzungumzia sana Mikoa ya pembezoni na kudhani kwamba ile Mikoa ya katikati huenda ndiyo inayofaidi, hapana. Mkoa wa Singida hauna tofauti na Mikoa mingine ya pembezoni kama Kigoma na kama atakumbuka Mheshimiwa Waziri kati ya Mikoa ambayo tulikuwa tumekutana nayo alikuwa amekutana nayo ilikuwa ni Mkoa wa Singida, Tabora, Shinyanga na Kigoma.

Kwa hiyo, naomba hilo ujaribu kulitazama na kama tukiweza kujenga hii barabara safari ya kutoka Arusha kwenda Mbeya ni fupi zaidi kupitia barabara hii ya Singida - Itigi, Rungwa mpaka Mbeya kuliko ile nyingine ya kutoka Arusha kupitia Dodoma, Iringa - Mbeya inakuwa ni ndefu zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hiyo itazamwe.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Mamlaka yake ya Ukusanyaji wa Mapato inafanya kazi nzuri sana. Nilikuwa naomba aangalie uwezekano wa kuwapatia watumishi wake wa Mamlaka ya Mapato pale Manyoni gari kwa ajili ya kufanyia kazi. Nasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Manyoni ni kubwa sana ina kilometa za mraba 28,620 na nafikiri ni zaidi ya Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Sasa nilikuwa naomba kwa sababu hiyo na kwa ajili ya usalama wao pamoja na mali ya Serikali tunakuomba Mheshimiwa Waziri hata *Suzuki* ndogo ndogo tu, usiwatafutie gari ya fahari, uweze kuwapatia waweze kufanya kazi bila usumbufu. Kuna maeneo mengine yana misitu mikubwa, yana mbung'o, kwa hiyo ,utakuwa umewasaidia sana hawa watumishi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo Mheshimiwa Waziri ujaribu kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuzungumza kuhusu Madaktari. Nilikuwa naomba Serikali kwa kila hali mimi niseme niko chini ya miguu ya Serikali iwaangalie hawa madaktari kuwaongezea mishahara kweli kabisa. Ninayo sababu ya kuzungumza hivyo, kwa sababu kwanza wanajihusisha na kazi ya kutibu watu ambayo inahusu uhai wa binadamu, sio kitu kidogo. Nilikuwa naomba hilo niliseme.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Madaktari tulionao Tanzania wengi wamesomeshwa kwa gharama ya Serikali. Sasa kama tunawasomesha kwa fedha zetu nafikiri matarajio makubwa ni kwamba warudi kuitumikia nchi hii hii ili Watanzania walipa kodi katika nchi hii waweze kufaidika na hiyo fedha inayolipwa na Serikali kuwasomesha Madaktari.

Sasa inakuwa sio vizuri hawa Madaktari baada ya kuona kwamba labda mishahara au maslahi sio mazuri nchini wakaondoka kwenda kufanya kazi katika nchi za nje na wengi wapo nje. Sasa hii ni hasara kwetu sisi kama Watanzania kwa sababu kwanza Serikali imewasomesha lakini matarajio ya kwamba waje kutumikia Watanzania wenzao yanakuwa pia hayapatikani wanakuwa wamekwenda nje ya nchi. Leo hii tukianza kuangalia katika Mkoa mingi na katika Wilaya nyingi utakata kuna upungufu

mkubwa wa Madaktari. Lakini sio kwamba hawasomeshwi. Mimi sina uhakika tunasomesha Madaktari wangapi wana graduate kila mwaka sina uhakika.

Lakini hata kama wana *graduate* 59 kila mwaka, tuna uwezo wa kila Mkoa kuweza kuupatia angalau Daktari mmoja. Lakini je, tukiangalia kila Mkoa umekuwa ukipata Daktari kila mwaka Daktari mmoja? Utakuta hakuna. Lakini wanakwenda wapi kama hawapatikaniMikoani? Kama hawapatikani basi kuna mahali wanakwenda na wanakwenda huko kutokana na sababu mbalimbali na kubwa nafikiri ni ya maslahi.

Lakini vile vile nilikuwa naomba tuangalie hawa Madaktari wote tunakubaliana hata Serikali inakubali kwamba katika vijana wanaosomea masomo magumu magumu hasa haya ya sanyansi huwa mara nyingi kwanza ni wachache na hata katika kuwafikilia nafasi hawa ndiyo wanaofikiriwa kwanza. Lakini vilevile kozi yao ni ndefu na ni ngumu. Wengine Shahada yao inachukua miaka mitatu ukija wa Engineering miaka minne, lakini wao ni mitano na mwaka mmoja wa kutazamiwa akiwa anasimamiwa na Mabingwa pale katika Hospitali ya Muhimbili. Kwa hiyo, ni miaka sita.

Sasa basi kuwe na mapato yanayolingana na mafunzo magumu ambayo hao Madaktari wanapata. Kwa hiyo, mimi hili nilikuwa naomba kabisa Serikali ijaribu kuliangalia, vinginevyo tutakuwa tunakutana hapa kila siku Serikali inaulizwa ni lini Hospitali yangu itapata Madaktari. Kama tutaliangalia hili mimi nina uhakika kabisa Madaktari hata huko vijijini watakuwa tayari kwenda kufanya kazi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo Serikali ijaribu kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba nizungumze kama walivyozungumza wenzangu suala la pensheni. Suala la pensheni wenzangu wamezungumza vizuri sana, lakini mimi nilikuwa naomba nizungumzie katika lile suala la kuwalipa hawa wanaokuwa wamestaafu. Wamekuwa na matatizo mtumishi anapomaliza utumishi wake wa umma amekamilisha taratibu zote kwa kweli imekuwa wengi wanasumbuka, ukienda pale Wizara ya Fedha Idara ya Pensheni kule Dar es Salaam utakuta wazee wanasota. Huyu mtu amekwishastaafu hana kipato anasuburi pensheni yake, haiji, anaamua kwenda Dar es Salaam kwa kujigharamia lakini na ule muda anaokaa pale labda awe na jamaa yake. Lakini vile vile kama atachelewa kulipwa anakuwa kero kwa jamaa yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inautaratibu kidogo ambao unashangaza, wewe kama muda wako wa kustaafu umefika, usipostaafu unaletewa barua. Kwanza kuna taratibu ya kukuletea barua ya kukumbusha kwamba muda wako wa kustaafu umekabiria. Sasa sijui hizi kumbukumbu huwa wanazipata wapi. Maana unapostafu unaambiwa leta barua ya ajira, lete sijui barua ya *confirmation* sijui na barua za nini. Lakini ukichelewa wanakuletea kwamba bwana wewe umechelewa kustaafu, hizi kumbukumbu huwa mnazipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukichelewa utakapokuwa unalipwa wanakukata mafao yako kwa sababu umechelewa. Sasa kama mnaweza mkakumbuka kwamba mimi nimechelewa kustaafu mkanikata basi muwe mnakumbuka vile vile kuwalipa mafao yao mapema na kama walivyowahi kuzungumza sehemu nyingine Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana

hizi huduma za kulipa mafao ya hawa watu walistaafu zikiweza kupelekwa Mikoani ua Wilayani mtakuwa mmewasaidia sana, hilo nilikuwa naomba nalo tuliangalie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nilikuwa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri katika ukarasa wa 18 ibara ya 32 pale anaposema usimamizi wa raslimali. Katika usimamizi wa raslimali Serikali imepata karibu faida ya gawio ya karibu bilioni 12.5. Kwa kweli kwa madhumuni ya Serikali kuwekeza hisa katika Mashirika mbalimbali hili ndilo mojawapo tunalolitarajia kwamba Serikali ikiwekeza mahali ipate gawio. Kama inapata gawio ina maana hata kodi itapata

Lakini twende kwenye Shirika letu la Bima kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge, tunaambiwa *insurance is the pulling of risks* yaani zile *risks* za sisi wateja wa Bima huwa tunaziweka wote pamoja na tunalipa *premiums* ambazo zinatakiwa zisaidie kwamba mwenzetu anapopata tatizo inatolewa fedha pale analipwa yule kumrejesha katika hali yake ya mwanzo ili asipate matatizo. Sasa kama hili shirika linafikia mahali haliwezi likapata faida, haliwezi likalipa wateja matatizo yako wapi?

Mheshimiwa Spika, nii wazi kwamba kuna matatizo ya usimamizi, *management* sio nzuri. Kuna Msajili wa Hazina ambaye yeye ndiye anayesimamia hizi hisa analetewa taarifa ya hesabu kila mwaka, ilitakiwa kama shirika la umma linaonekana limepata hasara alitakiwa aulize kwamba hii hasara imepatikana kutoka na nini na kama ikiwezekana kuweze kuchukuliwa hatua. Lakini sasa utakuta haya mashirika yanakaguliwa, Msajili wa Hazina anapelekewa nakala anasoma anakuta kuna hasara mle labda kuna madeni mengi yako mule ndani, lakini namna ya kuchukua hatua inakuwa ni ngumu, hata Wizara mama wakati mwengine na yenyewe inapelekewa lakini hakuna kinachofanyika.

Sasa mimi nafikiri kungelikuwa na utaratibu, kunapopatika zile taarifa za ukaguzi wa mahesabu kwa husika wanapopelekewa basi wawe wanachukua hatua vinginevyo tutakuwa na mashirika yanapata hasara na sisi tumewekeza kule na sababu ya kuwekeza kule inakuwa haipo. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba tulitazame kupitia Ofisi yako ya Msajili wa Hazina kwa yale mashirika yote yanayopata hasara vinginevyo hili shirika la Bima halipaswi kupata hasara halipaswi kushindwa kulipa wateja. Kwa sababu hawa watu wanalipa premium kili mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie kukushukuru kwa kunipa nafasi na nasema naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa kupewa nafasi hii. Kwanza kabisa naomba niwapongeza kwanza Waziri wa Fedha, Manaibu wake na wataalam wote.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuwapongeza kwa sababu katika kipindi cha Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, amekuwa Waziri wa Fedha ambaye amekuwa na ubunifu wa kila aina ambao umeliweka Taifa letu katika sura ambayo inaheshimika na

inatolewa mfano watu wanakuja kujifunza mambo ambayo yanatokea Tanzania. Kwa hiyo, mimi naomba nimpongeze sana.

Tabia yake ya ubunifu ndiyo imetufanya tuione Wizara ya Fedha ni ya kawaida, zamani ilikuwa Wizara mojawapo ambayo ilikuwa hairidhishi sana yaani hata ikifika hapa siku za Bajeti inatia hofu, inatia wasi wasi. Lakini toka ameingia Mheshimiwa Basil Mramba, siku ya Bajeti inakuwa kama siku ya furaha tu kwa watu wote. Kwa hiyo, ameondoa sura ile ya kwamba Bajeti inakuwa ni kitu cha kumtisha kila mtu lakini inakuwa ni kitu cha kawaida, cha kufurahisha na cha kuleta matumaini kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya hali ya ubunifu tunaweza kuyaona, kwanza ni ongezeko la mapato. Tumeona, tumeshuhudia ukuaji wa uchumi, tumeshuhudia pia *inflation* kushuka kwa kiasi kikubwa sana na hata ile waliyosema wenzangu kwamba hata ubunifu wa kuamua kuwasaidia wale wastaafu waliochukua kwa mkupuo mapato yao kuwarudisha tena kuwa ni mapato ya kila kipindi nayo ni ubunifu wa hali ya juu sana. Kwa hiyo, mimi naomba niwapongeze kwa hayo yote. Nadhani pia ni ule usikivu wa ushauri mbali mbali ambao anapewa kuanzia ndani ya Bunge pengine na nje ya Bunge kutoka kwa watu mbali mbali pamoja na Wataalam wake mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kuongezea mambo machache tu kwa sasa. Kuhusu Pensheni, mimi naomba nikubaliane na ushauri ambao Mheshimiwa Monica Mbega, amesema. Mimi naamini kabisa tukiendelea kufuatilia wale wastaafu 3,000 ambao hesabu zao hazijulikani, nyaraka zao zimepotea, tukiendelea kufuatilia kwanza kabisa, tunatumia muda mwingi sana wa Hazina. Kama mngekuwa mnaweza kufanya hesabu ni muda gani mnatumia kuendelea kuwasikiliza na kuwafuatilia hawa watu kwa upande wa Hazina yenyewe, mngekuta ni hela nyingi sana tunazotumia. Lakini pia mngeenda kwa hao hao wastaafu wanaokuja kila siku kufuatilia hapo Hazina na kwenda na kurudi na wengine wanakufa na wengine kutoa manung'uniko ya kila aina, ungekuta nao hasara tunayoipata kwa kuendelea kuwaacha hawa waendelee kutafuta kwenye mafaili ambayo mnajua hayapo, kwa kweli gharama yake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nashauri kabisa tena kwa nia njema na kwa kuamini ubunifu wenu mlionao, tuwe na *cut of date.* Wale watu tunaweza kukadiria kabisa ni kiasi gani wanaweza kuchukua, wala hawatachukua zaidi wala hawatachukua pungufu sana. Wakalipwa hawa mkaondokana nao kabisa, kusudi muendelee na utaratibu mzuri ambao sasa hivi unatumika, kwa sababu gharama yake ni kubwa kwa upande wa Hazina hata kwa hao wenyewe wastaafu wenyewe. Kisiasa manung'uniko ya watu pia ni gharama nayo kubwa. Kwa hiyo, mimi naomba kabisa hili suala tutumie *cut of date* tuwalipe hawa halafu tuendelee mbele na utaratibu ambao ni mzuri zaidi na wa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita, Mheshimiwa Rais alikuwa anafanya kazi fulani, nimesahau ilikuwa kazi gani, lakini alitoa wito kwamba Watanzania mjitahidi kila unaponunua kitu udai risiti na hii siyo ameisema tu juzi hata wakati tunaanzisha *VAT*

wakati ule mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, tulipokuwa tunapewa semina kuhusu *VAT* kikubwa katika suala zima Tanzania ambalo hatufanyi na hatujafanya na tunaweza kulifanya pia, ni kupata risiti baada ya kununua kitu chochote mahali popote. Inafika mahali sisi wenyewe tunaona ni udhia tu kuomba risiti, lakini ukweli katika kuacha risiti tunapoteza mapato makubwa sana ya Serikali katika ngazi mbali mbali na tunawasaidia watu hao wanaotaka kuficha mapato ya Serikali kwa namna moja au nyingine. Tunawasaidia kuficha, sisi hao hao.

Kwa hiyo, tunajipunguzia sisi Watanzania uwezo wetu wa kufanyiwa mambo makubwa na Serikali kwa sababu risiti zile ndiyo tunaficha *revenue* ya Serikali. Lakini wakati huo huo natambua ugumu uliopo, maana inatakiwa kwamba mtu awe anaandika kila unapofika anakuandikia, anakuandikia, sasa ile kazi ya kuandika pia ni kero kwa watu, wale wenye maduka.

Mheshimiwa Waziri, katika ubunifu huo, hebu mfikirie, mbona kule nje mnakosafiri na sisi tuliosafiri tunaona, kila unaponunua, kitu mtu anagonga tu mashine anakukatia risiti yako hapo hapo. Rahisi tu, yaani unagonga tu kiasi kile cha pesa unapata risiti yako. Kwa nini Tanzania hatuwezi kufikiria kuwa na aina hiyo ya mashine zinazopatikana kwa bei rahisi lakini za uhakika ambayo Wizara ya Fedha itasimamia, kwamba mtu unaponunua kitu chochote unawagongea tu mashine unapewa tu risiti, hata kama huisomi lakini unapokea tu. Katika kufanya hivyo wanalipa kodi wale watu wanaohusika.

Mimi hili suala niliwahi kulisemea kule Ruvuma kwa yule aliyekuwa mtu wa *TRA* pale, labda lilikuwa tu Ruvuma tena na huku Makao Makuu ni mbali, lakini sasa naomba Mheshimiwa Waziri hebu fikiria hilo suala. Zikapatikana mashine za kuaminika, kwani kote tunakokwenda duniani iko hiyo. Lakini ukimtaka mtu aandike na mkono na kalamu kweli hataandika hata wewe mwenyewe unayesubiri pale unaona wanakupotezea muda. Kwa hiyo, una hiari potelea mbali hiyo senti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea hata Marekani utashagaa kitu kidogo sana kama kibanio cha nywele kinalipa kodi. Hata kibanio cha nywele unanunua kinalipa kodi, hata kama ni *zero zero point* ngapi ya senti, lakini ni hela. Lakini sisi ni vingapi vitu vikubwa vikubwa kabisa wala havishughulikiwi kwa sababu tunashighulika tu na Mashirika makubwa na wale watu wanaonekana. Lakini hivi vitu vidogo vidogo namna hii hatuvioni kuwa vina mchango wa kodi.

Mimi naamini tungefanya hivyo pia, tungeweza kuongeza sana mapato yetu wenyewe na kuwafanya Watanzania wawe wanawajibika katika kudai risiti kwa hao wanaonunua vitu vyao kusudi achangie katika mchango wa kuongeza pato la Serikali.

Mimi hili ninaomba nipendekeze na naamini Waziri kama hutakuwa na majibu, lakini naomba mkalifikirie sana hilo suala kwa sababu naliamini kwamba tunapoteza mapato mengi na Watanzania hatuwajibiki katika kukusanya pesa zile tunazonunua kidogo unachonunua unachangia Serikali. Ukiacha risiti, unamwachia yule mtu mapato

na akipata yeye mapato, hatakuchangia wewe katika maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, mimi nadhani tunaweza tukaongeza hayo mapato yetu yakawa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama *PPF, NSSF, LAPF* na ile mingine yote. Siku moja tulikuwa tunazungumza na wataalam katika Mifuko hii, ikaonekana kwamba Mifuko hii inawahudumia wananchi Watanzania asilimia kama 3 tu, asilimia 97 ya Watanzania hawana Hifadhi ya Jamii yoyote.

Kwa hiyo, tunaishi hivyo, lakini ni haki ya binadamu kuwa na uhakika kwamba anapoishi ana mahali anaweza kukimbilia siku ambayo anakuwa hana uwezo wa kufanya mambo fulani fulani. Kwa hiyo, mifuko yote, tunayo kama 6 hivi, jumla yake inahudumia kama asilimia 3 tu ya Watanzania. Asilimia nyingine yote ya Watanzania hakuna kitu chochote unachoweza kusema mimi maishani mwangu nikitindikiwa naweza kufanya hivi, hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tunapendekeza pia hili nalo tulifanyie mkakati mzuri kabisa, kusudi hata mkulima wa kawaida anapokuwa na nguvu anaweza kulima, atakapokuwa hana nguvu, hawezi kulima na watoto wenyewe tunaozaa sasa wanawaacha wazazi wao wanaenda zao wanakokwenda. Mzee wa watu unakuta anakufa ndani ya nyumba yake ingawaje alikuwa anajituma kwa nguvu sana katika kuzalisha wakati ana nguvu.

Mheshimiwa Spika, sasa hana nguvu hawezi, hana mahali pengine pa kwenda. Kwa hiyo, tunafikiri napo kama mlivyowabunifu, hebu jaribuni kuona ni namna gani tunaweza tukawa na utaratibu huu.

Nashukuru kwenye suala la afya utaratibu umebuniwa ingawa Watanzania wengi hawajaupokea kwa nguvu lakini tulifikiri nao ni muhimu ule Mfuko wa Afya ya Jamii. Ni kama aina ya Bima ya Afya ya Jamii ambapo familia inaweza ikakata hiyo kipande wakatumia kutibia familia yake wakati wanakuwa hawana uwezo wa kupata fedha. Imeanza lakini haijaenea sana, lakini nafikiri na Mifuko hii mingine pia ingeweza ikatafutiwa ubunifu wa namna fulani hata wakitaka sisi Wabunge tuje tutunge sheria hapa kuweza kubariki suala hilo, ni muhimu sana.

Kwa hiyo, mimi nafikiria Hifadhi ya Jamii ni suala la muhimu na ni haki ya binadamu yeyote kusaidiwa pale atakapokuwa hawezi, yeye mwenyewe hajiwezi. Suala la kutegemea watoto wetu watanipa hiki, watanipa hiki, linaanza kuwa halipo tena. Si ajabu kumwona mzazi mtu mzima leo anabakia ni kuomba tu, huku ana watoto wake ambao wako sijui wapi anakojua mwenyewe. Lakini kumbe tungekuwa na utaratibu ambao haujali una mtoto huna mtoto, unachangia wakati una nguvu, wakati unakuwa huna nguvu unao uwezo wa kuishi, mimi nadhani pia ni jambo zuri ambalo pia tungeweza kulizingatia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, Waziri wa Mambo ya Ndani alizungumzia habari ya Kitambulisho cha Taifa. Yeye anasema ni mradi mkubwa sana unatakiwa tuwe

na subira, unakumbuka hii sheria tumeitunga mwaka 1985 ya Vitambulisho vya Taifa, mpaka leo tena nadhani inatakiwa hata tufanyie *amendment* hiyo sheria. Kwa sababu hivi Vitambulisho vya Taifa vinatufikisha mahali hata Mabenki hayatuamini.

Mheshimiwa Spika, mtu anakwenda mahali ana jina moja halafu kesho anabadilisha anakuwa na jina lingine. Imetokea hivi jana, leo asubuhi nilikuwa nasikiliza kulikuwa na kesi moja mtu alikuwa na deni fulani alipoona yamemzidi akabadilisha jina. Lakini tungekuwa na Kitambulisho cha Taifa hakuna mtu anayeweza kubadili jina, atakuwa anaonyesha kile Kitambulisho cha Taifa.

Kwa hiyo, haya Mabenki yaliyopo yanashindwa kukopesha watu kwa sababu mojawapo hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na Mambo ya Ndani wanasema wamepata bilioni mbili wataendelea mpaka mradi mzito, mimi nadhani ni muhimu sana katika kupambana na umaskini bila kufanya hayo mambo mengine ni ya msingi tu bila kuyatolea uamuzi sasa, mengine pia yatatushinda.

Kwa hiyo, mimi naomba kabisa katika dhana ya ubunifu na hili nalo ni kero toka mwaka 1985 sheria tumeitunga humu ndani mpaka leo hakuna Vitambulisho vya Taifa. Yaliyotokea mimi sitaki kuyajua lakini nafikiri sasa tumeamka tuweze kuhakikisha Watanzania wanapata vitambulisho. Halafu suala lingine la kurasilimisha mali za wanyonge nalo hilo baadaye tutazungumza lakini hili kwanza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Spika, miongoni mwa kero kuu za Muungano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ni kuhusu mgawanyo wa fedha/mapato na michango inayopitisha kupata/kuchangia katika mfuko mkuu wa Muungano. Jambo hili limezaa manung'unikio kutoka pande zote mbili.

Serikali ya SMT imeunda Tume ya Fedha kuratibu masuala yote ya kifedha baina ya Serikali mbili hizi. Tulitegemea kwamba angalau ripoti ya awali ya Tume hiyo ingeweza kupatikana kabla ya uhai wa Bunge hili kumalizika. Aidha, Tume hii imejaribu mara mbili kutaka kuwapatia semina Waheshimiwa Wabunge juu ya utendaji wa Tume hii pamoja na kupata taarifa ya awali. Lakini jaribio hili limekuwa linazimwa na Wizara.

Mheshimiwa Waziri atueleze kuna nini ndani ya Tume ya pamoja ya fedha kunakosababisha kuwa hadi leo hatujapata taarifa yoyote ya utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, inaonekana dhahiri kwamba kuna ubaguzi mkubwa katika uajiri wa watendaji katika taasisi za fedha za Serikali ya Muungano. Tumekuwa tunaona wengi wa watendaji wa taasisi hizo katika Ofisi za Zanzibar ni kutoka Tanzania Bara na mara nyingi hata viongozi wake ni kutoka Bara. Lakini watendaji katika Ofisi za Taasisi

hizo zilizoko Tanzania Bara ni Watanzania Bara pekee kama utamkuta Mzanzibari basi ni cheo cha chini kabisa.

Mheshimiwa Spika, huu ni ubaguzi mkubwa. Mheshimiwa Waziri atueleze kwa ufasaha kabisa ni kwa nini Wakurugenzi wa Benki Kuu *BOT* ambao ni 18 na Manaibu Wakurugenzi ambao ni 47 wote wanatokea upande mmoja wa Muungano yaani Tanzania Bara lakini hamna hata mmoja kutoka Zanzibar, je, huu nao si ubaguzi?

Baada ya kupata maelezo ya kina juu ya kasoro hii pia Mheshimiwa Waziri atueleze ni hatua zipi atachukua kuiondoa ili kuleta uwiano ulio sawa na ile taswira ya kuwa upande mmoja wa Muungano unataka kumeza upande mwingine ifutike ndani ya nyoyo za watu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge na Waziri wa Fedha kwa hotuba yake fupi lakini yenye maelezo ya wazi na yanayoeleweka. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kuwapongeza Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, kwa kumsaidia Waziri wa Fedha kwa juhudi na maarifa.

Vile vile napenda kuwapongeza Makatibu wakuu, Bwana Gray Mgonja na Bwana Peniel Lyimo, Naibu Katibu Mkuu, B.W.R Khijah na watendaji wakuu wa taasisi chini ya Wizara hiyo na wataalamu wote kwa kutoa ushauri makini kwa Waziri na Naibu Mawaziri na kufanya hoja za Wizara ya Fedha kuwa nyepesi humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja tena kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na upendo nachukua na kuitumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili, Makatibu Wakuu wote wawili, Naibu Katibu Mkuu, Maafisa, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa hotuba yao hii nzuri, yenye mafanikio makubwa kwa maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia ili kuiwezesha Wizara hii iweze kutekeleza shughuli na majukumu yake kwa faida na maendeleo ya nchi yetu na ya Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naungana na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha juu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta yetu hii ya fedha. Naiomba Wizara kuongeza juhudi ili tuweze kupata mafanikio makubwa zaidi yatakayo iwezesha nchi yetu kuwa kati ya nchi zenye uchumi na maendeleo makubwa katika Bara letu la Afrika na Duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza sana Wizara yetu hii ya Fedha kwa juhudi na mipango yake inayothibitisha kuwepo juhudi kubwa katika kusimamia vizuri sana bajeti ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naiomba Wizara kuongeza juhudi zake katika kusimamia vizuri bajeti hii ya Serikali na pia kuongeza juhudi kuziba yale maeneo ambayo yanasababisha upotevu au matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuinukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa saba ambao anaelezea juu ya misaada na mikopo ya nje.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa kuwa Wizara inayo majukumu ya kutafuta na kuratibu misaada na mikopo nafuu kutoka nchi marafiki na mashirika ya fedha ya Kimatiaifa kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii pia inaelezea juu ya usimamizi na udhibiti wa matumizi, ambapo Wizara inaeleza kuwa inaendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa matumizi ya fedha za Serikali. Napongeza uimarishwaji, usimamizi na uwajibikaji huu wa matumizi ya fedha za Serikali na ni matumaini yangu kuwa suala la upotevu wa fedha nyingi za Serikali na umma katika Halmashauri zetu mbalimbali hapa nchini pamoja na katika sekta mbalimbali zinazohusika na fedha za umma utapungua au kuisha kabisa. Pia naomba Serikali yetu kuchukua hatua kali na za Waziri kwa zile sekta ambazo zinapoteza fedha nyingi za umma cha kushangaza taarifa za upotevu wa aina hii unaona katika vyombo vya habari kama magazeti kuwa mabilioni kadhaa ya fedha yamepotea katika sekta fulani bila ya kuwepo maelezo mengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba mtindo huu uachwe na udhibitiwe ipasavyo ili kulinda fedha za umma zisipotee ovyo.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inaelezea juu ya huduma za wastaafu.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kupunguza adha inayowapata wastaafu. Naipongeza sana Serikali kwa hatua zake hizi inazozichukua kuhusiana wastaafu wote na naiomba iongeze juhudi ili suala kama hili sasa liwe ni historia katika nchi yetu, wastaafu hawa kwa upande mmoja wametoa mchango mkubwa sana kwa Taifa letu hili ambalo leo hii limefika hapa lilipo na tukiwa na matumainio ya kwenda mbele zaidi katika maendeleo makubwa ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, vile vile ninaitumia fursa hii kuiomba Seikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza misaada ya fedha ya kiuchumi na kimaendeleo kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano kusaidia maendeleo ya Zanzibar. Nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa aliyoitoa tarehe 26/4/2004, kutimiza miaka 40 ya Muungano wetu wa Tanzania uwanja wa Amani, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo ya Mheshimiwa Rais ilisema kuwa Muungano wetu umefikisha miaka 40 na upo imara, nguvu yake ni Watanzania wenyewe wengi wao asilimia 84.8 wakiwa hawajui uraia mwingine ispokuwa Utanzania. Watanzania hawa waliozaliwa mwaka 1964 na kuendelea hawana uzoefu kuwa kitu kingine isipokuwa Watanzania hawajui mfumo mwingine isipokuwa wa Serikali mbili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maneno haya ya Mheshimiwa Rais wetu mwadilifu na mkweli kwa Taifa na Muungano wetu, ni vizuri tukayachambua vizuri, kuyatekeleza na kuyalinda muda wote kwa faida ya nchi na wananchi wote wa Tanzania. Tuheshimu, tuilinde na kuifuata Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zote za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tuondoe tofauti zetu na ubinafsi wowote ule ambao unaweza kutuletea matatizo ya umoja wa Taifa letu hili nzuri la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Lingine ambalo naliomba ni kuiomba Wizara ya Fedha na Serikali yetu ya Muungano wa Tanzania kuipatia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar fedha shilingi milioni mia tisa kwa ajili ya kuwalipa wastaafu wake.

Mheshimiwa Spika, nalileta ombi hili baada ya kusikia katika vyombo vya habari taarifa ya habari ya Redio ya Zanzibar hivi karibuni kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatafuta fedha kwa wafadhili kulipa wastaafu wake. Naiomba Serikali ya Muungano kuipatia Zanzibar fedha hizi za kuwalipa wastaafu wake.

Vile vile naipongeza Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kwa kutoa msaada wa fedha shilingi bilioni 43 kujengwa gati ya Zanzibar. Pia ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kulisaidia ombi langu la mradi wa maji Vitongoji kama tulivyowahi kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, namtakia kila la heri na mafanikio. Asante na naunga mkono hoja.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA:** Mheshimiwa Spika, kwa hakika kazi kubwa imefanywa na Wizara hii, hongera na pongezi nyingi sana ziwaendee Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi, Makamishina wote na wataalam wote kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Spika, maombi, imeonekana wazi kwamba wapo watu katika Wizara hii wameteuliwa kuwa wajumbe katika Bodi nyingi na baadhi yao wanatumia nafasi au madaraka yao vibaya. Wanajisahau kwamba wao ni wajumbe kama wenzao tu, tabia ya kujipendelea au kuonyesha madaraka mbele ya vikao vya bodi siyo sahihi kisheria na inaua ari ya utendaji na kukatisha tamaa wajumbe na menejimenti na mahali pengine baadhi yao unaanza kujiondoa au kujiuzulu au kuacha kazi. Ni vema Wizara iangalie tatizo hili na kulirekebisha mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, *LART,* ni chombo muhimu sana katika kukusanya madeni sugu nchini. Naona kinayumba, naomba Serikali ione tatizo lililopo pale ni nini na hasa kwa sababu limejitokeza hivi karibuni, wakati huko nyuma chombo hiki kilifanya kazi kubwa sana kwa furaha, uelewano na uthabiti. Ni nini kimetokea hadi kusababisha watu waanze kukimbia chombo, kujiingiza katika vitendo viovu? Naona kuna tatizo ambalo lapaswa kumalizika ili kuwezesha utendaji na uendeshaji mzuri wa *Trust* hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba pale panapowezekana Wizara iketi na vyombo mbalimbali vinavyosaidia Wizara kuendesha shughuli zake kama Bodi, Taasisi *PSRC* na kadhalika kujenga mazoea ya kukutana kuzungumzia migogoro au mafanikio badala ya kuendelea kuwasilisha kwa njia ya barua/nyaraka peke yake, jambo ambalo laweza kujenga chuki na uhasama baina ya wadau husika hasa pale ambapo lugha ya kuudhi kutisha, kebehi, vinajitokeza.

Waziri wa Fedha ulinipa nafasi katika chombo cha *LART* na umeendelea kunishirikisha katika mashauri mbalimbali kwa uaminifu mkubwa. Mheshimiwa Waziri umeenzi kwa kiwango kikubwa michango na ushauri wangu asante sana.

Nakuombea heri na fanaka Mheshimiwa Waziri katika uchaguzi ujao kwenye Jimbo lako la Rombo. Nakushukuru sana.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, shukrani, Waziri Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Gavana wa *BOT*, Wakuu wa Taasisi za *BOT, NIC, TRA, NBC, NMB, TPB, TIB, PPF Pension.* Shukrani nan pongezi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyongeza ya pensheni, pensheni kima cha chini kiliongezwa hadi 20,000/= mwaka wa nyuma, Je, mwaka huu imeongezwa shilingi ngapi kwa kima cha chini cha pensheni?

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa. Hivi Deni la Taifa hivi sasa tunadaiwa shilingi ngapi? Tangu zoezi la kupunguziwa au kufutiwa madeni ya nchi changa, Tanzania tumefutiwa shilingi ngapi hadi leo hii 19 Julai, 2005?

Kuhusu bei ya mafuta, kwa nini kusiwe na chombo cha kusimamia bei ya mafuta tu maana hadi sasa Serikali haijachangamka udhibiti wa mafuta ya magari, mitambo, *petrol*, *disel* na mafuta ya taa ambayo ni bidhaa muhimu sana kwa raia wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, *BOT* inajitahidi sana kudhibiti vyombo vya fedha nchini hadi sasa nidhamu ya mabenki iko juu, napongeza kitengo cha *Bank Supervision* wanafanya kazi nzuri sana, kitengo hiki kipanuke wapewe vifaa ili kufuatilia mabenki matapeli.

Mheshimiwa Spika, *TRA*, kuwe na *TRA Officers* chini ya Wilaya zenye biashara nyingi kudhibiti mienendo ya kodi kwenye Wilaya hizo mkoani Morogoro. *TRA* wanafanya kazi vizuri sana wanastahili pongezi

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha, kusaidia mashirika ambayo yamechoka mfano *TRC,* hivi Serikali (Wizara ya Fedha) imejiandaa vipi juu ya *TRC*, mabehewa mafao na utendaji wa kazi ndani ya Shirika hili muhimu naomba sana kwa *TRC* ni shirika nyeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba na Manaibu Waziri Mheshimiwa Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kusimamia masuala ya mapato na matumizi ya fedha za Serikali ya nchi. Baada ya pongezi hizo ningependa kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Benki za Umma, ni muda sasa si chini ya mwaka mmoja tangu azma ya kubinafsisha Benki ya *NMB* ilipojitokeza wazi, ninalotaka kufahamu ni lini basi benki hii itabinafsishwa? Ufahamu huo utasaidia kujibu maswali ya mara kwa mara ambayo tunaendelea kuulizwa na wananchi hasa wafanyakazi waliopo kwenye matawi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Asasi za Uwekezaji Wananchi, ni ukweli usiofichika kuwa Serikali ya awamu ya tatu imepania kuondoa umaskini wa mwananchi mmoja mmoja kwa kuandaa mazingira mazuri ya kuwawezesha kuwekeza hata kwa wananchi wenye kipato kidogo kabisa hasa katika mpango wa mfuko wa umoja ambao Wizara inaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha kuwekeza katika mfuko huu. Inatia faraja kwani katika mpango huu kwa kuanzia unawahusika Raia wa Tanzania peke yao tu.

Mheshimiwa Spika, ingawa matangazo yanasema kuwa mwisho wa kununua vipande ni tarehe 29 Julai, 2005 lakini nashauri Serikali ione uwezekano wa kuongeza muda ili kutoa nafasi kwa wananchi wa vijijini kuweza kununua vipande baada ya kuuza mazao yao ambayo kwa sehemu kubwa ya Tanzania sasa ndiyo msimu wa kuuza mazao ya nafaka.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu biashara ya michezo ya kubahatisha, nimefarijika kupata maelezo kuwa Bodi ya usimamizi wa michezo hiyo tayari imeanza kazi tangu Julai, 2003. Katika Sheria ya michezo hii iliyopitishwa Bungeni mwaka 2003 nilishauri kuwa kiasi cha fedha zitokanazo na michezo hii isaidie pia kufadhili michezo ya watu wenye ulemavu nchini. Kwa msingi huu naomba ufafanuzi toka Wizara ni kiasi gani cha fedha tayari zimetolewa kufadhili michezo hiyo?

Baada ya mchango huo naunga mkono hoja na kuwatakia wahusika utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2005/2006.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Basil Mramba na Manaibu wake kwa kuongoza Wizara hii kwa mafanikio

makubwa. Natoa pongezi kwa utaratibu mzuri mlioweka kwa kuwalipa walimu malimbikizo yao nchi nzima. Napongeza bajeti hii na ninaunga mkono, napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo na misaada ya wanawake wafanyabiashara wadogo wadogo, kuna wafadhili wengi ambao kwa hivi sasa wamezuka nchini kwetu kwa ajili ya kutoa mikopo ya nafuu kwa akina mama wafanyabiashara ndogo ndogo. Je, wafadhili hawa mbalimbali mfano ikiwa *Finca, Pride* na wengi wengineo wanadhibitiwa na nani katika taratibu zao za mikopo wanavyotoa Wizara ya Fedha inahusika kwa njia gani kuhakikisha ya kwamba hawa wafadhili siyo wako kwa ajili ya manufaa yao na biashara ya fedha.

Je, kuna mafanikio gani ambayo akinamama wanaokopa wamepata? Nina wasi wasi ya kwamba kufuatana na fedha ndogo wanazokopeshwa haziwezi kuzunguka na kuwapa hawa akinamama akiba ya kuweza kukuza biashara zao na kujikwamua kiuchumi. Isije ikawa wanafanya kwa ajili ya mazoea na wafadhili hawa kupata sifa ambazo siyo za kweli kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, ni lini Wizara ya Fedha itaamua kwa makusudi kushauri au kusaidia kuanzisha mfumo wa Benki ambazo zitakuwa tayari kukopesha wanawake mikopo mikubwa (fedha za kutosha kufanya biashara ya uhakika badala ya biashara ya uchuuzi ambazo wanawake wengi ndiyo wamo humo). Wanawake hawana dhamana lakini nao wanahitaji mikopo mikubwa kwa maendeleo ya biashara zao.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina na unaothibitisha jinsi ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ilivyotekelezwa nchini Tanzania. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, nawaomba wananchi wa Jimbo la Rombo ambao kama alivyosema Waziri mwenyewe kuwa wana macho na masikio, waturudishie tena Mheshimiwa Basil Mramba, hapa Bungeni ili tuendelee kuvuna hazina kubwa aliyonayo kichwani mwake.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kukumbushia madai ya watumishi wa Wilaya ya Hai sio Walimu ambayo bado yapo Wizara ya Fedha ili yaweze kupatiwa ufumbuzi kabla ya kuvunjwa kwa Bunge mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yake. Pongezi hizi ziwafikie wafanyakazi wote wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu zoezi la kuwarudisha kwenye malipo ya pensheni wote waliochukua kwa mkupuo linasuasua, maana bado wafanyakazi wengi hawajaingizwa kwenye mfumo wa pensheni. Je ni kwa nini zoezi hili linasuasua? Ni

vema basi wananchi wakaelezwa sababu hizo na vile vile lini wategemee kupata pensheni zao.

Mheshimiwa Spika, wananchi bado wanapata shida katika kupata fedha za mirathi. Inachukua miaka hadi sita, saba, ili aliyefiwa kupata mirathi hata wakati ambapo taratibu zote za mirathi zinapokuwa zimekamilika, je, tatizo ni nini? Ni vema basi Wizara ikatafiti sababu hizo na kuzipunguza kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 50 mwaka huu wa fedha kwa malipo ya waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rai yangu kwa wafanyakazi ni kwamba wafute kesi yao ili Wizara iweze kuwalipa fedha, kwa upande wa Wizara ni vizuri elimu ya kutosha ikatolewa kwa wananchi kuhusu suala hili ili kusiwe na upotoshaji wa nia njema ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua pia ni sababu gani zinapelekea wafanyakazi waliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki pensheni zao za kila mwezi? Wakala wa mdhamini wa Serikali ulioko Arusha umeshindwa kuwalipa pensheni wastaafu kwa muda mrefu, kwa mfano Ndugu Gasper Francis, c/o Bertha Kayilla, S.L.P. 669, Tabora ambaye hajalipwa pensheni tangu Januari, 2002.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nachangia hoja hii kwa mtindo wa maswali ili Waziri ajibu na kwamba wananchi wasikie kupitia Waziri mwenyewe.

Moja, Waziri amesema kwamba Serikali imekopesha Shirika la Bima fedha bilioni 4 ili Bima ilipe madeni yote ya wateja mara moja. Je, kazi hiyo ya kulipa inaanza lini na ni kweli fedha hizo zitatosha kulipa madeni yote? Nahitaji maelezo.

Pili, nini hatma ya Shirika letu hilo muhimu kwa utoaji huduma kwa wateja?

Tatu, kwa kuwa wastaafu wengi wanalalamika kuwa kiwango cha pensheni bado ni kidogo sana hasa kima cha kuazia, je, Serikali imefanya mipango gani ya kunyanyua kima chao cha chini na nyongeza ya wengine ni kwa asilimia ngapi? Nne, ni kwa nini wastaafu wasilipwe kila baada ya miezi mitatu badala ya miezi sita? Wastaafu wanaomba kulipwa kila baada ya miezi mitatu. Naomba uwafikirie sana suala hili, toa maelezo wasikie wenyewe.

Tano, kwa nini chuo chako cha *IFM* ambacho hutoa masomo ya Stashahada, Shahada na *Masters,* kisiwe rasmi Chuo Kikuu Kishiriki kama vingine? Kwa nini hamkitendei haki? Wizara hii ni kubwa na nyeti sana kwa nini inashindwa kukipa hadhi kamili ya Chuo Kikuu? Naomba maelezo zaidi toka kwako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, napenda kueleza furaha yangu kwa utendaji mzuri wa Wizara ya Fedha hususani wewe mwenyewe Waziri Mheshimiwa Basil Mramba na wasaidizi wako wakuu ndugu Grayson Mgonja, Katibu Mkuu na ndugu Peniel Lyimo, pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Naomba pia kwa kupitia kwako niwapongeze watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuboresha malipo ya wastaafu Serikalini ziendelezwe zaidi, bado upo usumbufu wastaafu kutopata malipo yao kwa wakati. Kwa sasa pia lipo tatizo kwa wastaafu waliorejeshwa kwenye mpango wa pensheni kutojua utaratibu mzima wa kupata haki zao. Nashauri elimu au taarifa jinsi wanavyopaswa kufuatilia mafao yao itolewe, inaonekana ofisi za mapato Wilaya hupokelea malipo yao hawapewi maelezo sahihi.

Mheshimiwa Spika, Fedha kwa Upanuzi wa Chuo cha Mahakama Lushoto, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa malalamiko yangu kwamba pamoja na jitihada zote za wewe Waziri wa Fedha na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, hata baada ya agizo la Rais kwamba Chuo cha Uongozi wa Mahakama kipewe kipaumbele katika kutengewa fedha za upanuzi ili kiweze kuongeza nafasi za mafunzo ya uhakimu lakini kwa bahati mbaya Chuo kimetengewa fedha kidogo sana.

Kwa kuwa Shirika la *NSSF* bado lina nia ya kukiwezesha chuo kujenga majengo ya kutosha na kukifanya Chuo cha Uongozi wa Mahakama kuwa cha Kimataifa kukidhi haja ya majengo na huduma mbalimbali. Naomba Serikali ikubali kutoa dhamana ambayo itaifanya *NSSF* kukubali na kuanza ujenzi wa majengo kulingana na mpango kabambe ambao umekwisha kabidhiwa ofisi yako.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana Serikali kukubali ombi la ufadhili wa Chuo hicho kupitia Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ambalo limekwisha wasilishwa Wizara ya Fedha. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi.Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni tutakapowasikia watoa hoja wakihitimisha hoja yao.

*(Saa 6.30 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikatia Kiti*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nami nitoe mchango wangu kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya Makadirio ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Magu, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, kuwa Mgombea wa Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya CCM, kuwa Mgombea Mwenza. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine, waliofariki dunia wakati na baada ya Bunge la Bajeti la mwaka 2004/2005. Waheshimiwa Wabunge na Viongozi hao ni pamoja na Marehemu Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Marehemu Mheshimiwa *Captain Comrade* Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Waziri katika Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Hayati Paul Bomani, aliyekuwa Muasisi wa CCM na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mtumishi wa siku nyingi wa Serikali na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa. Hawa wametutangulia katika haki, bado zamu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sasa kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Benedict Losurutia na Mheshimiwa Ismail Iwvatta, walitoa hoja kwamba, Wizara iimarishe Ofisi za Fedha kwa kuondoa ukosefu wa vitendea kazi kwa watumishi wa *TRA* Manyoni na Kiteto kama vile magari, samani na majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mapungufu katika utawala wa kodi na ili kuimarisha ukusanyaji wa fedha, Wizara ya Fedha kwa kupitia Mpango Mkuu wa Miaka Mitano wa *TRA,* imepanga kuboresha mfumo mzima wa utawala na ukusanyaji wa kodi ikiwa ni pamoja na kukarabati nyumba na ofisi za mamlaka na kujenga nyingine mpya. Katika huu Mpango Mkuu wa Miaka Mitano, pia Serikali inahakikisha kuwa, nyenzo zote muhimu za kufanyia kazi zinapatikana katika Ofisi zote za Mamlaka, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Manyoni na ile ya Kiteto. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wavute subira, matatizo katika ofisi hizo yatatatuliwa chini ya huu Mpango Mkuu wa Miaka Mitano unaoishia mwaka 2008. Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kwamba, tayari katika sehemu nyingi ofisi nyingi zimeshakarabatiwa kama vile Tunduma, Kasumulu na kadhalika. Hali ilikuwa mbaya sana kwa mfano pale Tunduma, lakini sasa hivi hali ni nzuri. Kwa hiyo, hata Manyoni, pamoja na Kiteto baada ya muda si mrefu hali hiyo itarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, aliuliza maswali kwamba, wafanyakazi wa kigeni wa Mashirika ya Dini wanastahili kulipa kodi ya mapato, pia, ni kwa nini kwenye baadhi ya Mikoa wanatozwa kodi na Mikoa mingine hawatozwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba, kimsingi mtu yeyote pamoja na wafanyakazi wa kigeni, ambaye ana mapato ya ajira, kutokana na ajira yake humu nchini, anastahili kulipia kodi mapato hayo. Hata hivyo, Serikali imetoa msamaha wa kodi kwa mapato ya ajira ya wafanyakazi wa kigeni wa Mashirika ya Hisani na ya Dini kwa masharti yafuatayo: Mfanyakazi awe anaishi hapa nchini kwa ajili ya ajira hiyo tu; mfanyakazi awe ameajiriwa na Taasisi kwenye Mradi wa Elimu, Afya ama huduma nyingine za jamii; Mradi uwe umeidhinishwa na Wizara husika na mshahara wa mfanyakazi uwe unalipwa kwa kutumia fedha zinazotoka nje ya nchi. Kwa sababu msamaha huwa una masharti, hivyo unatolewa baada ya kutimiza masharti haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, ni dhahiri kwamba, kutakuwa na stahili ya kodi tofauti kati ya *expatriates employees* wa Mashirika ya Dini, si tu kati ya Mikoa tofauti, bali hata kati ya wafanyakazi tofauti wa Taasisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda; Mbunge wa Njombe, aliuliza na kutoa hoja kwamba, ili kupunguza upotevu wa mapato yatokanayo na *VAT,* Serikali iweke utaratibu ambao risiti za mauzo zitatolewa kwa njia ya mashine badala ya kuandikwa kwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *VAT* inawataka wafanyabiashara wa rejareja waliosajiliwa *VAT* watumie mashine zijulikanazo kama *electronic cash registers* katika kutoa risiti kwenye mauzo yao ya bidhaa au ya huduma. Pia, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, amepewa uwezo wa kisheria kumuamuru mfanyabiashara yeyote, hata asiyeuza rejareja, kutumia mashine hizo endapo ataridhika kufanya hivyo kwa ajili ya kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali. Ili kuhamasisha wafanyabiashara wanamudu kununua mashine hizo, Serikali imeondoa ushuru wa forodha, pamoja na wa *VAT* kwenye uingizaji na ununuzi wa mashine hizo. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri, hivyo Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, itaendelea kusimamia kwa karibu ili kuhamasisha na kuhakikisha kuwa, wafanyabiashara wote wanatoa risiti kwa kutumia mashine za *electronic cash registers. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, alizungumzia kuhusu *Air Tanzania Corporation Limited.* Wizara ya Fedha kama mhisani wa Serikali kwa asilimia 51 katika Shirika hili, imeendelea kuwasiliana na wahisani wenzetu, yaani *South African Airways,* ili kuboresha zaidi mtaji wa Kampuni na uendeshaji wake. Katika kutekeleza azma hiyo, tayari Serikali na *South African Airways,* wamekubaliana kimsingi kuhusu namna gani wataweza kupanua na kuboresha huduma zinazotolewa na Kampuni hii, ikiwa ni pamoja na kuongeza mtaji ambao toka Shirika lianzishwe mtaji wake ulikuwa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, alizungumzia hatua za ubinafsishaji wa *NMB.* Taratibu zote za kubinafsisha Benki hii zimeishakamilishwa na *PSRC.* Wizara ya Fedha, imeandaa Waraka kuwasilisha rasmi mapendekezo ya Serikali ili hatimaye mwekezaji kiongozi aliyepatikana aweze kutangazwa rasmi na hatua za ununuzi wa hisa ambazo ni asilimia 49 katika Benki zikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Utaani, walitoa hoja kwamba, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya nini hadi sasa na mbona haijatoa taarifa? Kwa mujibu wa ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ina jukumu kuu la kuchambua mapato, matumizi na mfumo wa fedha wa Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili. Hadi kufikia Juni, 2005, Tume imefanya uchambuzi wa mambo yafuatayo na kupeleka mapendekezo yake Serikalini:-

(a) Majukumu, muundo, ikama na viwango vya mishahara kwa watumishi wa Tume.

(b) Mapitio ya Sheria Namba 14 ya mwaka 1996 iliyounda Tume kwa lengo la kubaini mapungufu yake na kupendekeza marekebisho.

(c) Kanuni za fedha, utumishi na uendeshaji wa Tume; na

(d) Zanzibar kujumuishwa kisheria katika kukusanya ushuru wa bidhaa.

Uchambuzi wa masuala yafuatayo unaendelea na uko kwenye hatua mbalimbali:-

(a) Vigezo vya kugawana mapato na matumizi ya mambo ya Muungano;

(b) Utambuzi wa Asasi za Muungano na gharama za kuendesha Asasi hizo; na

(c) Madeni baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na uchambuzi huu unakusudiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Baada ya kukamilika, Tume itatoa mapendekezo yanayostahili Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Margareth Mkanga, alitoa hoja kuhusu mchango wa *Gaming Board of Tanzania* kwamba, ni kwa vipi michezo ya kubahatisha inachangia katika michezo ya walemavu? Sheria Namba 4 ya mwaka 2003 iliyoanzisha Bodi ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha Tanzania, inawataka waendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa kuchangia katika maendeleo ya michezo nchini. Kiasi hicho ambacho ni sawa na nusu ya kodi, yaani *gaming tax* inayolipwa na waendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa, hulipwa kwa Baraza la Michezo Tanzania kupitia Bodi ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi imekwishatoa leseni mbili za kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa, hadi kufikia tarehe 19 Julai, 2005. Leseni hizo ni kwa ajili ya *lotto* ambayo imeanza tarehe 14 Mei, 2005 na *SMS lottery,* ambayo inatarajia kuanza shughuli zake katikati ya Septemba, 2005. Hadi kufikia Juni 30, 2006, Taasisi hizo mbili zinategemewa kuchangia shilingi za Tanzania milioni 283 kwa ajili ya kuendeleza michezo nchini. Tunatarajia kwamba, Baraza la Michezo la Taifa, litatenga kiasi fulani katika fedha hizo ili kuendeleza michezo kwa walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, alitoa hoja kuhusu Chuo cha Sheria cha Lushoto kutengewa fedha nje ya *ceiling* kwa ajili ya ujenzi wa majengo na miundombinu mingine muhimu ya chuo. Serikali imelipokea suala hilo na litawekwa katika mipango ya Serikali ya kuendeleza Sekta ya Sheria. Aidha, Serikali inaandaa taarifa ya kupeleka kwenye Kamati ya Taifa ya Mkakati wa Kudhibiti Madeni ili suala hili la kukiwezesha chuo kupata udhamini toka Serikalini chini ya Sheria ya *Government Loans and Guarantee of 2003,* liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, kama mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, kuhusu ajira ya Wazanzibari Benki Kuu katika ngazi ya Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi. Ajira ya Benki Kuu huzingatia stahili, ujuzi na uwezo. Ujuzi na uwezo wa mwajiriwa mtarajiwa, huchambuliwa wakati wa usaili. Aidha, usaili hufanywa baada ya matangazo ya nafasi za kazi Benki Kuu kutolewa katika Vyombo vya Habari vinavyosambazwa Bara na Visiwani na waombaji hujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu haiajiri Wakurugenzi au Manaibu Wakurugenzi wake kutoka nje ya Benki Kuu kutokana na hoja ya kuwa na uzoefu na ujuzi wa kazi katika ngazi hizo. Hii ni kuzingatia kuwa, kazi zifanywazo Benki Kuu ya nchi yoyote ile ni za pekee, kwani Benki Kuu huwa ni moja tu kwa kila nchi. Waajiriwa wa namna hii, hupandishwa vyeo kutokana na ubora wa kazi zao na mfanyakazi akifikia kiwango cha *Principal Officer,* huweza kufikiriwa kusimamia idara kama Naibu Mkurugenzi ikiwa nafasi itajitokeza. Ifahamike kuwa, haiwezekani kila mfanyakazi wa Benki Kuu, hata akiwa *Principal Officer,* awe Mkuu wa Idara *(Deputy Director).* Wakurugenzi huteuliwa kwa kupandishwa vyeo kutoka Manaibu Wakurugenzi. Nafasi nyingi za Ukurugenzi na Unaibu Ukurugenzi, haiwezekani kuajiri toka nje ya Benki Kuu, kwa sababu mafunzo na uzoefu wa kazi za Benki Kuu ni wa pekee na hauwezi kupatikana nje ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitolewa hoja juu ya ongezeko la fedha katika uchumi na Taasisi za Fedha. Ni kweli katika miaka kama kumi iliyopita, kulikuwa na fedha nyingi za amana katika mabenki hapa nchini, zilizofikia zaidi ya shilingi bilioni 400, ambazo zilikuwa hazichangii kwa kiasi kikubwa kutoa mikopo kwa Wananchi. Hata hivyo, baada ya Serikali kuboresha hali ya uendeshaji wa Sekta ya Fedha, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mifuko ya Udhamini wa Mikopo *(Credit Guarantee Schemes),* kumekuwepo na ongezeko kubwa la utoaji wa mikopo kwa Sekta Binafsi. Aidha, utoaji wa mikopo hiyo umekuwa ukiongezeka kwa zaidi ya asilimia 30 kwa

mwaka. Hali hii imepunguza sana kiasi kinachokaa bure cha limbikizo la fedha katika mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Waziri wa Fedha, aliunda Kamati ya Wadau Wakuu wa Sekta ya Fedha chini ya Uenyekiti wa Gavana wa Benki Kuu na Wajumbe kutoka Wizara ya Fedha Bara na Visiwani, Sheria, Ardhi, Utumishi, Ushirika na Masoko na Vyombo vya Fedha, pamoja na Mifuko ya Pensheni na Sekta ya Bima. Kamati hii imepewa jukumu la kusimamia maandalizi na utekelezaji wa awamu ya pili ya marekebisho katika Sekta ya Fedha. Mabadiliko haya yanalenga katika kuifanya Sekta ya Fedha, itoe mchango mkubwa zaidi katika ukuaji wa uchumi na kufuta umaskini nchini. Sekta zote zitaguswa na mabadiliko haya ikiwa ni pamoja na Mabenki, Mashirika ya Pensheni, Bima, Masoko ya Mitaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya masuala yanayoangaliwa ni kuandaa Sera Bora ya Uwekezaji wa Fedha za Mifuko ya Pensheni itakayowezesha fedha hizi kutumika kwa ufanisi ili ziongeze kasi ya kufuta umaskini. Suala lingine muhimu linaloangaliwa ni kuona jinsi ya kuongeza Wanachama wa Mifuko hii ili kuwashirikisha wazalishaji ambao si waajiriwa wa Serikali au Mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ismail Iwvatta na Mheshimiwa Paschal Degera, waliuliza kwa nini Shirika la Bima linashindwa kulipa madai kwa wateja wao na hivyo kusababisha kero? Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993, Shirika la Bima la Taifa, lilitoa kinga kwa majanga mbalimbali na pia kuchangia Pato la Taifa kwa kipindi chote hicho hadi mwaka 1996, Sheria ya Bima ilipobadilishwa na kuruhusu biashara huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitisha Sheria mpya ya Bima Namba 18 ya mwaka 1996, Bunge lilitoa msamaha wa miaka miwili ili kuliwezesha Shirika kufanya marekebisho ya kiutendaji na yale ya kimuundo ili lipate kushindana na Makampuni Binafsi kwenye biashara huria, kwani pasipo kufanya hivyo Shirika lisingehimili ushindani. Hata hivyo, msamaha huo haukulisaidia sana Shirika kwani biashara yake nyingi kiasi cha asilimia 60 ilikwenda kwenye Makampuni Binafsi. Hali hii imelisababishia Shirika ugumu wa kulipa madai ya wateja wake inavyotakiwa na hivyo kuathiri utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa kulinusuru Shirika ni pamoja na kuuza vitega uchumi vyake na pia Serikali inaendelea kuliandaa kwa ajili ya ubinafsishaji. Serikali imetoa mkopo wa shilingi bilioni nne kwa ajili ya kulipia madai ya Bima za Maisha, wakati yale madai mengine yanaendelea kulipwa kwa utaratibu wa kuuza mali za Shirika. Taarifa za ukaguzi wa mali na vitega uchumi vya Shirika la Bima la Taifa, zinaonesha kuwa Shirika hilo lina uwezo wa kulipa madai yake yote pindi juhudi hizi zitakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Chubi, alitoa hoja kuhusu kesi za waliokuwa wafanyakazi wa Shirika la Bima na alitaka kujua Waziri ana mpango gani kuhusu wafanyakazi 200 wa Shirika la Bima la Taifa, ambao walishinda kesi kuhusu

mafao yao, lakini Menejimenti ya Shirika la Bima la Taifa imekataa kuwalipa kwa kuendeleza rufani mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi iliyofunguliwa Mahakama ya Kazi Namba 52 ya mwaka 2002, inasubiri uamuzi unaotegemewa kutolewa tarehe 28 Julai, 2005. Kesi hii inahusisha wafanyakazi wote wapatao 1,163 akiwemo Mheshimiwa Omar Chubi, dhidi ya Shirika. Jumla ya mafao yanayodaiwa kulipwa ni zaidi ya shilingi bilioni 55. Kwa kuwa kesi haijaisha, itakuwa siyo sahihi kwa Shirika kufanya malipo kwa mdai yeyote, akiwemo Mheshimiwa Omar Chubi. Hata hivyo, Wizara itaunda Kamati itakayochunguza madai ya Mheshimiwa Omar Chubi na kumshauri Waziri ili alipatie suala la Mheshimiwa Mbunge ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za Menejimenti ya Shirika la Bima la Taifa kubadilika kutoka katika ajira ya muda mrefu na kuwa mikataba ya miaka mitatu mitatu, jibu ni kwamba, katika kipindi cha mpito kuelekea ubinafsishaji, Wizara kwa kushirikiana na *PSRC,* imekuwa ikifanya marekebisho mbalimbali ndani ya Shirika ili kuleta ufanisi mahali pa kazi, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji. Marekebisho haya yanaendelea ili kuliweka Shirika katika hali nzuri tukiwa tunasubiri kulibinafsisha. Hata hivyo, hakuna kiongozi yeyote wa Shirika la Bima la Taifa, ambaye amelipwa mafao ya kustaafu hadi leo katika zoezi hili.

Kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Magu na kwa niaba yangu binafsi, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri aliyoifanya akiwa kama Waziri wangu, amenifundisha kazi vizuri na ninaamini kwamba, amefundisha watu wengi wakiwemo Wabunge ambao wamo ndani ya Bunge hili. Pia, ninapenda nishukuru ushirikiano nilioupata kutoka kwenye Wizara ya Fedha kwa ujumla na ni matumaini yangu kwamba, Wananchi wa Jimbo la Magu, watanirudisha kwa kishindo tena katika Bunge hapo Oktoba, 2005 na ninaamini kwamba, wana macho na wana masikio na kazi zangu wameziona Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninamshukuru vile vile Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, kwa majibu yake mazuri kwa niaba yangu. Nafikiri ameturahisisia sana kazi na kwa hiyo, nitajitahidi kwa haya yaliyobaki. Nafanya hivyo kwanza, kwa kutambua michango ya Kamati ya Fedha, ikiongozwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka na wenzake waliosoma na kufanya kazi hiyo kwa niaba, kadhalika Kambi ya Upinzani. Nami nimefarijika zaidi kwa sababu nadhani leo ilikuwa mara ya kwanza, kwa miaka yote ambayo nimefanya kazi hapa, kwa moyo mkunjufu na kwa uadilifu na sifa zote, alizomwaga Mheshimiwa Omar Chubi kwamba, Kambi ya Upinzani leo imeona ni vema na haki kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Kambi ya Upinzani kwa sababu sasa nakubali walivyosema kwamba, wanaangalia maslahi ya Taifa zaidi kuliko itikadi. Ndugu yangu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, yupo na anajua ninavyosema ni

kweli. Kwa hiyo, ninawatakia Wapinzani kila la kheri, lakini na mimi najitakia kheri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia hoja yangu baada ya hao wawili wa upande wa Upinzani na upande wa Kamati ya Fedha, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mheshimiwa Profesa Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Semindu K. Pawa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, ambaye pia ameniletea barua kutoka kwa Wazee wa Songea, kupeleka kwa Mheshimiwa Rais, kumshukuru kwa kazi nzuri ya kuwakumbuka Wazee. Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, napokea barua hiyo na nitaishughulikia, nimeshaelewa inasema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Omar S. Chubi, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta na Mheshimiwa Anne S. Makinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wote nawashukuru kwa mawazo yao mazuri, ambayo baadhi nitayachukua na ningependa hasa kuanza na ushauri wa Mheshimiwa Monica Mbega na Mheshimiwa Anne Makinda, kuhusiana na masuala ya pensheni. Ushauri huo nitauchukua na nitaufanyia kazi, angalau niuweke kwenye mstari kabla ya mwisho wa mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli ungeweza ukasema kwamba, kwenye mjadala wa leo suala kubwa lilikuwa ni la malipo ya uzeeni (pensheni). Ni kubwa kwa sababu linahusu watu wengi na watu wazima ambao wameitumikia sana Serikali yetu. Kwa pamoja nitajaribu kuwajibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi Hazina tunaelewa kwamba, hili tatizo ni kubwa na linasumbua. Kwa pensheni za kawaida za watumishi wa Serikali, tumeanzisha Shirika *PSPF,* ambalo linahudumia kisasa kabisa wafanyakazi wastaafu wa hadi miaka miwili iliyopita. Kabla ya hapo, ndiyo hao tunaoendelea kuhangaika nao, hao waliokuwa wanatajwa hapa kwamba barua hazionekani, mafaili hayaonekani, wenyewe pia mara nyingine uelewa wao siyo mkubwa, mara cheki zinaenda mikoani, lakini wao wanadhani ziko Dar es Salaam, wanazifuata Dar es Salaam na mambo mengi yanayosumbua kama matatizo ya mirathi, mtumishi anafariki, lakini ukoo unampa urithi mtu mwingine na yule mtu mwingine wala haelewi sawa sawa marehemu yule hasa alikuwa ana haki gani na kadhalika, ni mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa niseme tu kwamba, tumekuwa tukiyashughulikia. Waajiri wahusika wamekuwa wakipelekewa barua za kuomba nyaraka, wengine wanajibu na wengine hawajibu. Nyaraka nyingine hazipatikani na zinachukua muda mrefu maana Hazina wamekuwa wakifuatilia kabisa kwa kuwafuata

watu mikoani kufuatilia nyaraka hizo, mara nyingine zinapatikana na mara nyingine hazipatikani. Kwa kweli tatizo hili tumekuwa tukilishughulikia, lakini bado linaendelea kujitokeza. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi upya. Ni lazima sasa tuketi, tufikiri njia nyingine bora zaidi. Hii njia ya kusema kuwe na *cutoff point* ina maana gani, *implications* zake ni nini na njia nyingine nyingi, ili labda tukifika mwakani tuwe na njia ambayo inatekelezeka vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya majibu ambayo yatapatikana ni kuhusu kima cha chini cha pensheni. Sasa hivi najua kwamba, tumewaondoa wastaafu kutoka chini sana tukafika Sh.20,000/=, lakini tunajua kwamba, hazitoshi. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kufanya kazi zaidi. Tunajua kwamba, wastaafu hawa wangeweza wakalipwa kule kule. Kwa hiyo, kuanzia mwakani wastaafu watakuwa wanalipwa kwenye ofisi zetu zote za Hazina Ndogo, ambazo ziko mikoani na maswali yao mengi yataulizwa huko huko kwenye Hazina Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba, kuna maombi na ni kati ya maombi yaliyotoka Songea pia kwamba, kwa nini watu wasilipwe kwa muda mfupi zaidi badala ya miezi sita sita, labda iwe miezi mitatu mitatu. Nami pia nafikiri kwamba, hilo linawezekana na mwakani naamini kabisa kwamba, tutakuwa tunalipa kila baada ya miezi mitatu mitatu, siyo miezi sita. Kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote na Wananchi kwa ujumla kwamba, tutajitahidi kufanya shughuli hii ya pensheni iwe nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo lingine ambalo nilijibu hapa wakati wa Bajeti kwamba, kuna watu wanaosema wale wanaostaafu leo wanalipwa vizuri zaidi kuliko waliostaafu miaka michache iliyopita. Hilo nalo ni tatizo tunalo. Kwa hiyo, tutayaunganisha yote haya na kuona ni kitu gani tunachoweza kufanya.

Lakini siri yake ni ukusanyaji wa kodi. Nimefurahi sana wale waliokuwa wanashauri hapa. Kama nilivyosema kuna kodi, kama Wananchi wangefanya yale aliyokuwa anatushauri Mheshimiwa Anne Makinda, kwamba hata kibanio, hata *pencil* inalipiwa kodi kwa maana ya kusema ukishanunua unapewa risiti na ile kodi, inawekwa pale maana yake ile bei unayolipia lazima na fedha ya *VAT* iko pale, hii ingesaidia sana. Lakini Watanzania kwa bahati mbaya sana, hatuna tabia ya kudai risiti. Wenye maduka wanafanya hii ndiyo biashara, bei kwa risiti, bei bila risiti. Kwa hiyo, wote wawili wanajikuta wanakwepa kodi bila sababu na kisha wanarudi sasa ndiyo wanadai pensheni, wanadai huduma nyingi bila kulipa kodi. Kwa kweli, naomba Wananchi wajitahidi kudai risiti na wenye maduka wajitahidi kulipa. *(Makofi)*

Kwa Dar es Salaam, tumeanza msako kwa kutumia makachelo fulani fulani, kupita kwenye maduka na kuona kama risiti hizi zinatolewa ama hapana. Mwaka 2004, tulifanisha tukapata shilingi kati ya 600 na 800 milioni kwa njia hizo za kufainisha watu kwa kutumia risiti na watu wasiotumia zile *cash register machines,* ambazo zimekuwa zikizungumziwa hapa. Lakini hiyo ni idadi ndogo kabisa ya watu wanaopaswa kulipa kodi. Hata hizo *cash register machines* ambazo duniani kote zinatumika, hapa kwetu hata

wenye maduka hawazinunui na wakizinunua hawazitumii. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana ya kuelimisha Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kurudia tena hili suala la *NIC* na nakubaliana na Mheshimiwa Omar Chubi, pendekezo lake kwamba, labda tuangalie tuunde hata tume au kamati ya kuangalia namna ya kushughulikia hili tatizo lililokuweko kule. Mimi niko radhi kufanya hivyo, lakini kwa sababu suala zima liko Mahakamani, itabidi tusubiri tunafikiri labda litakwisha haraka, nadhani kwenye tarehe 28 natumaini labda litaamuliwa halafu tutaangalia tufanye nini. Kwa hiyo, nilichukue kwamba, niko tayari kuliangalia kiraia baada ya kutoka Mahakamani kama litasaidia. *(Makofi)*

Vile vile ningependa kusema kwamba, Shirika la *NIC* liko kwenye utaratibu wa kuboreshwa. Nimetoa maagizo hivi karibuni kwamba, kazi hii ifanywe kwa haraka zaidi ili kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, nadhani alikuwa Mheshimiwa Paschal Degera, tuwe na shirika ambalo linaeleweka na linafanya kazi kama zamani ili liweze kutoa huduma zinazotakiwa. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba, ndani ya miezi michache, Shirika hili litakuwa limeboreshwa na labda haya matatizo ya hofu zilizoko kwa wateja na hasa wateja wa Bima za Maisha, yatakuwa yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la wadai wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, nirudie tu kwa kusema kwamba, hakuna ujanja, wala udanganyifu, wala kuchengachenga, wala wasiwasi, kwa upande wa Serikali. Kinachoendelea ni watu fulani fulani, kwa sababu zao wenyewe, wanataka kulifanya jambo hili liwe kubwa. Hakuna jambo lolote litakaloharibika, maana ukitaka kuelewa inakuwaje Rais wa Nchi anatamka kwamba nitalipa, hili ndiyo la msingi alisema nitalipa hata kama itakuwa ni baada ya mimi kuondoka. Ile aliyonisomea hapa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ndivyo inavyosema, nitaanza kulipa. Rais alisema nitaanza kulipa nikiwa madarakani na ndicho tunachofanya, tutaanza kulipa, hakusema tutamalizia. *(Makofi)*

Nashukuru sana kwamba, ni upande wa Upinzani ndiyo umesoma kabisa kauli ya Rais kwamba, tutaanza kulipa. Nashukuru sana ni *CUF* ndiyo wanaosema na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mahesabu ya Serikali ndani ya Bunge, ndiyo anayesema Rais alisema tutaanza na tunaanza na mwezi wa nane tutaanza kulipa. Mimi niseme hapa, tutalipa kwa uwazi na ukweli, kwa kutangaza kwenye magazeti na tutaanza na shilingi 50 bilioni. Sisi tunafikiri kwamba, zile shilingi 50 bilioni zinatosheleza kabisa kwa mahesabu yetu. Kama zisipotosheleza tutalipa na tunaanza, si hesabu zipo. Mimi kama nilivyosema hapa, wako maofisa 30 waliobobea, kazi yao toka asubuhi mpaka jioni na Jumamosi na Jumapili ni ukokotoaji. Serikali haiwezi kulipa bila kukokotoa, ni ukokotoaji hilo la kwanza.

La pili, hizi fedha shilingi bilioni 50 ziko kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha, ziko hapa leo ndio naomba muidhinishe. Kwa utaratibu wa Serikali siwezi kulipa hata senti bila nyie kuidhinisha na ziko ndani ya Wizara yangu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mkiidhinisha na ukokotoaji uko tayari unaendelea, mwezi ujao naanza kazi kwa kutangaza. *(Makofi)*

Sasa sielewi mgogoro uko wapi, kila siku nikijaribu kupata usingizi wanasema Mramba, Mramba, Mramba nimefanya nini? Mimi natoa hela halafu wananilaumu! Ohoo mbona Rais atatoka, Rais yupi, nataka mtu yeyote anyooshe mkono au aseme ni Rais yupi alisaini *cheque* ya Serikali. Aniambie mimi nilipokuwa fulani, Rais Nyerere alisaini *cheque* yangu, Rais Mwinyi alisaini *cheque* yangu, Rais Mkapa hajasaini *cheque.* Marais hawasaini *cheque,* hii ni kazi ya wadogo zaidi. Mbona wanafikiri Rais wewe ni Ofisa. Hata mimi hapa sisaini *cheque,* kuna wadogo zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Watu wanafikiri Rais ndiyo atafanya kazi zote, ndiyo maana ana wasaidizi chungu nzima 300,000 ndani ya Serikali na zaidi kwenye Mashirika wanamsaidia. Kwa hiyo, kazi yangu ni kuamua kwa niaba ya Rais na kuleta mambo hapa Bungeni, mnaamua mkiridhika na mambo kama vile ambavyo mmesharidhika yaliyobaki ni watendaji tu.

Nimeshukuru sana kwamba, Waheshimiwa Wabunge, wamelielewa, nilishalimaliza zamani kwa hiyo, kilichobaki ni kulipa na mimi nataka kuwahakikishia kwamba, nitasimamia ulipaji huo na hata kama nikiondoka atakuja mwingine. Serikali hii haifi wala haiendi yote kwenye kura, Watumishi wa Serikali hawako kwenye tarehe 30 Oktoba, wanaendelea, hata wakibadilika wanakuja wengine, hata wakistaafu hawa walioko wanakuja wengine. Kwa hiyo, Serikali ipo na italipa. Hii ndiyo kauli kubwa kuliko zote ambazo tunataka watu waelewe. Wasiwe na wasiwasi, hakuna Rais, anayesaini *cheque,* wala Waziri wa Fedha anayesaini *cheque*. Siyo ndani ya Tanzania, labda kwenye nchi zile ambazo zinaitwa *Banana Republic,* siyo *Republic* ya Tanzania hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia tena Wananchi, watupe nafasi tufanye hii kazi, wapunguze kelele ambazo kwa kweli hazina maana. Nashukuru kwamba, tuko na wanakamati na wale wanaohusika na jambo hili na tumeelewana, tumeshafanya vikao, tunaelewana, tunaendelea na kazi ya kukokotoa ili kupata hesabu kamili, kwa sababu senti ya Serikali haitoki mpaka hapo itakapothibitishwa, la sivyo nitakuja tena hapa mkinilaumu kwamba, nimekuwa mbadhirifu katika matumizi ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru wanaanza kuelewa mambo ya Mifuko ya Udhamini. Mifuko ya Udhamini imeanza ni miaka miwili toka tuanze, iko mitatu kama nilivyoeleza. Huo mmoja hasa ule uliokuwa unadhamini Vyama vya Ushirika, ili wanunue mazao waweze kuuza nje, ndiyo tulianza nao kwa sababu ya umuhimu wa kushughulikia mazao. Lakini baadaye kuanzia mwaka huu, tumekuwa na mfuko mwingine unaohudumia viwanda vidogo na shughuli ndogo ndogo, huo tayari masharti yameshakamilika, taratibu zake za kisheria zimeshakamilika, tuko tayari kuanza kudhamini. *(Makofi)*

Uko Mfuko mwingine wa tatu wa kudhamini Mashirika makubwa, yanayotaka kuuza nje. Mfuko ule nao umeungwa mkono na Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia kwamba, tunaweza sasa tukadhamini watu wanaotaka kuuza nje mazao yao makubwa, yaani kama nguo, bidhaa za viwandani, bidhaa za kilimo na kadhalika. Toka shughuli hii ianze mwaka 2003, Vyama vya Ushirika 17 vilidhaminiwa kwa jumla ya

shilingi bilioni 6.7. Mwaka uliofuata (2003/2004), Vyama vya Ushirika 19 na Kampuni ya *Pyrethrum* kule Mufindi, ambayo inashughulikia zao la pareto na mashamba ya maua kule Arusha, jumla ya shilingi bilioni 7.5. Mwaka huu uliopita ni Vyama vya Ushirika tisa na baadhi ya mashamba ya maua kule Arusha na viwanda, kwa mfano, *Morogoro Canvas Mill* na Kiwanda cha Tumbaku na mashamba. Kwa hiyo, Serikali iko makini kufanya jambo hili, kwa sababu tunataka Benki zetu zipate ari ya kukopesha shughuli za uchumi ndani ya nchi kwa kujua kwamba, wale wasipolipa, kuna mtu atakayekuwa amekwisha wadhamini. Kazi hii, itaendelea na nafikiri ni jambo zuri kwamba, tufanye hivyo kwa sababu ndiyo namna ya kuendeleza uchumi wetu. *(Makofi)*

Hii Tume ya Pamoja ya Fedha imezungumzwa hapa na Naibu Waziri, amenisaidia kujibu. Lakini niseme kitu kimoja, ningependa wenzetu wanaojaribu kufuatilia jambo hili, waelewe kwamba, kuna kazi ambayo imekuwa ikiendelea. Kwa mfano, Tume ile imekuwa ikishughulikia majukumu na muundo wa Tume yenyewe, mapitio ya Sheria Namba 14 ya mwaka 1996 iliyounda Tume hiyo na kubaini mapungufu kama yako, kanuni za Fedha, Utumishi na uendeshaji wa Tume yenyewe na namna ya kujumuisha Zanzibar kisheria katika kukusanya ushuru wa bidhaa.

Hivi sasa uchambuzi unaendelea wa masuala mbalimbali, kwa mfano, vigezo vya kugawana mapato na matumizi ya mambo ya Muungano, utambuzi wa asasi za Muungano na gharama za kuendesha asasi hizo, madeni baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Inategemewa kwamba, uchambuzi huu utakamilika ikifika mwisho wa mwaka huu.

Ningependa ieleweke kwamba, tusiwe na matumaini sana kwamba, labda kuna kitu ambacho upande mmoja wa Muungano umekuwa ukipunjwa. Hivi sasa tunagawana misaada kutoka nje kwa asilimia 4.5. Kuna watu wanaosema asilimia 4.5 ni nyingi mno, kwa sababu ukienda kwa idadi ya watu, Zanzibar ni asilimia 2.6 ya idadi ya watu wa Muungano. Kwa hiyo, haki yao ingekuwa asilimia 2.6. Kwa hiyo, sasa sisi tumekubaliana wakati ule, asilimia 4.5, nasema acha Tume ifanye kazi. Mheshimiwa William Shellukindo, namwona pale, ndiyo Mwenyekiti ananisikiliza kwa makini. Ametembelea nchi nyingi duniani kama Australia, Scotland, India, zenye Muungano wa namna hii na kuona kule wanalipanaje. Watachukua Elimu waliyoipata, mazingira halisi ya humo ndani na kupendekeza Serikalini mfumo na viwango ambavyo vitasaidia katika kugawana mapato ya Muungano. Tuwasubiri wamalize hizi kazi, hivi sasa kuna taarifa ya muda na baadaye wataleta taarifa kamili, nafikiri kwamba, taarifa hiyo ndiyo itakayojadiliwa na ndiyo itakayoweza kutupa jibu la kudumu. Nasisitiza kwamba, tunatafuta jibu la kisayansi, siyo jibu tu ambalo si la kisayansi. *(Makofi)*

Mwisho, kuna swali limeulizwa juu ya mishahara ya Watumishi wageni, wanaofanya kazi ndani ya nchi yetu na hasa kwenye Mashirika ya Dini. Niseme tu, Serikali imetoa msamaha wa kodi kwa mapato ya ajira ya Wafanyakazi wa kigeni wa Mashirika ya Hisani na ya Dini kwa masharti yafuatayo: Mfanyakazi awe anaishi hapa nchini kwa ajili ya ajira hiyo tu; mfanyakazi awe ameajiriwa na Taasisi kwenye mradi wa elimu, afya au huduma zingine za kijamii; Mradi wenyewe uwe umeidhinishwa na Wizara husika na mshahara wa mfanyakazi uwe unalipwa kutumia fedha zinazotoka nje

ya nchi. Kama mshahara unatoka nje hakuna kodi, kama ni wa hapa lazima atalipa kodi. Kwa sababu hiyo, ni dhahiri kutakuwa na stahili ya kodi tofauti kati ya Wafanyakazi wa nje wa Mashirika ya Dini, si tu kati ya Mkoa tofauti bali hata kati ya Wafanyakazi tofauti ndani ya Taasisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimalizie kwa kuwashukuru, kwa moyo wa dhati, Waheshimiwa Wabunge, kwa namna walivyokuwa wananielewa. Najua kule mwanzo ilikuwa vigumu kunielewa kwa sababu nilikuwa mpya, lakini muda kwa muda wameendelea kunielewa na mimi pia nimeendelea kuwaelewa.

Ningependa niseme kama nilivyosema kwenye Hotuba ya Bajeti kwamba, Wizara ya Fedha, imefaidika sana na michango ya Waheshimiwa Wabunge na hasa Kamati ya Fedha kwamba, bado sisi kule tunafikiri kuna mambo hatujafanya, lakini kwa nje nashukuru mnaona mambo mazuri, sisi kule ndani sisi tunaona bado kuna kazi kubwa za kufanya. Moja kwa mfano ni hii ya pensheni, bado sisi hatujaridhika kule ndani na hali ya pensheni kwa viwango kwa namna tunavyolipa, namna tunavyohudumia, moja ni hilo. Ungeniuliza kazi ambayo hatujafanya vizuri ni hilo. *(Makofi)*

Yako mambo mengine ya sera za fedha, kwa mfano, inakuwaje hapa Tanzania kila kitu kinanunuliwa kwa *cash* na duniani kote watu wananunua vitu kwa utaratibu mwingine. Kwa hiyo, yako mambo ya namna ile ambayo yamebaki na mengine mengi tumaini langu ni kwamba, mbele ya safari, Wizara ya Fedha, itaendelea kuyashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tena hoja kwamba, hoja yangu ya Bajeti ya *Vote 50* na *Vote* nyingine, sasa ikubaliwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 22 - *Public Debt and General Services***

Kif. 1011 - *Administration and General* ... ... Sh. 523,234,528,000.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3001 - *Public Debt Management* .. ... Sh. 1,021,335,700.00
Kif. 3002 - *Expenditure Management* ... ... Sh. 2,304,870,500.00
Kif. 3003 - *Financial Management* ... ... Sh. 69,706,534,600.00
Kif. 3004 - *Systems and Internal Audit* ... Sh. 8,445,596,500.00

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kif. 3005 - *Sub Treasury Arusha* | ... ... | Sh. | 188,000,000.00 |
| Kif. 3006 - *Sub Treasury Coast* | ... ... | Sh. | 175,996,000.00 |
| Kif. 3007 - *Sub Treasury Dodoma* | ... ... | Sh. | 236,568,700.00 |
| Kif. 3008 - *Sub Treasury Iringa* | ... ... | Sh. | 179,996,600.00 |
| Kif. 3009 - *Sub Treasury Kagera* | ... ... | Sh. | 163,914,700.00 |
| Kif. 3010 - *Sub Treasury Kigoma* | ... ... | Sh. | 179,893,600.00 |
| Kif. 3011 - *Sub Treasury Kilimanjaro* | ... ... | Sh. | 202,940,000.00 |
| Kif. 3012 - *Sub Treasury Lindi* | ... ... | Sh. | 169, 985,500.00 |
| Kif. 3013 - *Sub Treasury Mara* | ... ... ..... | Sh. | 199,990,000.00 |
| Kif. 3014 - *Sub Treasury Mbeya* | ... ... | Sh. | 205,920,000.00 |
| Kif. 3015 - *Sub Treasury Morogoro* | ... ... | Sh. | 349,279,500.00 |
| Kif. 3016 - *Sub Treasury Mtwara* | ... ... | Sh. | 183,813,000.00 |
| Kif. 3017 - *Sub Treasury Mwanza* | ... ... | Sh. | 189,992.700.00 |
| Kif. 3018 - *Sub Treasury Rukwa* | ... ... | Sh. | 201,918,600.00 |
| Kif. 3019 - *Sub Treasury Ruvuma* | ... ... | Sh. | 117,958,700.00 |
| Kif. 3020 - *Sub Treasury Shinyanga* | ... ... | Sh. | 214,987,100.00 |
| Kif. 3021 - *Sub Treasury Singida* | ... ... | Sh. | 193,938,600.00 |
| Kif. 3022 - *Sub Treasury Tabora* | ... ... | Sh. | 174,913,500.00 |
| Kif. 3023 - *Sub Treasury Tanga* | ... ... | Sh. | 199,945,000.00 |
| Kif. 3024 - *Sub Treasury Manyara* | ... ... | Sh. | 179,940,000.00 |
| Kif. 7001 - *Pensions and Gratuity* | ... ... | Sh. | 449,643,200.00 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 - *National Audit Office***

Kifu 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 8,147,420,200.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 8,667,578,100.00

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 50, Programu Na. 10, *Sub-Vote* 1001, Kifungu 250100, *Basic Salaries - Pensionable Posts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningeomba sina kusudi la kuzuia Bajeti, lakini nataka ufafanuzi wa mambo matatu yafuatayo: Kwanza, Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anataja *percentage* za Zanzibar na Bara alisema kwamba, Serikali ya Muungano ina shilingi milioni thelathini na Zanzibar ina kama asilimia mbili. Naaelewa kwamba, anaposema Bara siyo Muungano, Muungano ni Zanzibar na Bara. Kwa hiyo, kwanza hilo asahihishe na aweke rekodi sawasawa.

La pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba vile vile asahihishe kwamba, tunapokataa Kambi ya Upinzani, si kwamba tunapinga kwa sababu hatuangalii maslahi ya Taifa. Tunaangalia sana maslahi ya Taifa na ndiyo sababu tuko hapa kila mmoja kuona kwa kiasi gani Taifa linaweza kufaidika na mchango wake. Hata Wabunge hapa wanapochangia, wakati mwingine wanakuwa na mawazo tofauti kabisa na yale ambayo yanaletwa na Serikali. Yote hayo wanayafanya kwa manufaa ya Taifa. Kwa hivyo, nalo hilo naomba aliweke kwenye rekodi na alisahihishe vile vile. Tuko hapa kwa maslahi ya Taifa. Pale tutakapokubaliana hata pale tunapopingana, sote ni kwa maslahi ya Taifa.

Tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, suala hili la wastaafu wa *East African Community,* nilikuwa nimeuliza maswali kama matano wakati wa hotuba yangu. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri, atajitahidi kuyajibu yale maswali ambayo nimeyauliza. Moja, Mheshimiwa Rais, amesema kwamba, yeye taarifa aliyokuwa nayo madai yalikuwa karibu shilingi bilioni 400 na akasema hizo pesa bado hazijahakikiwa. Leo Waziri hapa amesema wataendelea kulipa na hivi sasa anazo shilingi bilioni 50. Lakini katika *statement* yake vile vile amesema hizo ndiyo hasa ambazo zimehakikiwa na kukubaliwa. Sasa tunataka kauli ya Serikali, hasa ni kiasi gani baada ya Rais kusema katika hotuba yake kwamba ni shilingi bilioni 400 na bado hazijahakikiwa, sasa hizi shilingi bilioni 400 baada ya kuhakikiwa ndiyo zimepatikana shilingi bilioni 50? Hiyo ni kauli ya kwanza ambayo tungehitaji kuipata.

Lakini ya pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, mwaka 1998/99, Serikali iliunda Tume. Punde Tume ikafikia muafaka kwa kuwa deni la wastaafu hawa ni shilingi bilioni 161.3 na alitafutwa hata Mtaalam kutoka *World Bank* kufanya hii kazi, leo tunaambiwa ni shilingi bilioni 30. Tukiangalia thamani ya pesa ya wakati huo na thamani ya pesa wakati wa sasa, hizi shilingi bilioni 50 zinalinganishwa na nini? Nafikiri nalo hilo tungepata ufafanuzi. Halafu ndiyo uliuliza vile vile kuna watu ambao wameshafariki na kadhalika. Serikali inafanya utaratibu gani kwa wale ambao wamefariki na haki zao watapataje?

Nne, tulitaka kujua wako wengine wanaendelea na kazi hivi sasa na je, hatma yao itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata ufafanuzi huo, sina matatizo na Bajeti ya Waziri. Ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, nadhani mimi nilikuwa nazungumza juu ya Muungano. Idadi ya watu ndani ya Muungano dhidi ya idadi ya watu Visiwani. Kwa hiyo, nilikuwa na nia ya Muungano siyo Bara. Kwa hiyo, nakubaliana naye, siyo Bara, ni Muungano *versus* Zanzibar, ndiyo hiyo asilimia. Lakini nilikuwa nasema huu ni ubishi tu ulioko katika suala hili, siyo uamuzi. Ni ubishi tu ulioko na tunasubiri Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo, itupe mwongozo juu ya suala hilo na mapendekezo.

La pili, zile shilingi 400 bilioni ndizo zilizokuwa zimekubaliwa na Kamati ile iliyowakilisha watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Wizara ya

Fedha. Kamati ile ndiyo iliyofikia shilingi 400 bilioni baada ya uchambuzi na hii ndiyo Rais alisema hata mimi naona kuna shilingi 400 bilioni. Hata Rais alisema hivyo. Hii ni tarehe 1 Mei, 2005 kule Songea ndiko Rais aliposema hivyo.

Lakini baadaye sisi HAZINA tumekuja kujua kwamba, haki halisi ya wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, waliofariki na walio hai ni shilingi bilioni 50, kwa kutumia kwanza yale masuala 12 ambayo Serikali iliyakubali. Utakumbuka nilipokuwa najibu hapa nilisema kulikuweko maswali 12, ambayo wote tulikubaliana na Serikali ikakubali. Zile Kamati zilikubaliana na Serikali ikakubali na kulikuweko na maswali mengine manne ambayo hawakukubaliana na Serikali haikuyazingatia katika kuamua.

Kwa hiyo, Serikali, yaani kwa maana ya Baraza la Mawaziri, ikaidhinisha hizo shilingi bilioni 50 kwamba, anzeni kulipa hizo na ndizo nilizoleta kwenye Bunge na Bunge likaidhinisha. Hii shilingi bilioni 50 ndiyo tunayokokotoa sasa ili tujue kila mtu atalipwa kiasi gani awe hai au amefariki na ilifikiwaje, ni utaratibu mrefu wa kimahesabu tu. Kwa mfano, zile fedha za wakati ule lazima ziletwe kwa bei ya sasa. Wakati ule iliwekwa *formula* na yule Bwana Umrichi, ambaye ndiye alikuwa msuluhishi na *formula* ile ikapita kwenye Bunge hapa. Kwa hiyo, kuna sheria yake na ndiyo iliyotumika na ndiyo inayotumika na itaendelea kutumika. Isipokuwa asilimia ile ilikuwa imetajwa na Bwana Umrichi, ambayo ilikuwa walipwe kwa ile *interest* ya asilimia 7.5. Serikali ya Tanzania licha ya kuleta zile hesabu zilingane na leo siyo wakati ule, licha ya kusema hivyo, imeweka pia asilimia zaidi kwenye *interest* ikawa 17.5, kwa nini? Hii ndiyo wastani badala ya saba. Serikali ya Tanzania, *Cabinet* imeweka 17.5 badala ya ile 7.5 kwa kuzingatia kwamba, hii ndiyo ilikuwa wastani wa *Bank Rate* kwa kipindi hicho.

Sasa ni jambo la kitaalam. Mtaalam yeyote anaweza akaangalia na hapa Serikali iko tayari kuleta mtaalam yeyote wa dunia yoyote, kuja kuangalia jinsi hizi hesabu zilivyofikiwa na kushauri. Kwa hiyo, nafikiri ndivyo tunavyoendelea na ndiyo maana nikasema kwanza, tushughulike na hii shilingi bilioni 50, maana shida ni pesa, tushughulike na hii watu waingize hela mfukoni kwanza. Kama kuna maneno tutaendelea kuelewana mbele ya safari. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Lakini kwa vile Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alisema ni vizuri tukaweka rekodi, yaani kumbukumbu sawa, nami napenda nifanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia sote hapa, nikasema kwa suala la mgao, *formula* iliyopo sasa hivi ya asilimia 4.5 ni kati ya Serikali ya Bara na Serikali ya Zanzibar. Napenda niieleze Kamati yako kwamba, hatuna Serikali ya Bara, tuna Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Nimeona hilo nisahihishe kwa sababu ndani yake, kwa kauli hiyo ni kwamba, tuna Serikali tatu. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza, nashukuru kwa ufafanuzi alioutoa Mwanasheria Mkuu, maana sasa Waziri atakuwa ameelewa alichokizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alikuwa na kitu kimoja ambacho hajakiweka sawa, nafikiri ni vizuri akakiweka sawa. Amesema mara hii analipa shilingi 50 bilioni na wataendelea kulipa, kama nimemwelewa vizuri. Lakini wakati huu alitoa *statement* akasema katika kukokotoa ndiyo wamefikia shilingi 50 bilioni. Nimemwelewa vizuri alipokuwa ana-*wind up.* Nafikiri hapo hapajakuwa sawasawa, *the total amount* ni *fifty billion* au *fifty billion* ni kianzio cha kulipwa na tunataka kujua kima halisi ni kiasi gani?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli *the total amount is less than fifty billion. A total amount could be less than fifty billion.* Lakini sisi tumekokotoa shilingi 50 bilioni tukafikiri ndiyo fedha zenyewe na ndizo tunafikiri tutalipa na zikishatumika hakuna atakayebaki akidai. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu la 50, Programu ya 10 na *Sub-Vote* 1001. Naomba niulize swali tu na namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anifafanulie. Wakati nilipokuwa nachangia, nimeeleza kilio cha wateja wa Bima waliokata Bima za Maisha. Nimesema hivi, katika Wilaya ya Kondoa kuna zaidi ya walimu 200 walichukua Bima za Maisha kwa malengo mbalimbali na hizo Bima zimekwishaiva miaka mitano iliyopita, wengine miaka miwili, mitatu, iliyopita. Kisheria baada ya Bima za Maisha kuiva walitakiwa walipwe mara moja. Lakini sasa Shirika hili limekalia haki za hawa watu. Bima ni sawa sawa na kuweka Benki. Ingekuwa ni ajabu sana unaweka akiba Benki halafu unakwenda kuambiwa kwamba pesa zako hazipo. *(Kicheko)*

Sasa hii ndiyo inayofanyika kwenye Bima hii. Wewe unadunduliza halafu unamwambia hazipo. Sasa tunafanya nini. Hawa walimu wangu wameweka kwa nia mbalimbali, wengine kusomesha, wengine kujenga nyumba, wengine walitaka kufanya biashara na malengo mbalimbali. Sasa tumewakwamisha, ningeomba Waziri anipe jibu. Ni kwamba, hawa wanatakiwa walipwe mara moja. Wala tusiseme kwamba, tupeni muda kwa sababu pesa zao zipo. Zimepelekwa wapi? *(Kichoko)*

Naomba nipewe maelezo ili niende nikawaambie wapiga kura wangu kwamba, watalipwa lini. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mheshimiwa Paschal Degera, awaambie walimu wake kwamba, hata leo tunavyozungumza, Shirika tayari limekwisha tangaza malipo hayo. Hata leo tunavyozungumza. Kwa hiyo, walimu hawa wanalipwa mara moja. Hiyo, fedha ni ipi, ni ile niliyosema hapa kwamba, nililikopesha Shirika shilingi bilioni nne na wengi wa hawa watu wanaodai hizi bima za maisha wengi wao ni walimu. Kwa hiyo, watalipwa mara moja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 50, Programu 10, *Sub-Vote* 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia asubuhi, sikuunga mkono hoja kwa ombi ambalo nilitoa kwa Mheshimiwa Waziri. Lakini nataka kuthibitisha sifa zile ambazo nilimwagia Waziri, kulingana na majibu aliyonipa sasa hivi. Kwa hiyo, naunga mkono. *(Kicheko/Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .... .... Sh. 4,500,404,800.00
Kif. 1004 - *Legal Services* ... .... Sh. 382,047,200.00
Kif. 1005 - *Information, Education and Communication* .... .... ..... ..... Sh. 1,102,000,000.00
Kif. 2001 - *Government Budget* ... .... Sh. 133,403,887,200.00
Kif. 2002 - *Policy and Research* ... .... Sh. 71,984,460,500.00
Kif. 2003 - *Treasury Registrar* ... ... Sh. 3,063,307,000.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *External Finance* ... .... Sh. 10,182,109,600.00

**WAZIRI WA FEDHA:** Kwenye *Sub-vote* 4001, *External Finance,* kuna masahihisho mawili. La kwanza, linahusu kifungu kidogo cha 250300, *Employment Allowance* badala ya 1.5 bilioni kisomeke 550,450,000, yaani ondoa ile moja. Ondoa ile moja kwenye ile *figure* ya mwisho ile 1.5 futa ile moja. Anza na 570 badala ya 1,570 ondoa ile moja.

Ya pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 280900 ukurasa huo huo pale chini badala bilioni sita sasa isomeke bilioni saba, yaani badala ya sita andika saba na namba nyingine zinabaki sawasawa. Hizi zote zilipitia kwenye Kamati ya Fedha, wanazifahamu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, ile jumla yake pale kwenye kifungu hicho haibadiliki.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Stock Verification* ..... .... Sh. 4,853,598,700.00
Kif. 5002 - *Central Tender Board* .... Sh. 1,716,917,900.00
Kif. 6001 - *Computer Services* ... .... Sh. 1,791,894,000.00
Kif. 6002 - *Tax Revenue Appeals Board* .... Sh. 675,470,900.00
Kif. 6003 - *Technical Audit Unit* .... Sh. 454,431,200.00

Kif. 6004 - *Tax Revenue Appeals Tribunal* Sh. 516,184,600.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3003 - *Financial Management* ... Sh.... 7,773,489,200.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 - *National Audit Office***

Kif. 1001 - *Administration and General* .... Sh.... 1,521,000,000.00

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 2,472,420,000.00
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... Sh. 1,650,000,000.00
Kif. 2001 - *Government Budget* ... ... Sh. 703,353,800.00
Kif. 2002 - *Policy and Research* ... ... Sh. 1,092,864,000.00
Kif. 2003 - *Treasury Registrar* .... ... Sh. 1,021,496,200.00
Kif. 4001 - *External Finance* ... ... ... Sh. 982,883,000.00
Kif. 5002 - *Central Tender Board* ... ... Sh. 3,513,953,000.00
Kif. 6001 - *Computer Services* ... ... ... Sh. 369,290,000,00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2005/2006, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.17 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano Tarehe 20 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*